

**MTAZAMO WA WANAFUNZI WA VYUO VIKUU KUHUSU MATUMIZI YA
LUGHA YA KISWAHILI KATIKA MABANGO YENYE JUMBE ZA UKIMWI**

**BY
MUKOKO ALICE KHAYALI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA
SHAHADA YA UZAMILI**

IDARA YA KISWAHILI NA LUGHA NYINGINE ZA KIAFRINKA

CHUO KIKUU CHA MASENO

©2021

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na wala haijawahi kutolewa popote kwa mahitaji ya shahada yoyote.

Sahihi.....

Tarehe.....

MUKOKO ALICE KHAYALI

(MTAHINIWA)

Sahihi.....

Tarehe.....

DAKTARI BEVERLYNE ASIKO AMBUYO

(MSIMAMIZI)

Sahihi.....

Tarehe.....

DAKTARI DEBORAH AMUKOWA NANYAMA

(MSIMAMIZI)

SHUKRANI

Shukrani zangu za dhati zinamwendea Maulana ambaye ameniwezesha kuikamilisha tasnifu hii ambayo imekuwa na pandashuka zake. Kwa kweli alinipa nguvu, uwezo na neema ili niweze kuikamilisha safari hii.

Shukrani nyingi ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Beverlyne Asiko na Dkt. Deborah Nanyama Amukowa waliojitolea kwa hali na mali kunielekeza kila nilipowahitaji. Nawashukuru kwa kuwa licha ya kuwa na shughuli nyingi waliweza kunihudumia. Walinipa mawaidha na maelekezo ya kitaalamu ambayo yalinifaa sana. Kwa kweli nawaombea Mungu aweze kuwapa afya na awazidishie hekima na neema.

Nawashukuru wahadhiri wangu wote katika Idara ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika ambao wamenielekeza katika kipindi cha usomi wangu hadi nikafikia kiwango hiki. Shukrani zangu za dhati ziwaendee Profesa Florence Indede, pamoja na Dkt. Beverlyne Asiko, Dkt. Deborah Nanyama Amukowa, Dkt. Lumwamu na Dkt. Benard Odoyo Okal.

Nashukuru wasimamizi wa wanafunzi, wakufunzi rika pamoja na wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili katika chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia na chuo kikuu cha Maseno walioshiriki katika utafiti huu. Hakika tasnifu hii haingekamilika bila ya mchango wenu. Aidha, nawashukuru wasomi wa uzamili wenzangu kwa ushirikiano katika masuala ya kiusomi na kijamii. Kwa kweli wamekuwa marafiki wa dhati kwa kunipa moyo. Hawa ni Peter, Florence, Christine, Yunia, Miheso na Ogonda. Mungu awabariki.

Familia yangu imechangia pakubwa ufanisi huu kwa hali na mali. Namshukuru mume wangu mpendwa Martin na watoto wetu Emmanuel, Shalom na Moen.

TABARUKU

Ninaitabarukia kazi hii kwa familia yangu. Mume wangu mpendwa Martin Shem Atemo.
Watoto wetu Emmanuel, Shalom na Moen.

IKISIRI

Mabango yametumika kama njia mojawapo ya kuhamasisha wanafunzi katika vyuo vikuu nchini Kenya kuhusu ugonjwa wa ukimwi. Licha ya haya, ugonjwa huu umeendelea kuwa changamoto kubwa katika vyuo hivi. Aidha utafiti huu ulichunguza mtazamo wa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mabango yenye jumbe za ukimwi ili kubainisha kiwango chao cha uelewaji. Sifa kuu ya mabango ni kupasha ujumbe kwa njia ya haraka na inayoeleweka kwa urahisi. Hali inayosababishwa na namna lugha ilivyotumika katika kuwasilisha ujumbe husika. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa moja, kupambanua fasiri zilizotolewa na wanafunzi kuhusu ujumbe unaowasilishwa na mabango yanayohusu ukimwi, pili kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango hayo, na tatu kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya umitindo (Leech na Short 2007) ambayo ilirejelea viwango vya grafolojia, leksia na semantiki katika kuchanganua mitindo. Nadharia hii ilimwongoza mtafiti kuchanganua fasiri zilizotolewa na wanafunzi, kupambanua mitindo ya lugha pamoja na kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango hayo kwa vijana. Utafiti huu ulitumia muundo mseto. Usampulishaji dhamirifu ulitumiwa kuteua mabango ya matangazo ya ukimwi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili. Mabango 15 yalitumika. Kati ya mabango haya 6 yalipatikana katika chuo kikuu cha Maseno, 7 yalipatikana katika chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia, na 2 yakapatikana katika hospitali kuu ya Kaunti ya Kakamega. Mabango haya yalipigwa picha kutoka sehemu hizo na kuwasilishwa kwa watafitiwa wakati wa majadiliano katika makundi teule. Aidha uteuzi sampuli usioratibiwa ulitumiwa kuteua sampuli ya vijana waliohusika katika utafiti huu. Wanafunzi 106 kutoka chuo kikuu cha Maseno pamoja na wanafunzi 98 kutoka chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia ndiyo walishiriki katika utafiti huu. Data ilikusanywa kuititia mbinu ya uchunzaji na majadiliano ya makundi teule, na kuchanganuliwa na kuwasilishwa kwa asilimia na maandishi yaliyoambatana na picha za mabango. Matokeo ya utafiti yalijadiliwa kurejelea maswala ya utafiti. Makundi teule yalikuwa kumi katika kila chuo kikuu. Vifaa vilivyotumika katika ukusanyaji data ni pamoja na kamera, kinasa sauti, orodha ya uchunzaji na dodoso ya maswali ya majadiliano ya makundi teule. Kutokana na fasiri za watafitiwa utafiti huu ulifichua kuwa mabango ya ukimwi yana wingi wa maana. Aidha mitindo ya lugha ilikuwa kizuizi katika kuelewa ujumbe na hadhira lengwa. Lugha fiche ilitumika kwa minajili ya heshima. Istoshe utafiti huu uliweka wazi changamoto zilizodhihirika watafitiwa walipokuwa wakifasiri ujumbe kwenye mabango ya ukimwi huku zikikisababisha watafitiwa kutofasiri ujumbe jinsi ilivytarajiwa. Utafiti huu utachangia katika utatuzi wa matatizo yanayokumba taaluma ya mawasiliano hasa kuhusiana na suala ibuka la ugonjwa wa ukimwi. Vile vile matokeo ya utafiti huu yataonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi katika kufafanua, kuhamasisha na kufahamisha masuala kuhusu ukimwi hasa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu na umma kijumla.

ABSTRACT

Posters have been used as one of the strategies of creating awareness of the AIDS pandemic among the university students in Kenya. Despite this, the pandemic has continued to be a challenge in these institutions. As a result, this research investigated the perception of the university students in Kenya on the use of Swahili language in the AIDS posters. This was to establish their level of understanding of these messages. The major characteristics of good posters is to communicate quickly and easily. This results from how language has been used to convey these messages. The objectives of this study were: to examine how the students interpret the messages found on AIDS posters; to evaluate the language styles used in these messages and lastly to analyse the challenges experienced by the students in understanding this messages. The research was guided by the stylistic theory (Leech & Short, 2007). The research dwelled on graphology, lexicon and semantics as levels of stylistic analysis. Leech and Shorts stylistic theory helped in evaluating the interpretations given by the youths concerning AIDS messages, analyzing the language styles and evaluating the challenges experienced by the youths in understanding the messages found on this posters. This study employed the mixed method design. Purposive sampling technique was used to sample out AIDS posters written in Swahili language. 15 posters were used. 6 posters were collected from Maseno University, 7 posters were collected from Masinde Muliro University of Science and Technology and 2 posters were collected Kakamega County Hospital. The posters were collected by photography method and were availed to the participants during the focus group discussions. On the other hand, simple random sampling technique was used to sample out the students who participated in this study. A total of 204 students, both of Maseno University and Masinde Muliro University of Science and Technology participated in this study. 106 students were from Maseno University and 98 students were from Masinde Muliro University of Science and Technology. Data was collected by use of observation method and focus group discussions. The data collected was analysed and presented through percentages, narration and photos of AIDS posters. The results of the research were discussed basing on the research questions. The focus groups were 10 from each university. The instruments used to collect the data were: the camera, sound recorder, observation check list and question guides for the focus group discussions. From the focus group discussions, it was discovered that messages on the AIDS posters had several meanings. The stylistic devices used in these messages contributed to the respondent's, failure to interpret the messages as intended. It was also discovered that this type of language was used in order to maintain respect. Either the research was able to expose the challenges experienced by the respondents in understanding these messages. The results of this research will show how the stylistic devices used in these AIDS messages have contributed in one way or another to the misinterpretation of the very messages, thus showing lack of understanding of the messages as intended. This study as a result will play a role in providing a solution to the challenges that affect the communication sector especially in the current situation of AIDS. Either the study will also depict the importance of Swahili as a national and official language in explaining and creating awareness of informing issues concerning AIDS to the university students and public at large.

YALIYOMO

IKIRARI	ii
SHUKRANI.....	iii
TABARUKU	iv
IKISIRI	v
ABSTRACT.....	vi
YALIYOMO.....	vii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa utafiti.....	1
1.2 Suala la utafiti	5
1.3 Maswali ya utafiti	5
1.4 Madhumuni ya utafiti.....	5
1.5 Upeo wa utafiti.....	5
1.6 Umuhimu wa utafiti	6
1.7 Nadharia ya utafiti.....	7
1.7.1 Nadharia ya Umitindo.....	7
1.7.2 Viwango vyta uchanganuzi katika nadharia ya Umitindo	8
1.7.2.1 Kiwango cha Maandishi / Grafolojia.....	8
1.7.2.2 Kiwango cha Kileksia/Mofolojia.....	9
1.7.2.3 Kiwango cha Semantiki	9
1.7.3 Matumizi ya nadharia ya utafiti	10
1.7.4 Hitimisho.....	10
SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDISHI.....	11
2.1 Utangulizi.....	11
2.2 Ufasiri wa ujumbe.....	11
2.3 Mawasiliano kupitia mabango	13
2.4 Mitindo ya lugha	16
2.5 Changamoto zinazokumba matumizi ya lugha ya Kiswahili.....	20
2.6 Hitimisho.....	22
SURA YA TATU: NJIA NA MBINU ZA UTAFITI	23
3.1 Utangulizi.....	23
3.2 Muundo wa utafiti.....	23
3.3 Eneo la utafiti	23
3.4 Kundi lengwa.....	24

3.5 Usampulishaji na Sampuli	24
3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data.....	27
3.6.1 Uchunzaji	27
3.6.2 Majadiliano ya makundi teule.....	28
3.7 Vifaa vya ukusanyaji data.....	29
3.8 Ufaafu wa vifaa.....	29
3.9 Utegemezi na Ukubalifu wa Data	30
3.9 Masuala ya maadili	31
3.10 Hitimisho.....	32
SURA YA NNE: UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI DATA.....	33
4.1 Utangulizi.....	33
4.2 Fasiri za vijana kuhusu ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi	33
4.2.1 Hitimisho.....	50
4.3 Mitazamo ya vijana kuhusu mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi	51
4.3.1 Sitiari.....	51
4.3.2 Mafumbo.....	54
4.3.3 Majazi	63
4.3.4 Methali	64
4.3.5 Kinaya	65
4.3.6 Tasfida.....	67
4.3.7 Kuchanganya Ndimi	70
4.3.8 Taswira.....	76
4.3.9 Taharuki	78
4.3.10 Matumizi ya Sheng	79
4.3.11 Matumizi ya ishara.....	82
4.3.12 Hitimisho.....	84
4.4 Changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.	85
4.4.1 Mitindo ya lugha	85
4.4.2 Maana ya umaanisho.....	89
4.4.3 Kutosoma sehemu zote za ujumbe au mabango	94
4.4.4 Kudharau na kupuuza lugha ya Kiswahili	95
4.4.5 Uhitaji wa ufahamu wa ujumbe wa awali	96

4.4.6 Masuala ya utamaduni	97
4.4.7 Wingi wa maana	97
4.5 Hitimisho.....	101
SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.....	103
5.1 Utangulizi.....	103
5.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti.....	103
5.2.1 Fasiri za vijana kuhusu ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi.....	103
5.2.2 Mtazamo wa vijana kuhusu mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi	104
5.2.3 Changamoto za matumizi ya lugha zilizodhahirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.....	106
5.2.4 Hitimisho.....	108
5.3 Mapendekezo	109
5.3.1 Mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye	110
MAREJELEO	111
VIAMBATISHO	115

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

Matumizi ya mabango ni njia mojawapo muhimu ya kupasha ujumbe. Hutumiwa kuitisha ujumbe kuhusu masuala mbalimbali katika jamii na huwa na majukumu ya kuvutia hisia za hadhira na kuwasilisha ujumbe uliomo. Madhumuni ya kutumia mabango katika kuwasilisha ujumbe ni kuhakikisha kuwa idadi kubwa ya hadhira lengwa inaona, kusoma na kufasiri ujumbe unaopatikana kwenye mabango husika.

1.1 Usuli wa utafiti

Mabango yametumika kama njia mojawapo ya kuwahamasisha wanafunzi katika vyuo vikuu nchini Kenya kuhusu ugonjwa wa ukimwi (WHO 2011). Licha ya haya, ugonjwa huu umeendelea kuwa changamoto kubwa katika vyuo hivi kama inavyodhahirika katika utafiti wa Gakahu (2015). Hali hii inaashiria kuwa aidha huenda wanafunzi katika vyuo vikuu hawajatilia maanani jumbe zinazopashwa kuitia mabango ya ukimwi au hawajaweza kufasiri jumbe hizo jinsi inavyotarajiwa. Iwapo wangetilia maanani jumbe hizi basi changamoto hii ingekuwa imesuluhishwa. Hali hii ndiyo iliyozua haja ya kufanyika kwa utafiti huu ili kuweza kubainisha kiwango chao cha uelewaji wa jumbe hizi. Watafiti wa ugonjwa wa ukimwi nchini Kenya wanadai kuwa wanafunzi wa vyuo vikuu ni mionganini mwa makundi yaliyo katika kiwango cha juu cha hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi (Muturi, 2005). Ueneaji wa ugonjwa wa ukimwi katika chuo kikuu cha Maseno na chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia ni asilimia 10% na asilimia 9% mtawalia. (Local World Health Organization Reference Centre on HIV/AIDS, 2018). Data hii ni ithibati tosha kuwa wanafunzi katika vyuo hivi wameathiriwa na ugonjwa wa ukimwi na hivyo sababu ya utafiti huu kufanyika katika vyuo hivi.

Kulingana na utafiti wa Owino (2004) kuhusu vyuo vikuu Afrika, vikiwemo chuo kikuu cha Maseno na chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia, uhamasishaji wa ujumbe kuhusu ugonjwa wa ukimwi umefanywa kwa kiwango cha juu kuitia mbinu mbalimbali kama vile nyimbo, drama fupi na mabango. Licha ya uhamasishaji huu, ugonjwa huu umeendelea kuwa changamoto mionganini mwa wanafunzi katika vyuo hivi. Aidha mbinu hizi hazijajitosheleza kukabiliana na changamoto hii vikamilifu. Jambo ambalo limetupa msukumo wa kufanya utafiti huu katika vyuo hivi ili kuweza kubainisha jinsi wanafunzi hawa wanavyofasiri jumbe zinazopatikana katika mabango haya.

Mojawapo ya mikakati iliyoteuliwa na Shirika la Afya Duniani (WHO, 2011) katika kuwahamasisha wanafunzi kuhusu ugonjwa wa ukimwi katika vyuo vikuu nchini Kenya ni matumizi ya mabango. Njia hii imejibainisha kama yenyewe uwezo wa kutahadharisha na kudhibiti mielekeo ya binadamu kwa vile lengo lake kuu ni kuzindua, kushawishi, kutahadharisha, kufahamisha, kuelimisha na kurekebisha mielekeo na mitazamo ya binadamu. Mabango ya matangazo ya ukimwi yameangikwa katika maeneo mbalimbali nchini kama vile: vituo vya afya, vyuo vikuu, mijini na kando ya barabara ili ujumbe wake uweze kufikia watu wengi. Kuwasilisha ujumbe fulani kwa jamii kwa njia mwafaka kunategemea sana lugha na ishara (Wamitila 2000). Kulingana na utafiti wa Fish (1970),

msomaji aliweza kufasiri matini kwa njia tofauti kutegemea hisia na tajriba yake ya usomi na maisha. Katika utafiti huu ufasiri wa ujumbe kwenye mabango haya ulitegemea lugha iliyotumika. Mitindo ya lugha iliweza kusababisha fasiri mbalimbali za ujumbe mmoja miongoni mwa wanafunzi. Hali hii iliweza kubainisha kiwango cha uelewaji wa jumbe hizi na wanafunzi katika vyuo vikuu.

Kupitia juhudhi za kuwasaidia wanafunzi wa vyuo vikuu kukabiliana na ugonjwa wa ukimwi, vyuo vikuu nchini Kenya vimeweza kufundisha na kuandaa baadhi ya wanafunzi kuwa wakufunzi rika wa masuala yanayohusiana na ukimwi pamoja na masuala mengine kama vile matumizi ya mihadarati na unywaji ovyo wa pombe (UNESCO, 2009). Wakufunzi rika hawa hutumia mabango ya ukimwi kama nyenzo katika kuwashauri wenzao kuhusu masuala ya ukimwi. Wanafunzi hawa wamekuwa na fursa ya kusoma mabango ya matangazo ya ukimwi mara kadha. Aidha, wanafunzi hawa walifasiri ujumbe kwa njia mbalimbali zinazohitilafiana. Mtafiti anachukulia kwamba maana zinazoibuliwa huweza kuzungukiwa na utata wa ujumbe iwapo matini zitazua zaidi ya fasiri moja. Hivyo basi utoshelevu wa mabango ya matangazo ya ukimwi utategemea ujuzi wa wanafunzi wa kusoma na kujua yanayoelezwa. Hali ya kuchunguza fasiri za maana katika kazi zinahusishwa na wanafalsafa wa Kigiriki kama vile Plato na Aristotle. Hata hivyo, mtazamo wa ufasiri wa maana umeangaziwa zaidi na kazi za mwana falsafa wa Kiswissi, Ferdinand de Saussure, zilizochapishwa baada ya kifo chake mwaka wa 1916. Kazi za mwanafalsafa huyu zimeupa utafiti huu msingi bora.

Luka (2013), katika utafiti alioufanya kuhusu vijikaratasi vya matangazo kuhusu dawa za Antibiotiki, alitambua kuwa lugha iliyotumika ilikuwa changamano kwa msamiati mwingi uliotumika ulikuwa wa taaluma ya Kemia na hivyo ikawa ngumu kwa watumizi wa dawa hizo kuelwa ujumbe kwa njia ya haraka. Matokeo ya utafiti huu yalikuwa ya muhimu kwa vile ndiyo yalichochea utafiti huu kufanyika ili kuweza kubaini namna wanafunzi wa vyuo vikuu wanavyofasiri ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi.

Kulingana na Mutekwa (2013) wasomaji wa mabango hutoa fasiri mbalimbali kwa sababu ya kuelekezwa na mambo kama vile kiwango cha elimu na mtazamo hasi walionao kuhusu lugha ya Kiswahili. Katika utafiti wake ilibainika wazi kuwa kuna baadhi ya watu ambao japo wameelimika hawapendi kusoma mabango ya Kiswahili kwa sababu ya mtazamo hasi walionao kuhusu lugha ya Kiswahili. Wao walichukulia kuwa Kiswahili ni kigumu na hakieleweki kwa haraka. Aidha utafiti wa Mutekwa (2013) ulishughulikia uchanganuzi wa kisemantiki wa mabango ya afya. Ilhali utafiti huu ulichunguza mitazamo ya wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango ya ukimwi na kubainisha wazi namna matumizi haya yamechangia katika kuzua changamoto zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango ya matangazo ya ukimwi kwa wanafunzi hawa.

Mabango ni njia ya mawasiliano ambayo inapasa kuvutia hisia za hadhira na kuwasilisha ujumbe uliomo kwa njia rahisi kueleweka, na si rahisi watu kuepuwa kuyasoma (Cross & Dublin, 2002). Kulingana na Dyer (1982) mabango hutumiwa ili kuhamasisha, kutahadharisha, kushawishi na hata kujuza jamii kuhusu mambo kadhaa, tahadhari kuhusu

ugonjwa wa ukimwi ikiwemo. Anaendelea kusema kuwa ni muhimu kutumia lugha inayoeleweka na wanajamii ndiposa ujumbe huo uweze kuwafikia walengwa. Forman (2009) anashadidia hoja hiyo anaposema kuwa lugha ni muhimu sana katika udhibiti wa usambazaji wa ugonjwa wa ukimwi. Anaendelea kusema kuwa ujumbe ambao umeandalika vyema pamoja na mbinu za mawasiliano huangazia masuala kuhusu ukimwi na hivyo kutapanya uwongo kuhusu ugonjwa huu. Kulingana na Wamitila (2003) mitindo ya lugha hufanya ujumbe uwe wa kuvutia, na wenyenye mnato na msisitizo mkubwa. Agu (2008) anashadidia maoni ya Wamitila anaposema kuwa matumizi ya tamathali za usemi na aina hii ya lugha hutumiwa ili kuyapa matini yaliyoandikwa uzuri, kuweza kutumia maneno machache ipasavyo na kupata uzito wa maudhui. Kutowana na maoni haya ni wazi kuwa ili mabango yaweze kuvutia ni sharti lugha ya mvuto itumike. Lugha hii pia inastahili iwe nyepesi ili yeyote aisomaye aweze kuelewa ujumbe pasipo na usaidizi. Kutowana na matokeo ya utafiti huu ilibainika wazi kuwa mitindo ya lugha imechangia katika kuzua fasiri mbalimbali kuhusu ujumbe mmoja. Hali hii kwa kiwango fulani ilisababisha ujumbe kukosa kueleweka jinsi ilivyotarajiwana hivyo kufanya jukumu la ujumbe huu kukosa kutimika.

Partington (2009) anaeleza kuwa lugha inayotumika kwenye mabango ya matangazo inastahili kuwa na mitindo ya lugha ambayo hunasa nadhari ya hadhira. Jambo hili, kulingana naye limeweza kutekelezwa kwa kutumia kauli zilizotiwa chuku. Kulingana na Leech na Short (2007) mitindo ya lugha hurejelea namna mtu anavyotumia lugha katika muktadha fulani na kwa lengo fulani. Wamitila (2003) anasema kuwa matumizi ya mitindo ya lugha yana umuhimu mkubwa sana katika kufanya ujumbe uwe wa kuvutia na wenyenye msisitizo na mnato mkubwa. Kulingana naye mitindo ya lugha hupunguza ukali au uzito fulani katika lugha. Aidha, utafiti huu ulifichua kuwa matumizi ya mitindo ya lugha ilizua changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa watafitiwa. Changamoto hizi zilisababisha baadhi watafitiwa kufasiri ujumbe kwa namna tofauti na maana tarajiwana. Hali kama hii inapotokea inatupa dhana kuwa matumizi ya mabango haya kama njia ya mawasiliano haijafua dafu. Hii ni kwa sababu lengo kuu la mabango ni kuwasilisha ujumbe kwa idadi kubwa ya hadhira ili iweze kusoma na kufasiri ujumbe husika kwa njia mwafaka bila usaidizi wowote.

Kulingana na Dodd (2007) na Robin (2009) mabango mazuri ni yale ambayo huwasilisha ujumbe kwa njia ya haraka, yanosomeka vizuri, yameandikwa kwa muhtasari, yametumia lugha nyepesi na ni rahisi kueleweka, huangazia mambo muhimu pekee, yanashawishi na yanavutia. Kutowana na maelezo haya ni wazi kuwa mabango yanastahili kuwa na ujumbe mfupi wenyenye lugha ya mnato ambayo ni nyepesi na rahisi kueleweka. Kwa upande mwingine, utafiti huu ulifichua kuwa mabango ya ukimwi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili yalitumia lugha fiche, na hivyo kuchangia katika kuzua changamoto za matumizi ya lugha zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa watafitiwa. Aidha kulingana na Maweja (2002), katika tamaduni nyingi za Kiafrika kuna miiko ya kiisimu ambapo maneno na misemo fulani haikubaliki kutajwa hadharani. Mambo

yanayohusiana na ngono katika jamii nyingi za Kiafrika ni mwiko kuyataja ilihali ndiyo yanayosababisha usambazaji wa ugonjwa wa ukimwi kwa asilimia kubwa.

Toncar na Munch (2001) wanadai kuwa fasiri ni muhimu sana na hivyo inafaa kupewa kipao mbele wakati wa kuwasilisha ujumbe. Kulingana na wao lugha yenyе utata inaweza kuathiri maana inayokusudiwa na ujumbe. Matumizi ya lugha yenyе utata imesababisha mabango ya ukimwi kutowasilisha maana vizuri. Mabango haya yalificha ujumbe sana kwa kuzingatia desturi za adabu za matumizi ya lugha na ishara katika jamii. Suala la ugonjwa sugu wa ukimwi lafaa kuzingatiwa kwa uwazi zaidi kwa vile limefungamanishwa na masuala ambayo jamii nyingi huyaona mwiko kuyataja.

Charon (2009) anadai kuwa watu hufasiri ujumbe kwa njia mbalimbali. Fasiri mbalimbali zaweza kusababisha ujumbe kupata maana tofauti au ujumbe kukosa kueleweka kabisa. Jambo hili linapotokea jukumu la ujumbe huo halijatimilika. Ujumbe kwenye mabango ya ukimwi umefasiriwa kwa njia mbalimbali zinazohitilafiana na hata kusababisha ujumbe huo kupata maana tofauti. Kuwasilisha ujumbe kwa njia mwafaka kwa jamii hutegemea sana lugha na ishara. Hili litaweza kutokea pale tu, maana na ujumbe unaolengwa na mwasilishi unamfikia mpokezi bila utata na upotoshi wa aina yoyote.

Kulingana na BAKITA (2004) kumekuwa na hali ya kudharau lugha ya Kiswahili nchini Kenya na nchini Tanzania. Lugha hii inaonekana kuwa lugha ya watu wa tabaka la chini na hivyo watu wengi hawapendi kunasibishwa na lugha ya Kiswahili. Hali hii pia imejitokeza mionganoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Baadhi yao hawapendi kunasibishwa na lugha ya Kiswahili lakini wanapenda kunasibishwa na lugha ya sheng.

Sheng ni msimbo wa kijamii unaotumiwa hasa na vijana wa mjini na mashambani nchini Kenya. (Ongechi 2002, Shitemi 2001). Sheng huwafanya watu waache kutumia maneno mengine ya Kiswahili wakidhani ni sheng (Okoto 2015). Hali hii inaashiria kuwa sheng hupotosha maana halisi ya maneno katika lugha ya Kiswahili. Utafiti huu umebainisha changamoto zinazoibuliwa na kilugha cha sheng zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe katika matangazo ya ukimwi na watafitiwa. Mtafiti amejaribu kutafuta ni kwa njia gani mabango ya ukimwi yanaweza kuwasilisha ujumbe kwa njia toshelevu. Mtafiti amekusudia kuwa kwa kubainisha wazi changamoto zinazodhihirika katika kueleweka kwa ujumbe kwa wanafunzi wa vyuo vikuu, utafiti huu utachangia katika utatuzi wa matatizo yanayokumba taaluma ya mawasiliano hasa kuhusiana na suala ibuka la ugonjwa wa ukimwi.

Nchini Kenya, lugha ya kiswahili iliratibiwa katika katiba ya mwaka wa 2010 kuwa lugha ya kwanza rasmi na ya taifa. Lugha ya taifa kwa mujibu wa Edwards (1985), ni lugha ambayo ina mvuto wa moja kwa moja hasa kwa kuzingatia misingi ya kimawasiliano na wajibu unaotekeliswa na lugha hiyo katika jamii. Kulingana na Chimera (1998), licha ya kuwepo lugha mbili rasmi nchini Kenya, lugha inayoweza kutumika kiufanisi kuhudumia nchi nzima ni lugha ya Kiswahili kwa vile inatumiwa na Wakenya wengi katika mawasiliano. Hivyo basi lugha ya Kiswahili ina nafasi nzuri ya kuwasilisha habari.

1.2 Suala la utafiti

Licha ya mabango kutumika kama njia mojawapo ya kuwahamasisha wanafunzi katika vyuo vikuu nchini Kenya kuhusu ugonjwa wa ukimwi, ugonjwa huu umeendelea kuwa changamoto kubwa katika vyuo hivi. Matumizi ya mitindo ya lugha katika mabango kuhusu ukimwi yamechangia kusababisha ujumbe huu kufasiriwa kwa njia mbalimbali na hata kuzua changamoto katika kuelewa ujumbe na hivyo kusababisha mabango haya kukosa kuwasilisha ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Ufasiri wa ujumbe hutegemea ubunifu wa mabango katika kuwasilisha ujumbe upatikanao kwenye mabango hayo. Hivyo utafiti huu umechanganya mtazamo wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi.

1.3 Maswali ya utafiti

Utafiti huu umeongozwa na maswali yafuatayo:

- I. Wanafunzi katika vyuo vikuu hufasiri vipi ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi?
- II. Je, mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi hufafanuliwa vipi?
- III. Ni changamoto zipi za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa hawa wanafunzi?

1.4 Madhumuni ya utafiti

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi. Madhumuni yafuatayo yalichangia katika kufikia lengo hili:

- I. Kupambanua fasiri zilizotolewa na vijana kuhusu ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi.
- II. Kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi.
- III. Kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.

1.5 Upeo wa utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza mtazamo wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Mabango yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili kuwasilisha ujumbe kuhusu ukimwi ndiyo yalirejelewa. Mabango haya yalirejelewa kwa sababu lugha ya Kiswahili hutumiwa na watu wengi katika mawasiliano na pia ni lugha ya taifa (Chimera 1998). Mabango 15 ndiyo yalitumika katika utafiti huu. Kati ya mabango haya 6 yaliptaikana katika chuo kikuu cha Maseno, 7 yalipatikana katika chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia 2 yakapatikana katika hospitali kuu ya Kaanti ya Kakamega. Mtafiti alipiga picha mabango haya na kisha kuwasilisha picha hizo kwa watafitiwa wakati wa majadiliano ya makundi

teule. Mtafiti alijikita tu kwa fasiri za wapokezi kwa vile msomaji ndiye ana nafasi ya kusoma, kuelewa na kuchambua maana ya ujumbe unoapatikana kwenye mabango hayo. Wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili pamoja na wakufunzi rika ndio walishirikishwa katika utafiti huu hasa wa cho kikuu cha Maseno na chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia. Wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili walishirikishwa katika utafiti huu kwa sababu ya tajiriba na umilisi wao katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hawa walikuwa na weledi mzuri wa kusoma na kuelewa mabango yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili na waliweza kutambua upungufu uliopatikana katika mabango haya. Kwa upande mwagine wanafunzi amba ni wakufunzi rika walishirikishwa katika utafiti huu kwa sababu wao hutumia mabango ya ukimwi kama nyenzo katika kushauri vijana wenzao kuhusiana na masuala ya ukimwi na hivyo wana nafasi nzuri ya kusoma mabango haya. Wakufunzi rika walioshirikishwa ni wale amba hawasomi kozi ya Kiswahili. Wakufunzi rika hawa waliwakilisha vijana amba hawana tajiriba na umilisi katika lugha ya Kiswahili. Hawa hawajaboea katika lugha ya Kiswahili.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya umitindo (Leech & Short , 2007). Nadharia hii inarejelea viwango vya kileksia, kisintaksia, kilahaja, sajili, kifonolojia, grafolojia, kimapisi, na kisemantiki kama viwango vya uchanganuzi wa mitindo. Utafiti huu ulirejelea viwango vya grafolojia, leksia, na semantiki. Kiwango cha semantiki kilirejelewa katika kupambanua fasiri zilizotolewa na vijana, viwango vya grafolojia, leksia na semantiki vile vile vilirejelewa katika kuchanganua mitindo ya lugha ya Kiswahilii iliyotumika katika mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi, aidha kiwango cha semantiki pia kilirejelewa katika kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.

1.6 Umuhimu wa utafiti

Uteuzi wa mada hii umetokana na utambuzi kuwa ugonjwa wa ukimwi umekuwa changamoto kubwa katika vyuo vikuu nchini Kenya licha ya matumizi ya mabango (Gakahu, 2015). Mabango ni njia ya mawasiliano ambayo inapasa kuvutia hisia za hadhira na kuwasilisha ujumbe uliomo kwa njia rahisi kuelewaka. Si rahisi watu kuepuka kuyasoma (Cross na Dublin, 2002). Ingawa mabango yametumiwa kueleza masuala ya ukimwi, hali ya afya mionganoni mwa vijana, hasa katika vyuo vikuu inazidi kudorora. Hadhira ina jukumu la kufasiri maana ya ujumbe upatikanao katika mabango hayo (White, 1995). Hii ni kwa sababu msomaji ndiye mtu wa mwisho aliye na nafasi ya kusoma na kuchambua maana ya ujumbe kwenye mabango. Hivyo basi, ilikuwa muhimu kufanya utafiti ili kubainisha namna vijana wanavyofasiri ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi, kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango hayo na kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika vijana wanapofasiri ujumbe wa mabango hayo. Mtafiti alizingatia mabango yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili sababu ikiwa lugha ya Kiswahili ni lugha ya taifa na pia hutumiwa na Wakenya wengi katika mawasiliano. Fauka ya hayo mabango kama njia ya mawasiliano yametandazwa kote nchini ili ujumbe uweze kufikia watu wengi.

Utafiti huu umekuwa na nafasi ya kuyaboresha mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi kwa kuweka wazi vikwazo vya mawasiliano mwafaka katika taaluma ya mawasiliano kwa

kudhihirisha fasiri tata za matini kwenye mabango ya ukimwi, pamoja na kubainisha wazi changamoto zinazodhihirika katika kuelewa kwa ujumbe kwa vijana. Utafiti huu umechangia katika utatuizi wa matatizo yanayokumba taaluma ya mawasiliano hasa kuhusiana na suala ibuka la ugonjwa wa ukimwi. Vile vile matokeo ya utafiti huu yameonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa na lugha rasmi katika kufafanua, kuhamasisha na kufahamisha masuala kuhusu ukimwi hasa kwa vijana na umma kijumla. Mabango ni njia muhimu ya mawasiliano ambayo inaweza kutumika katika kuhamasisha vijana kote nchini kuhusu ugonjwa wa ukimwi na hivyo palikuwa na haja ya kufanya utafiti huu ili kutathmini utoshelevu wake kama njia ya mawasiliano.

1.7 Nadharia ya utafiti

1.7.1 Nadharia ya Umitindo

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Umitindo katika kupambanua fasiri zilizotolewa na wanafunzi, kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango ya ukimwi pamoja na kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Nadharia ya Umitindo hujihusisha na uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma ambayo ina uhusiano wa karibu na mtazamo wa kifasihi. Nadharia hii vile vile hueleza jinsi mtu hutumia lugha katika muktadha fulani na kwa lengo fulani. Nadharia hii imeshughulikiwa na wataalamu wengi. Baadhi ya wataalamu hawa ni pamoja na Leech (1969), Crystal na Davy (1981), Lyons (1981), Finch (2000), Simpson (2004), Leech na Short (1981, 2007), Agu (2008) na Wamitila (2008).

Kulingana na Leech (1969) Umitindo ni uhakiki na fasiri ya matini katika mtazamo wa kiisimu kama taaluma, unaofungamanisha uhakiki wa kifasihi na kiisimu ingawa haujisimamii kivyake. Anaendelea kusema kuwa msamiati mpana wa kimsingi wa uhakiki wa kifasihi hususan sitiari, taswira, kinaya, kejeli, usambamba na jazanda hauwezi kufafanuliwa bila kurejelea dhana za kiisimu. Kwa hivyo kama msingi wa kutumia taaluma za kifasihi na za kiisimu, Umitindo ni uwanja ambamo masuala haya hushughulikiwa.

Crystal na Davy (1981) wanasema kuwa Umitindo unalenga kuchanganua sifa za lugha kwa kusudi la kuzitambua kutokana na matumizi kawaida ya lugha na kuziweka katika kategoria kutegemea matumizi ya sifa hizo kimuktadha. Kulingana na wao nadharia ya Umitindo hutafiti na kueleza mitindo ya lugha katika matini kwa kueleza dhima na umuhimu ili kuweza kufasiri ujumbe jinsi inavyostahili.

Lyons (1981) anasema kuwa Umitindo ni uchunguzi wa ubadilishaji wa mtindo katika lugha na jinsi ambavyo watumiaji wake wanavyoutumia. Naye Finch (2000) anaeleza Umitindo kama tawi la Isimu linalotumia njia za kiisimu kuchanganua dhana ya mtindo katika lugha.

Leech na Short (2007) wanaeleza kuwa nadharia ya Umitindo huangazia umuhimu wa lugha katika kueleza maana ya matini, na pia hutumiwa kurejelea jinsi lugha inavyotumiwa katika muktadha fulani na kwa lengo fulani. Kulingana na Leech na Short (2007) malengo ya stadi za Umitindo ni fasihi pamoja na maumbo mengine ya matini. Umitindo hujaribu kubainisha

kanuni za kueleza uteuzi uliofanywa na mwandishi katika matumizi yake ya lugha kuhusu mambo ya kijamii, utoaji na upokeaji wa maana, uhakiki wa kidiskosi na wa kifasihi. Kwa mujibu wa Leech na Short (2007) nadharia ya Umitindo ina viwango ambavyo humwezesha mchanganuzi wa matini kuvizingatia ili kutekeleza uhakiki kwa njia inayofaa. Wataalamu hawa wameweza kuorodhesha aina za ukiushi wa kaida za matumizi ya lugha ambaeo hutokea katika mtindo wa kazi za fasihi na hata matini mengine. Viwango hivi vya ukiushi ni kama vifuatavyo: *ukiushi wa kimsamiati/kileksia, ukiushi wa kisaruft/sintaksia, ukiushi wa kilahaja ukiushi wa sajili, ukiushi wa kifonolojia, ukiushi wa kimaandishi/kigrafolojia, ukiushi wa kimapisi /kihistoria na ukiushi wa kisemantiki*.

Agu (2008) anasema kwamba nadharia ya Umitindo inajumlisha uchunguzi wa sintaksia, uteuzi wa maneno, nahau, taswira na mengine. Anaeleza kuwa katika kiwango cha kisintaksia unahuishisha miundo ya sentensi, uteuzi wa maneno na jinsi yanavyopangwa ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa. Anaendelea kusema kuwa Umitindo pia unahuishisha matumizi ya tamathali za usemi na aina hii ya lugha hutumiwa ili kuyapa matini yaliyoandikwa uzuri, kuweza kutumia maneno machache ipasavyo na kupata uzito wa maudhui.

Wamitila (2008) pia ameeleza kuhusu nadharia hii ya Umitindo. Anasema kuwa Umitindo hutumiwa kurejelea mkabala wa uchanganuzi unaohusisha manufaa ya Isimu na huweza kueleza kama nadharia ambayo iko katikati ya Isimu na Fasihi. Anaendelea kusema kuwa kimsingi nadharia hii ina mwelekeo wa kifani na inadhamiria kuchunguza mitindo katika matini. Msingi wa nadharia ya Umitindo kulingana na Wamitila (2008) ni nadharia ya balagha. Nadharia ya Balagha ilikuzwa na kuendelezwa katika jadi ya Kiyunani na Kirumi ambayo ilithamini jinsi ya kuzungumza au kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kimaandishi. Wamitila anaendelea kueleza kuwa nadahria hii inajikita kwenye uchunguzi wa lugha kwa kiasi kikubwa. Uchunguzi huu wa lugha unapania kubainisha ubunifu uliopo na kuutekeleza kwa undani na unasaidia katika uelewaji wa matini.

1.7.2 Viwango vya uchanganuzi katika nadharia ya Umitindo

Utafiti huu ulirejelea viwango vya uchanganuzi katika nadharia ya Umitindo kwa kurejelea mtazamo wa Leech na Short (2007). Kama wanavyoelezea Leech na Short (2007) kuna viwango vingi vya kuchunguzwa katika matini kwa kutegemea nadharia ya Umitindo. Utafiti huu ulirejelea viwango vifuatavyo:

1.7.2.1 Kiwango cha Maandishi / Grafolojia

Kiwango hiki pia huitwa kiwango cha utendaji. Kiwango hiki kinahusu vipengele vya kigrafolojia. Kiwango hiki kinahusu jinsi lugha inavyotamkwa na kuandikwa. Ukiushi wa kiwango hiki unahusu kubadilisha matamshi ya maneno, matumizi ya herufi kubwa kwa njia isiyo ya kawaida; kutumia herufi ndogo mahali pa herufi kubwa, matumizi ya herufi za mlazo na matumizi ya viwakifishi kama koma, alama hisi, koloni na vistari. Leech na Short (2007) wanasema kuwa matumizi ya vipengele hivi vya kigrafolojia katika maandishi huwa na athari ya uchimuzi. Wanafafanua uchimuzi kama dhana yenye maana ya matumizi ya mbinu za kimuundo zinazokiuka uandishi wa kawaida kwa lengo la kukifanya kipengele

fulani kionekane zaidi ya kingine. Ogsiji (2007) anasema kuwa kando na matumizi ya maneno, mwandishi anaweza kutumia alama zingine zisizo maneno katika kuiendeleza kazi yake, na kwamba alama hizi zisipuuze kwa vile huwa zimebeba ujumbe fulani na hivyo huwa na athari fulani kwa msomaji wa ujumbe huo. Kulingana na Lodge (2009) fonolojia inahusu utaratibu wa mpangilio wa sauti katika msamiati wa lugha. Anaendelea kusema kuwa kila lugha ina utaratibu wake wa mpangilio wa sauti ambao unatumika kuunda mofimu ambacho ni kipashio kidogo kabisa cha maana katika neno. Kiwango hiki kiliufaa utafiti wetu kwa vile kiliongoza utafiti kuchunguza vipashio vyta kigrafolojia vinavyopatikana katika mabango ya ukimwi na jinsi vinavyochangia kuzua changamoto katika matumizi ya lugha ya Kiswahili.

1.7.2.2 Kiwango cha Kileksia/Mofolojia

Matumizi ya lugha kwa kawaida huhusisha uteuzi wa maneno au msamiati maalumu. Kiwango hiki huchunguza maumbo ya maneno, hushughulikia uambishaji, mwambatano, ufupisho, akronimu, uhulutishaji, tafsiri mkopo, utohozi, onamotopea, polisemia, urudifishaji na aina za maneno yalivyo sasa pamoja na historia zao. Kiwango hiki pia huhusu kuchanganya ndimi, kuhamisha ndimi na matumizi ya maneno ya kigeni kama Kiingereza au Kilatini (Cyrstal 2008). Kiwango hiki kiliufaa utafiti kwa kupeana dira katika kuchanganua maumbo ya maneno yanayopatikana katika mabango ya ukimwi, na namna maumbo hayo yalivyochangia katika changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa watafitiwa kwa kurejelea fasiri zao.

1.7.2.3 Kiwango cha Semantiki

Kulingana na Leech na Short (2007) semantiki ni sayansi ya maana. Huchunguza maana katika lugha. Maana ya maneno huchunguza kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Kuna maana elekezi na maana ya umaanisho. Maana elekezi ni maana inayotokana na kule kuonyesha kwa kuelekeza kwa kitu kinacholengwa, na maana ya umaanisho ni ile ambayo mtu husema kitu na kumaanisha kitu kingine. Kulingana na wao kiwango hiki hushughulika na uchunguzi na uchananzi wa maana za maneno kutokana na uhusiano wa maneno katika muundo wa tungo za lugha inayohusika. Wanaendelea kusema kuwa huchunguza maana ya kimuktadha kuhusiana na maana ya kimsingi. Kutokana na maana msingi, maneno huhusishwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani kimsingi. Kiwango hiki pia kinahusu lugha ya kitamathali na miundo ya lugha ambayo ni sifa muhimu ya kuchunguza matini tunapotumia nadharia ya Umitindo. Ni jinsi matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Ukiushi wa kiwango hiki unahusu matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali za kawaida. Aghalabu huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huwepo matumizi ya tamathali za usemi, mbinu za kinaya, kejeli, kweli-kinzani, sitiari, jazanda, tabaini, taswira, chuku, maswali ya balagha n.k. Kiwango hiki kiliongoza utafiti huu kupambanua mitazamo ya vijana kuhusu mitindo ya lugha ya Kiswahili ambayo imetumika katika mabango ya ukimwi. Kiwango hiki pia kiliongoza utafiti kutathmini namna mitindo hiyo inavyochangia katika kuzua changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhihirika katika kuelewa kwa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.

1.7.3 Matumizi ya nadharia ya utafiti

Utafiti huu umetumia nadharia ya umitindo (Leech na Short 2007). Kiwango cha semantiki cha kilitumika katika kuongoza utafiti kuchunguza madhumuni ya kwanza ambayo yalikuwa ni kupambanua fasiri zilizotolewa na vijana kuhusu ujumbe unaopatikana kwenye mabango ya ukimwi. Aidha viwango vya grafolojia, leksia na semantiki vilitumika katika kuongoza utafiti kuchunguza madhumuni ya pili ambayo ni kuchanganua mitindo ya lugha ya Kiswahili iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi. Isitoshe, kiwango cha semantiki pia kilitumika kuongoza utafiti kuchunguza madhumuni ya tatu ambayo yalikuwa ni kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa watafitiwa. Nadharia hii ilitumika kuongoza utafiti huu katika kutekeleza madhumuni yake.

1.7.4 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia usuli wa utafiti kwa kueleza hali ilivyo kuhusu suala nzima la ukimwi mionganini mwa vijana katika vyuo vikuu nchini Kenya. Sura hii pia imeonyesha kuwa lugha ni kipengele muhimu katika kuwasilisha masuala kuhusu ukimwi. Maeleo pia yametolewa kuonyesha kuwa mabango ni njia mojawapo muhimu ya kuwasilisha ujumbe wa ukimwi kwa wanajamii. Mbali na haya mwelekeo uliochukuliwa na utafiti umeelezwa mintarafu madhumuni na maswali ya utafiti. Sura hii pia imeweka wazi kiunzi cha dhana kilichoelekeza utafiti huu. Sura hii imetupa msingi wa kuhakiki maandishi mintarafu malengo ya utafiti kama ilivyoshughulikiwa katika sura ya pili ifuatayo.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI

2.1 Utangulizi

Sehemu hii inahakiki maandishi mbalimbali yanayohusiana na matumizi ya lugha. Ili kuchunguza suala hili vipengele mbalimbali vilishughulikiwa. Vipengele hivi ni pamoja na ufasiri wa ujumbe, mawasiliano kuitia mabango, mitindo ya lugha na changamoto zinazokumba matumizi ya lugha ya Kiswahili, nadharia ya mwingiliano kiishara na nadharia ya umitindo. Kwa kufanya hivyo tulichunguza michango, mitazamo na mapendekezo ambayo yaliwahi kutolewa kuhusu matumizi ya lugha ili kuonyesha pengo lililoachwa.

2.2 Ufasiri wa ujumbe

Kufasiri ni ile hali ya kutoa maana ya jambo lililofichika, ni kufafanua maana ya ujumbe (TUKI 2004). Ufasiri ni dhana muhimu sana katika mawasiliano. Ili mawasiliano yatimilike vyema ni lazima ujumbe ufasiriwe vyema na anayepokea ujumbe huo. Mawasiliano, kwa mujibu wa Murray (2005) ni ile hali ya kutoa, kupokea au kubadilishana ujumbe, maoni au mawazo kwa njia ya maandishi, maongezi au kwa kutazama. Mawasiliano husemakana yamefanikiwa iwapo ujumbe unaotumwa unapokelewa na kueleweka inavyohitajika. Ujumbe wowote ule hauwezi kuwasilishwa na kufikia hadhira bila ya kuwako kwa lugha. Jinsi lugha inavyotumika huathiri namna msomaji atakavyosoma na kufasiri ujumbe wowote ule.

Fish (1970), alichunguza maoni mbalimbali ya wanafunzi ili kubainisha jinsi walivyofasiri wahusika katika ngano walizosoma. Kulingana na Fish kila msomaji aliifasiri matini kwa njia tofauti kutegemea hisia na tajriba yake ya usomi na maisha. Makala haya yanadhihirisha kuwa kila msomaji huipokea na kuifasiri matini kwa njia tofauti kutegemea hisia na tajriba yake ya usomi na maisha. Aidha Fish anaendelea kueleza kuwa uwezekano wa akili ya msomaji kufanya kazi inapokutana na matini huegemea kwenye misingi ya kijamii. Yaani akili ya msomaji haiwezi kufanya kazi ya kufasiri matini bila kuathiriwa na misingi ya kijamii. Utafiti uliofanywa na Fish (1970) ni muhimu sana kwa utafiti wetu kwa vile aliweza kuchunguza namna wanafunzi walivyotoa fasiri tofauti tofauti kuhusu makala waliyoisoma. Tofauti iliyoko ni kuwa Fish alichunguza jinsi wanafunzi walivyofasiri wahusika katika ngano walizosoma na utafiti wetu ulichunguza jinsi wanafunzi walivyofasiri ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi.

Iser (1974) naye anaeleza kuwa muktadha wa msomaji, ufaamu wake, mazingira yake, pamoja na sifa zinazomzunguka huathiri maana atakayoipa kazi ya fasihi. Leech na Short (2007) nao wanatilia mkazo mawazo haya wanaposema kuwa maana ya maneno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Isitoshe, Charon (2009) anadai kuwa binadamu hufasiri ujumbe kulingana na ufaamu wake. Mawazo ya wataalamu hawa yaliuwekea utafiti huu misingi katika kuchanganua fasiri zilizotolewa na wanafunzi kuhusu ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi kwa kuzilinganisha na muktadha husika.

Aidha kulingana na Tompkins (1980), maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri namna ambavyo ataifasiri matini. Msomaji huongozwa na asili ya mielekeo na maadili yake, kwa hivyo matini ile ile inaweza kufasiriwa kwa njia tofauti na wasomaji tofauti au ikafasiriwa kwa njia tofauti na msomaji yule yule ikiwa ataisoma kwa kipindi tofauti. Mawazo haya ya Tompkins yalikuwa na mchango kwa utafiti wetu kwa vile utafiti wetu ulichunguza namna tajiriba aliyonayo mtafiti katika lugha ya Kiswahili iliathiri namna alivyofasiri ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi.

Tucker (1981) anasema kuwa ufasiri hutegemea hali ya kisaikolojia ya msomaji. Kwani fasiri huweza kutofautiana ama kulingana baina ya wasomaji wawili tofauti kutegemea tajiriba zao maishani. Msomaji anaweza kuifasiri kazi ya fasihi kulingana na tajiriba yake ya maisha au usomaji. Mielekeo ya kibinagsi pia ina athari kubwa kuhusu namna msomaji hupokea kazi fulani. Mawazo haya ya Tucker (1981) yaliuwekea utafiti wetu msingi katika kuchanganua fasiri zilizotolewa na wanafunzi kuhusu ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi kwa kuzilinganisha na tajiriba zao katika lugha ya Kiswahili.

Barthes (1984) katika utafiti alioufanya kuhusu matangazo ya biashara aligundua uwepo wa fasiri tata na polisemi za maana katika matangazo ya biashara na akapendekeza matumizi ya lugha elekezi inayo ambatana na misingi ya jamii husika. Polisemia ni hali ambapo maneno huwa na maana zaidi ya moja (Habwe & Karanja, 2004). Aidha Barthes anaendelea kudokeza kuwa, lengo kuu la kuhakiki matini ni kuivunja katika sehemu ndogo alizozia leksia. Hivi ni kama vitengo vidogo vya usomaji vinavyodhihirisha misimbo au kanuni fulani ambazo huwa muhimu katika kuifasiri kazi fulani. Utafiti wa Barthes (1984) uliwekea msingi utafiti wetu kwa vile alichunguza ufasiri wa lugha katika matangazo ya biashara, tofauti iliyoko ni kuwa utafiti wetu ulizingatia matangazo ya mabango ya ukimwi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili.

Kulingana na Witte (1992) watu wawili wanaweza kufasiri ujumbe kwa njia tofauti kabisa kwa sababu ya tajiriba tofauti ya maisha, tamaduni tofauti na mitazamo tofauti kuhusiana na ujumbe mmoja. Mawazo haya yalikuwa na umuhimu mkubwa kwa utafiti wetu kwa vile yalitupatia mskumo wa kubaini sababu za uwepo wa fasiri tofauti tofauti mionganoni mwa watafitiwa kwa kutathmini changamoto zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango ya ukimwi kwa wasomaji.

Tanaka (1994) alitathmini utata katika matangazo unaoweza kuibua farakano kati ya hali halisi mionganoni mwa hadhira na jamii kwa jumla kutokana na fasiri potovu. Kulingana naye fasiri potovu zilikuwa na mchango hasi katika jamii na hivyo kusababisha kutengana kwa wanajamii. Fasiri potovu ni ishara ya ujumbe kukosa kufasiriwa jinsi ilivyotarajiwa. Matokeo ya utafiti huu yaliuwekea msingi utafiti wetu kwa vile yalitupatia msukumo wa kutathmini changamoto zinazosababisha fasiri potovu.

Andrew Bennet na Nicolas Royle (1995) wanashadidia mawazo ya Fish (1970) wanaposema kuwa jamii hushiriki mfumo wa kanuni na taratibu zinazokubalika na jamii husika. Jamii moja huweza kutumia ishara za aina sawa na kuelewana katika ufasiri wa maana na ujumbe. Hata hivyo ufasiri hutofautiana kwa watu binagsi. Aidha kama wasemavyo wahakiki wa chuo

kikuu cha Yale,- Geofrey Hartman, Hills Miller, Paul De Mann na Harold Bloom, kuna uwezekano wa matini kuwa na fasiri nyingi zilizolingana au kukinzana na zote zikakubalika (Blamires 1991). Mawazo ya wataalamu hawa pia yaliuwekea utafiti wetu msingi kwa kutuwezesha kubaini namna misingi ya kijamii ilivyoathiri fasiri zilizotolewa na vijana kuhusu ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi.

Yakub (2008) alichunguza matangazo ya kibiashara ya mtandao wa Safaricom. Katika utafiti wake alielezea utaratibu wa kuzingatiwa wakati wa kufasiri matangazo ya kibiashara ya mtandao wa Safaricom kwa vile lugha hufinyangwa na ishara za kisanii zisizofahamika na wasomaji. Utafiti huu ulikuwa wa manufaa kwa utafiti wetu kwa vile tulichunguza uwepo wa matumizi ya ishara za kiisimu zisizofahamika na wanafunzi wa chuo kikuu kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi ambazo zilisababisha changamoto katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.

2.3 Mawasiliano kupitia mabango

Bango ni kazi sanifu ambayo ina lengo la kuwasilisha ujumbe kupitia hisi ya kuona. Samovar (1995) anaongeza kwa kusema kuwa kutumia hisi ya kuona katika mawasiliano ni muhimu sana kwa sababu watu huhifadhi asilimia ishirini ya wanachokisikia na asilimia hiyo huongezeka hadi asilimia hamsini mawasiliano yanapohusisha hisi ya kuona na kusikiliza. Njia mojawapo ya kutoa matangazo ni kupitia mabango.

Kulingana na White (1995) madhumuni ya kutumia mabango wakati wa kutangaza ni kuhakikisha kuwa idadi kubwa ya hadhira lengwa inaona, kusoma na kufasiri ujumbe upatikanao kwenye mabango hayo mara kwa mara. Aidha anaendelea kusema kuwa lengo kuu la mabango ni kuathiri mitazamo, kuuza bidhaa na huduma au kubadilisha mienendo ya watu. Kulingana naye mabango ya ukimwi yamo katika kategoria ya tatu, kwani lengo lao ni kubadilisha mienendo ya umma ili kuinua kiwango chao cha afya. Kutokana na maelezo haya utafiti huu umeweza kupambanua mtazamo wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha kwenye mabango yanayohusu ukimwi. Crystal (1996) anasema kuwa hatuwezi kuepuka matangazo ya mabango kwa sababu tunakutana nayo tunapotembea na hutundikwa sehemu ambazo watu wengi huzuru.

Kuna aina mbalimbali za mabango. Kuna yale yaliyo na maandishi tu, mengine huwa na picha tu na mengine huwa na maandishi pamoja na picha (Dodd, 2007). Mabango hupitisha ujumbe kuhusu masuala mbalimbali katika jamii na huwa na majukumu ya kuvutia hisia za hadhira na kuwasilisha ujumbe uliomo. Kwa mujibu wa Dodd (2007) mabango mazuri ni yale ambayo yana maandishi yanayosomeka vizuri na yaliyoandikwa kwa muhtasari, na huangazia tu mambo muhimu pekee yake.

Robin (2009) anasema kuwa tafiti nyingi zimeonyesha kuwa ni nadra sana kwa watu kutumia zaidi ya dakika tano kusoma mabango. Anaendelea kusema kuwa aghalabu watu huchukua tu dakika moja kuyasoma mabango iwapo watasimama kuyasoma kwa vile hawana muda wa kusoma. Wataalamu wa afya kwa umma wameweza kutambua kuwa mawasiliano kupitia mabango yanayohusiana na masuala ya afya ni njia mwafaka ya kuwasilisha ujumbe wa afya kwa umma. Kampeni kupitia mabango haya zimewezesha wataalamu hawa kuwasilisha

ujumbe wa afya kwa umma kuhusu afya yao (Cooter na Stein, 2010). Mawazo ya wataalamu hawa yaliuwekea utafiti wetu msingi thabiti. Mabango ya ukimwi ni mojawapo ya mabango ya afya. Mbali na ujumbe wa afya kuwasilishwa kwa umma kupitia mabango, kulikuwepo na haja ya kufanya utafiti ili kuchunguza namna ujumbe huo unavyofasiriwa na wapokezi. Hii ni kwa sababu mpokezi ndiye anayekuwa wa mwisho kuzingatia yaliyomo kwenye ujumbe baada ya kusoma, kwani wasomaji ndio wanaostahili kufanya juhudini kupata na kusimbua maana iliyosimbwa. Kiwango cha uelewaji wa ujumbe fulani hutegemea namna ujumbe huo ulivyowasilishwa. Kukosa kukuza ujumbe uliowazi kwenye kampeni yoyote ile huambulia patupu iwapo hadhira lengwa itashindwa kuelewa ujumbe kulingana na uwezo wao.

Mabango ni njia mojawapo muhimu ya kuwasilisha ujumbe kuhusu masuala ya ukimwi. Mabango haya huwa na majukumu ya kuvutia hisia za hadhira na kuwasilisha ujumbe uliomo.

Ingawa Cross na Dublin (2002) wanadai kuwa mabango hunasa na kuhifadhi nyoyo, hisia na akili za walengwa na hivyo si rahisi watu kuepuwa kusoma ujumbe unaopatikana katika mabango hayo, ugonjwa wa ukimwi umeendelea kusambaa kwa haraka sana hasa mionganoni mwa vijana katika vyuo vikuu nchini Kenya, licha ya mabango kutumiwa katika kuwasilisha ujumbe kuhusu ukimwi. Utafiti huu umechunguza na kuweza kubaini namna vijana wanavyofahamu ujumbe kwenye mabango haya kwa kerejelea fasiri zao.

Utafiti wa Ward & Hawthorne (1995) ulichunguza iwapo wagonjwa husoma mabango wakiwa hospitalini wanaposubiri kuhudumiwa. Matokeo ya utafiti wao ni kuwa wagonjwa wengi husoma na hukumbuka ujumbe wa mabango hayo. Vile vile walitambua kuwa mabango yanaweza kutumika kama njia ya uhamasishaji kuhusu masuala ya afya. Matokeo ya utafiti wao yameuwezesha utafiti huu kuchunguza namna ujumbe usomwao katika mabango kuhusu ukimwi na ulioandikwa katika lugha ya Kiswahili unavyofasiriwa na vijana.

Ombogi (2003) alichunguza matangazo katika magazeti yaliyochapishwa nchini Kenya, na aliweza kuonyesha jinsi matangazo hayo yalivyotumia lugha shawishi. Utafiti wetu ultathmini mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mabango yanayotoa matangazo kuhusu ukimwi ili kutambua mitindo ya lugha iliyotumika katika mawasiliano hayo na namna mitindo hiyo inavyochangia kuzua changamoto zilizodhihirika vijana walipofasiri ujumbe huo.

Bankole, Aderinokun na Denloye (2005) wanasema kuwa mabango ya picha pekee katika mahali pa kazi hayakuweza kubadili mtazamo wa watu kuhusu changamoto fulani za kiafya. Wanasema kuwa mabango yalikuwa na athari wakati yalipotumika katika maingiliano ya wanajamii. Wanaendelea kudai kuwa mbinu ya kutengeneza mabango pasipo na kuzingatia namna yatakavyotumika itafanya mabango hayo kutotimiza lengo. Kulingana nao mabango lazima yawe wazi ili yaweze kueleweka vema bila usaidizi wowote, yaweze kuvutia macho, na yaangikwe mahali ambapo hadhira lengwa yaweza kuyaona. Isitoshe, mabango haya yaweze kubadilishwa mara kwa mara, la sivyo itafika wakati ambapo watu hawatakuwa wakiyatambua. Wanaendelea kusema kuwa ni vema mabango yote yaundwe na kuchorwa kwa uangalifu mkubwa kisha kufanyiwa majoribio awali kwa kundi lengwa. Utafiti huu

ulikuwa na mchango mkubwa katika utafiti wetu kwani ulitupatia msingi kuwa kila bango hutengenezwa kutimiza lengo fulani.

Kimani (2006) katika utafiti wake, aliweza kuchanganua uwiano wa maana za picha na matini katika mabango ya matangazo ya ukimwi kwa kurejelea mtazamo wa kisemiotiki. Utafiti huo uligundua kuwa uwiano wa picha na matini katika mabango ya ukimwi ulimwekeea mfasiri mipaka na kuathiri namna anavyofasiri ujumbe. Matokeo ya utafiti wa Kimani yalichangia katika utafiti huu kwa kumwezesha mtafiti kuchunguza namna vijana wanavyofasiri ujumbe upatikanao katika mabango hayo. Tofauti iliyopo kati ya utafiti wetu na wa Kimani (2006) ni kuwa utafiti wake ulishughulikia uwiano wa picha na matini ilihali wetu ulijikita katika mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango haya.

Hashim (2010) katika utafiti wake, alishughulikia uchaguzi wa lugha, ubadilishaji misimbo na kuchanganya misimbo pamoja na dhima ya lugha ya Kimombo katika mabango ya matangazo ya biashara kule Malaysia. Kulingana naye, kando na mabango ya biashara kutumia lugha shawishi, uchaguzi wa aina ya lugha itumiwayo katika mabango haya huzingatiwa sana wakati wanapowasiliana na jamii zenye uwili lugha na wingi lugha. Kule Malaysia, Hashim (2010) anaeleza kuwa mitindo ya lugha ya kuchanganya na kubadilisha misimbo imeathiri sana lugha ya Kiingereza sanifu kwani lugha ya Kiingereza imechanganywa na lugha ya Kimalaysia. Utafiti huu umetofautiana na utafiti wetu kwa vile sisi tumejikita katika mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi na wala si matumizi ya lugha katika matangazo ya biashara. Hata hivyo utafiti huu umekuwa wa mchango kwa utafiti wetu kwa vile umetathmini uwepo wa matumizi ya mitindo ya lugha ya kuchanganya na kubadilisha misimbo kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi na namna mitindo hii imeathiri lugha sanifu ya Kiswahili.

Cook (2013) katika utafiti wake kuhusu mabango ya biashara kule Uingereza, anasema kuwa matangazo ni kiwakilishi cha diskosi maalumu ambapo lugha na ishara ina jukumu la kushawishi, kuhamasisha, kuburudisha na kutahadharisha watu. Anaendelea kusema kuwa matumizi ya mitindo ya lugha katika mabango hayo huathiri na kubadilisha mawazo ya watu na kuwafanya hata wanunue bidhaa ambazo hawahitaji, kwani mabango hayo ya biashara hutumia lugha iliyo na utajiri mwangi wa mapambo ya lugha kama mbinu ya kuwavutia wateja. Utafiti huu wa Cook (2013) umekuwa na mchango mkubwa kwa utafiti wetu kwa vile utafiti wetu umejikita vile vile katika kuchanganua mitindo ya lugha ambayo imetumika katika mabango ya ukimwi.

Kulingana na utafiti wa Mutekwa (2013) kuhusu uchanganuzi wa kisemantiki wa mabango ya Kiswahili kuhusu suala la afya kuna watu ambao japo wameelimika hawapendelei kusoma mabango ya Kiswahili. Kwani wana mtazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili. Mtazamo huu umeathiri namna wanavyofasiri ujumbe unaopatikana katika mabango ya Kiswahili ya afya. Utafiti wa Mutekwa umeweza kuchochea utafiti huu. Sababu ni kuwa matokeo ya utafiti huo yamechangia katika kuchunguza namna fasiri mbalimbali

zinazojitokeza katika mabango huchangia kuzua changamoto zinazodhihirika katika uelewaji wa ujumbe upatikanao katika mabango yanayohusu ukimwi na vijana.

Sharndama (2013) alichanganua vipengele vya kiisimu kwenye mabango ya siasa kwa kutumia nadharia ya umitindo. Utafiti huu ulibainisha kuwa mabango ni mbinu muhimu sana ya mawasiliano ambayo hutumiwa na wagombeaji katika kuwasilisha ujumbe. Kwani mabango haya yalishawishi wananchi na kuathiri maoni yao. Kulingana na utafiti wa Sharndama, katika kiwango cha leksia msamiati huchaguliwa kwa umakini mkubwa. Msamiati huo huwa wenyewe kuamsha hisia za hadhira lengwa ili kuwafanya kuunga mkono wagombeaji hao. Sintaksia iliyotumika katika sentensi hizi ilikuwa sahili na nyepesi kueleweka. Matumizi haya ya lugha husababisha hadhira kubwa kuweza kuelewa ujumbe katika mabango haya. Matokeo ya utafiti wa Sharndama yalikuwa na mchango mkubwa kwa utafiti huu kwa vile utafiti huu ulichanganua namna watafitiwa wanavyoolewa ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi kwa kurejelea fasiri zao.

Luka (2017) alitumia nadharia ya umitindo katika kuchanganua ujumbe kwenye vijikaratasi vya matangazo kuhusu dawa za Antibiotiki. Luka alichanganua ruwaza ya mfangamano ya mfumo wa sarufi kuanzia kiwango cha neno hadi kiwango cha sentensi. Utafiti huu ulishughulikia muundo wa sintaksia katika undaji wa sentensi katika ujumbe unaopatikana kwenye vijikaratasi hivi. Sababu ni kuwa lugha ina nafasi muhimu katika kuwasilisha ujumbe kuhusu maarifa ya jinsi ya kutumia dawa hizo. Kupitia utafiti huu ilitambulika kuwa lugha iliyotumika ilikuwa changamano kwa vile msamiati mwangi uliotumika ulikuwa wa taaluma ya Kemia. Utafiti huu ulipendekeza matumizi ya lugha nyepesi inayoeleweka haraka na watumizi wa dawa hizo. Matokeo ya utafiti wa Luka yalikuwa ya muhimu kwa utafiti huu kwa vile utafiti huu ulichunguza mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi kwa kutathmini namna watafitiwa wanaelewa maana za ishara za kiisimu zilizotumika kuusimba ujumbe kwa kutumia nadharia ya umitindo.

2.4 Mitindo ya lugha

Lugha ndiyo nyenzo kuu katika mawasiliano. Ujumbe wowote hauwezi kuwasilishwa na kufikia hadhira bila ya kuweko kwa lugha. Jinsi lugha inavyotumika huathiri namna msomaji atakavyosoma na kuelewa ujumbe wowote ule. Kupitia lugha watu hubadilishana habari, maana na hisia. Uchunguzi wa matumizi ya lugha yoyote ile hujumuisha mitindo mbalimbali. Hivyo basi mitindo ya lugha hujitokeza katika miktadha maalumu kama ilivyobainika katika utafiti huu kuhusu mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Mtindo ni upekee wa kujieleza katika maandishi au mazungumzo. Ni jinsi waandishi huandika na pia ni njia tofauti za watu wanavyozungumza au kuandika katika miktadha ya kawaada ya kila siku. Mtindo unaweza kuhuishwa na lugha ilioandikwa, lugha ya kifasihi na isiyokuwa ya kifasihi.

Kulingana na Leech na Short (2007) mitindo ya lugha hurejelea namna mtu anavyotumia lugha katika muktadha fulani na kwa lengo fulani. Aidha wanasema kuwa kiwango ambacho tunaweza kuanza kuchanganua mitindo chawenza kuwa matini nzima au sehemu ya kazi

fulani. Crystal na Davy (1985) nao wanafafanua mitindo ya lugha kama sifa maalumu za mwandishi au mazoea ya mwandishi fulani kujionyesha kwenye fani yake. Wanaendelea kusema kuwa mazoea hayo ya mwandishi ya kuandika, kuteua msamiati, tamathali za usemi, taswira, uakifishaji, sentensi miongoni mwa mengine humpambanua mwandishi kutoka kwa waandishi wengine. Kwa mujibu wa haya utafiti huu ultathmini mtazamo wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu mitindo ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi.

Kulingana na Wamitila (2003) mitindo ya lugha ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuuwasilisha ujumbe wake. Dhana hii inarejelea sifa maalumu za maandishi. Sifa hizi ni kama vile: tashhis, sitiari, tashbihi, chuku, methali, tasfida, kinaya, dhihaka, tabaini, maswali ya balagha, takriri, tanakali za sauti, kuchanganya ndimi, kuhamisha ndimi, taswira, jazanda, misimu, lakabu, na misemo. Kwa mujibu wa haya utafiti huu ulichanganua ufanuzi wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu mitindo hii pamoja na namna mitindo hii inavyozua changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya.

Leech na Short, (1981) wanaeleza kuwa mtindo kwa fasiri ya kijumla ni jinsi lugha inavyotumika katika muktadha fulani kwa madhumuni fulani. Mtindo unaelezwa kuwa sifa za lugha inayotumiwa. Aidha, Agu (2008), anasema kuwa mitindo ya lugha ni mfano wa ala ambazo hutumiwa na waandishi ili kubuni upya na upekee katika lugha. Matumizi ya mitindo hii huifanya lugha ya mwandishi fulani kutofautiana na waandishi wengine. Mitindo hii vile hutumika katika kuyafanya maandishi kuwa ya kuvutia na hivyo kupendeza watu wengi. Aidha utafiti huu uliweza kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi kwa kurejelea mitazamo ya watafitiwa.

Wamitila (2003) anaendelea kusema kuwa matumizi ya mitindo ya lugha yana umuhimu mkubwa sana katika kufanya ujumbe uwe wa kuvutia na wenye msisitizo na mnato mkubwa. Anaendelea kusema kuwa baadhi ya mitindo ya lugha hupunguza ukali au uzito fulani katika lugha. Lugha itumikayo kwenye mabango inastahili kuwa ya kuvutia na yenye msisitizo na mnato mkubwa ndiposa iweze kuwavutia wasomaji wengi (Dodd, 2010). Kutokana na mawazo haya utafiti huu uliweza kupambanua nafasi ya mitindo ya lugha iliyotumika katika kuwasilisha ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi.

Lodge (2009) anasema kuwa mitindo hutegemea vipengele mbalimbali kama vile wakati, mahali, washiriki, mbinu za mawasiliano na mada. Utafiti huu umetathmini namna matumizi ya lugha katika mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi hutegemea vipengele kama vile wakati na mahali.

Kitsao (1975) alihakiki mtindo katika kazi za kinathari za Kiswahili akitumia nadharia ya umitindo. Kitsao amefafanua kwa undani dhana ya mtindo na elimumitindo. Kisha akachunguza jinsi mtindo unavyojitokeza katika kazi teule alizozishughulikia kama vile mashairi, tamthilia, hadithi fupi na riwaya. Matokeo ya utafiti wa Kitsao ni muhimu kwa utafiti huu wetu kwa kuwa yametupatia mwelekeo wa kuchanganua vipengele vyta mtindo katika ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi.

Mzee (1980) alijadili tofauti zilizoko kwenye matumizi ya baadhi ya rejista za matini ya Kiswahili kuhusu habari kwa kutumia nadharia ya umitindo. Katika utafiti huu Mzee alitambua kuwa kila sehemu iliyoashiria utangazaji wa habari ilifuatilika hadi kwa lugha chapwa ya Kiingereza. Kulingana naye Kiswahili sanifu kiliathirika na Kiingereza sanifu kwa vile lugha zote mbili zilitumia sentensi changamano. Hata hivyo utangazaji habari katika Kiswahili haukuzingatia sana muundo wa utangazaji katika lugha ya Kiingereza kwa vile ulizingatia msamiati wake kwa kufuata kanuni za sarifi ya Kiswahili na hata kusababisha uundaji wa vivumishi vipyta. Matumizi ya nadharia hii katika utafiti wa Mzee yaliupa utafiti huu mwelekeo kwa vile utafiti huu ulishugulikia mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha katika rejista ya mabango ya ukimwi.

Bryne (1992) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha katika matangazo ya biashara. Kulingana na utafiti wa Bryne lugha ya matangazo ya biashara ni shawishi, imesheheni chuku, kuna matumizi ya kuchanganya na kuhamisha msimbo. Aidha lugha hiyo ni legevu na kwa kiwango fulani haijazingatia lugha sanifu. Anasema kuwa katika matangazo ya biashara kuna mtazamo fulani ambao mtangazji humtarajia mlengwa wa ujumbe kuwa nao. Kulingana naye jukumu la mlengwa ni kufasiri maana inayokusudiwa na tangazo. Tangazo moja linaweza kupata fasiri idadi sawa na ya wapokezi, kila mmoja akiwa amelifasiri tangazo fulani kwa namna tofauti. Kazi hii ya Bryne (1992) imekuwa na mchango mkubwa kwa utafiti wetu kwa vile utafiti wetu umejikita katika kupambanua namna wanafunzi wa vyuo vikuu wanavyofasiri ujumbe upatikanao kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Tofauti iliyopo kati ya utafiti wa Bryne (mtajwa) na wetu ni kuwa yeye alirejelea matumizi ya lugha katika biashara na utafiti wetu umeepambanua mitazamo ya vijana kuhusu matumizi ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi.

Michira (1993) alifanya utafiti kuhusu lugha ya wachuuzi katika soko la Gikomba mjini Nairobi na lugha ya biashara ya redio. Utafiti wake ulijikita katika misingi ya nadharia ya elimu-muundo. Alishughulikia uteuzi wa matumizi ya msamiati katika mitindo hiyo miwili ya lugha. Kutokana na utafiti huo alitambua kuwa lugha hizo zote mbili zilionyesha sifa za kuchanganya ndimi kwa hali ya ju una matumizi ya sheng. Licha ya lugha hizo kuwa na makosa mengi ya kisarufi na yaliyo wazi, sintaksia ya lugha hizo ilikuwa nyepesi. Aidha, Shartiely (2013) anasema kuwa mtindo wa kuchanganya ndimi sio matumizi ya lugha yanayojitokeza kwa bahati mbaya bali ni mojawao ya mbinu za kimawasiliano zenye lengo maalumu kutegemea muktadha. Anaendelea kusema kuwa ni mbinu ya kupunguza mchomo wa kauli. Utafiti wetu umefaidika kutokana na utafiti wa Michira (1993) katika kubainisha mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Utafiti wa Michira (1993) umetofautiana na utafiti wetu kwa vile yeye alishughulikia lugha ya usemi katika biashara na sisi tumeshughulikia mtazamo wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Kwa upande mwingine kwa kurejelea mtazamo wa Shartiely (2013) utafiti huu pia umechunguza mtazamo wa wao kuhusu mtindo wa kuchanganya ndimi katika mawasiliano kwenye mabango ya ukimwi yaliyotumia lugha ya Kiswahili.

Kutokana na utafiti uliofanywa na Brierly (1995), matangazo ya biashara hutumia lugha shawishi kwa kutumia vivumishi vinavyojenga rajamu za bidhaa na vinavyozua taswira na kutia chuku sifa za bidhaa husika. Utafiti huu ulionyesha kuwa michezo ya maneno hujaribu kufanya bidhaa kutambulika wazi na kusifika zaidi katika soko lenye wingi wa bidhaa kama hiyo. Kazi hii ilichangia kwenye utafiti wetu ambao umechunguza namna matumizi ya mitindo ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi yanavyochangia katika kufanya ujumbe kutoeleweka kwa uwazi.

Toncar na Munch (2001) wamezingatia maana katika utafiti wao. Wanadai kuwa maana ni muhimu sana katika matangazo ya biashara na hivyo inafaa kupewa kipaumbele wakati wa kuwasilisha ujumbe. Kwa mujibu wao lugha yenye utata inaweza kuathiri maana inayokusudiwa na ujumbe. Kazi hii ya Toncar na Munch (2001) imechangia pakubwa katika utafiti wetu katika kuchunguza maana zinazotolewa na vijana kwa kuzingatia fasiri zao na jinsi mitindo iliyotumika inavyozua changamoto na utata na kuathiri namna wanavyoolewa ujumbe kusudiwa.

Aloo (2002) alichunguza matumizi ya lugha katika matangazo ya biashara kwenye redio na runinga. Utafiti wake ulidhihirisha jinsi lugha ya matangazo ya biashara inavyoshawishi hadhira bila kuifahamisha vya kutosha kuhusu bidhaa zinazotangazwa. Utafiti wake pia ulidhihirisha mbinu mbalimbali za ushawishi pamoja na mitindo ya lugha inayotumiwa na watangazaji katika matangazo ya biashara. Utafiti huu umekuwa wa msaada sana kwa utafiti wetu katika upambanuzi wa matumizi ya mitindo ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi na namna lugha hiyo imeweza kuwafahamisha vijana kuhusu ugonjwa wa ukimwi kwa kurejelea fasiri zao.

Muchura (2004) katika utafiti wake aliweza kuchunguza mitindo inayotumika katika matangazo kwa kutumia picha za jinsia ya kike katika magazeti nchini Kenya kwa kuchunguza uamilifu wa mitindo katika matangazo. Utafiti huu ulidhihirisha wazi kuwa sajili ya matangazo ina mitindo yake maalumu kama vile sitiari na chuku. Kwa kurejelea matokeo ya utafiti wa Muchura, utafiti huu umeweza kuchanganua mitindo inayotumika katika mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi.

Mutonya (2008) ametafiti kuhusu matumizi ya kilugha cha sheng na watangazaji kama mbinu ya kufikia hadhira kubwa zaidi katika jiji la Nairobi ambalo limeathiriwa sana na wingi lugha. Kutokana na utafiti wake watangazaji jijini Nairobi kwa vile wameathiriwa na mabadiliko ya kijamii na kiisumu ili kuakifiana na mienendo katika jamii nyingine wanaendelea kubadili usemi wa utangazaji. Mutonya (2008) alijikita kwenye matangazo yaliyoandikwa kwenye magazeti, mabango na matangazo mengine yaliyokuwa yameangikwa hadharani. Tofauti iliyoko kati ya utafiti huu na wetu ni kuwa utafiti wetu umetathmini namna kilugha cha sheng kinavyochangia katika kuzua changamoto zinazodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.

Mukhwana (2008) alifanya utafiti kuhusu matumizi ya lugha jijini kwa kurejelea miji mitatu mikubwa nchini ambayo ni Nairobi, Mombasa na Kisumu. Lengo la utafiti wake lilikuwa ni kuangazia na kuchanganua lugha inayotumiwa jijini na vile matumizi haya ya lugha

yanavyoathiri sera ya lugha nchini. Pia alichunguza mabadiliko yanayoingia katika lugha hizi kila uchao pamoja na mpangilio wa lugha pendwa jijini na namna lugha hii inavyokubalika na watumizi wake na pia katika wingi lugha. Kazi hii imekuwa ya mchango kwa kazi yetu ambayo imeshughulikia mtazamo wa vijana wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango ya ukimwi. Tofauti ni kuwa kazi ya mtafiti huyu imerejelea matumizi ya lugha kiusemi pekee ilihali yetu imerejelea matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi.

Katika utafiti mwingine uliofanywa na Guowen (2008) kuhusu utangazaji wa usajili wa askari, Guowen ameonyesha namna mtindo wa ubadilishaji wa msimbo katika lugha unatumiwa kwa nia iliyofichika. Kulingana na utafiti wake ubadilishaji na uchanganyishaji msimbo ni mitindo ya lugha ambayo hutumiwa kama hila ya kudhibiti hadhira. Kwa mujibu wa maelezo haya utafiti wetu umechunguza matumizi ya mitindo ya kuchanganya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi na namna mitindo hii inavyoathiri lugha ya Kiswahili.

Lugwiri (2011) alifanya uhakiki wa kimtindo katika *Utenzi wa Tambuka*, alishughulikia sitari, taashiria na tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira. Katika utafiti huu, Lugwiri alitumia nadharia ya umtindo na akabainisha wazi jinsi vipengele vya tamathali za usemi vinavyobainika katika utenzi-husika. Alionyesha kuwa tamathali za usemi ni mihimili mikuu ya maudhui na dhamira. Utafiti huu unahuusu mtindo katika ujumbe unaopatikana kwenye mabango ya ukimwi. Matokeo ya utafiti wa Lugwiri yalikuwa ya manufaa katika kuchanganua vipengele vya kimtindo tutalivyovishughulikia.

2.5 Changamoto zinazokumba matumizi ya lugha ya Kiswahili

Pamoja na hadhi na umaarufu wa lugha ya Kiswahili, bado lugha hii inakumbana na matatizo makubwa katika matumizi yake. Kwa mujibu wa Mwansoko (1992) uundaji wa kudhamiria wa istilahi za Kiswahili ambao umekuwa ukiendelea tangu mwaka wa 1930, umekuwa ukikabiliwa na matatizo anuwai na hivyo kufanya usiwe na mafanikio ya kuridhisha. Matatizo haya, yanajumuisha upungufu mkubwa wa istilahi katika takriban nyanja zote za taaluma. Kulingana wa utafiti wa BAKITA (2005) kwa kiasi kikubwa, mchakato wa uundaji istilahi za Kiswahili umekuwa hauwashirikishi kikamilifu wataalamu wa nyanja za maarifa husika, hususan katika ngazi ya ukusanyaji wa istilahi katika lugha chanzi na ufanuzi wa dhana za istilahi hizo. Athari kubwa inayotokana na hali hii ni uundaji istilahi kiholela usiozingatia kujenga utoshelevu wa mawasiliano katika uwanja husika wa maarifa. Matokeo ya uholela huo ni kuwepo kwa upungufu mkubwa wa istilahi katika nyanja mbalimbali za maarifa. Upungufu huo husababishwa na dhana zaidi ya moja katika lugha chanzi. Mawazo haya yaliupa utafiti huu nguvu kwa sababu utafiti huu ultathmini iwapo kuna matumizi ya istilahi zilizoundwa kiholela na hivyo kusababisha changamoto kwa vijana katika kuelewa ujumbe wa mabango haya na hivyo kusababisha ukosefu wa utoshelevu wa mawasiliano katika nyanja husika.

BAKITA (2004) inadai kuwa kutokana na utandawazi kumekuwa na hali ya kudharau lugha ya Kiswahili nchini Tanzania na nchini Kenya, ambapo lugha hii inaonekana kuwa lugha ya

watu wa tabaka la wasionacho. Taasisi hii inaendelea kudai kuwa upinzani mkubwa unatokana na lugha ambazo zimekwisha jitanua katika dunia kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kireno na Kiarabu. Isitoshe, katika utafiti wa Mutekwa (2013), ilibainika wazi kuwa kuna baadhi ya watu ambao japo wameelimika hawapendi kusoma mabango ya Kiswahili kwa sababu ya mtazamo wao hasi kuhusu lugha hii. Wao walichukulia kuwa Kiswahili ni kigumu na hakieleweki haraka. Kutokana na mawazo haya, utafiti huu uliweza kutathmini mitazamo ya vijana kuhusu hadhi ya lugha hii na namna hali hii imechangia katika kutolewa kwa ujumbe unaowasilishwa kwenye mabango ya ukimwi kwa vijana.

Uibukaji wa kilugha cha sheng mionganoni mwa vijana ni mojawapo ya changamoto zinazokumba matumizi ya lugha ya Kiswahili. Kulingana na utafiti wa Shitemi (2001) na Ogechi (2002) sheng ni msimbo wa kijamii unaotumiwa hasa na vijana wa mijini na mashambani nchini Kenya. Vijana hutumia kilugha hiki cha sheng ili kujitambulisha kama kundi la kijamii. Sheng ni tukio la kitamaduni ambalo linafungamana sana na mawazo au fikra, hisia, na matakwa ya watumiaji wake. Ni msimbo ambao hauzingatii sheria za sarufi na tahajia kwa sababu mbalimbali. Mionganoni mwa sababu alizozitaja ni kama vile: kutojua lugha vizuri na hivyo kukosa msamiati, kuficha siri, kurahisisha mawawsiliano, kutaka kuwatenga wengine, na kujinasibisha na hadhi ya kilugha cha sheng kwa kudhani kuwa kina hadhi kubwa kuliko lugha zingine. Anaongezea kwa kusema kuwa ingawa muundo wake wa kisarufi ni ule wa Kiswahili, sheng hupuuza sarufi ya Kiswahili katika matumizi yake. Sheng imelaumiwa kwamba inasababisha vijana kutozingatia kanuni za sarufi na tahajia. Kupitia mawazo haya utafiti huu umeweza kutathmini namna kilugha cha sheng husababisha changamoto katika matumizi ya lugha ya Kiswahili na hatimaye uelewaji wa ujumbe unaowasilishwa kwenye mabango hayo.

Momanyi (2009) katika utafiti wake kuhusu athari za sheng katika ufunzaji wa lugha ya Kiswahili alitambua kuwa sheng hushusha viwango vya uelewaji wa lugha sanifu ya Kiswahili. Utafiti huu wa Momanyi (2009) umekuwa wa manufaa kwa utafiti wetu kwa vile utafiti wetu umeshughulikia kutambua uwepo wa matumizi ya sheng katika matumizi ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ugonjwa wa ukimwi na namna kilugha hiki kinavyochangia katika kuzua changamoto zinazodhihirika katika kuelewa ujumbe kwenye mabango haya vijana wanapofasiri ujumbe huo.

Okoto (2015) katika utafiti wake aligundua kuwa sheng huwafanya watu waache kutumia maneno mengine ya Kiswahili wakidhani ni sheng. Maneno haya ni kama vile „demu“, katika lugha ya Kiswahili maana yake ni kitambaa kinachotumika kufungia maziwa ya mwanamke anapolima. Neno hili limepewa maana tofauti katika sheng nayo ni ‘msichana’. Mfano mwengine ni neno „kuro“ katika Kiswahili lina maana ya mnyama wa porini anayefanana na kulungu lakini katika sheng lina maanisha „kahaba.“ Hali hii inaashiria kuwa sheng hupotosha maana halisi ya maneno ya Kiswahili. Utafiti huu wa Okoto umekuwa muhimu sana katika utafiti wetu. Hii ni kwa sababu katika utafiti wetu tumechunguza uwepo wa matumizi ya msamiati visivyo na hivyo kupotosha vijana kiwango cha wao kutotumia maneno mengine ya Kiswahili kwa kudhania kuwa ni sheng.

Maweja (2002) katika utafiti wake aligundua kuwa katika tamaduni nyingi za kiafrika kuna miiko ya kiisimu ambapo maneno na misemo fulani hairuhusiwi kutajwa hadharani, na iwapo

itatajwa itakuwa ni kuwakosea wanajamii heshima. Aghalabu mambo yanayohusiana na ngono au kajamiana na usenge katika jamii nyingi za Kiafrika ni mwiko kuyataja ilihali mambo haya ndiyo yanayosababisha usambazaji wa ugonjwa wa ukimwi kwa asilimia kubwa miongoni mwa vijana. Kutokana na mawazo haya utafiti huu uliweza kutathmini namna utamaduni umechangia katika kuzua changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhihirika katika ujumbe wa mabango haya kwa vijana.

2.6 Hitimisho

Katika sehemu hii tumehakiki maandishi ya wataalamu mbalimbali kuhusu matumizi ya lugha katika matangazo mbalimbali. Mapitio ya maandishi yanadhihirisha wazi kuwa utafiti mwingi umefanywa kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika matangazo mbalimbali haswa katika sekta ya biashara. Kutokana na mapitio ya maandishi haya ni wazi kuwa bado kulikuwa na mapengo ambayo yalifaa kuzibwa. Ingawa watafiti wengi wamefanya uchunguzi kuhusu matumizi ya lugha katika matangazo mbalimbali; uchunguzi wa mitazamo ya vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye matangazo ya mabango kuhusu ukimwi bado ulihitajika. Uchunguzi huu umetusaidia kubainisha mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Kuzibwa kwa mapengo haya kulisaidia kuonyesha namna vijana hufasiri ujumbe mmoja kwa njia mbalimbali kwa kukosa kutambua mitindo ya lugha iliyotumika. Uzibaji wa mapengo haya vile vile ulisaidia kuonyesha jinsi mitindo ya lugha inavyozua changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe kwenye mabango haya na vijana.

SURA YA TATU

NJIA NA MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu njia na mbinu za utafiti. Vipengele viliyoshughulikiwa ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, kundi lengwa, sampuli na usampulishaji, mbinu za ukusanyaji data, ufaafu wa vifaa na masuala ya maadili.

3.2 Muundo wa utafiti

Utafiti huu ulizingatia muundo mseto. Cresswell (2003), anaeleza kuwa aina hii ya muundo huwa katika viwango viwili, ambapo kiwango cha kwanza huhusisha muundo wa kitakwimu na kiwango cha pili huhusisha muundo wa kithamano. Katika utafiti huu muundo mseto wa takwimu elezi na kithamano ulijumuisha maelezo ya fasiri mbalimbali za wasomaji kuhusu matumizi ya lugha katika mabango ya matangazo ya ukimwi. Kulingana na Bryman (2004), muundo mseto humwezesha mtafiti kupata data kwa utondoti na kwa undani, data ambayo inamwezesha kutimiza malengo ya utafiti na kujibu maswali ya utafiti vilivyo.

Teddlie (2007), wanatetea hoja kuwa utafiti wa kithamano humsaidia mtafiti kuelewa namna matukio mbalimbali yanavyoathiriwa na hali halisi ya maisha. Kwa upande wao, Johnson na Onwuebuzie (2002) wanatoa hoja kuwa utafiti wa kithamano ni bora kwa kuwa mtafiti huweza kutumia tukio fulani kudhibitisha waziwazi tukio lingine muhimu kwa wasomaji kupitia maelezo. Muundo wa takwimu elezi hutumiwa kueleza tukio ambalo halijulikani.

Aidha muundo wa takwimu elezi husaidia katika upatikanaji wa ufahamu mpya ulio tofauti na hali inayojulikana (Bryman, 2004). Muundo huu pia uliwezesha utafiti huu kubaini kiwango cha utokeaji ambacho kiliweza kutupatia idadi kwa asilimia. Matumizi ya vipimo vya asilimia hutumika kudhihirisha utukiaji. Tafiti zinazojishughulisha na uchanganuzi wa matini hutumia uchanganuzi wa takwimu elezi kutimiza uchanganuzi wa kithamano huku uchanganuzi wa takwimu elezi ukitumiwa kusisitiza vipimo pamoja na vipengele vinavyokuwa vinatafitiwa (Fairclough, 2004). Maadamu muundo mseto wa takwimu elezi na kithamano ni muhimu sana. Utafiti wa kithamano hukusanya data ambayo haiko katika hali ya kitakwimu. Data ya aina hii ya kithamano huwa ni ya maelezo na kwa hivyo huwa changamoto katika uchanganuzi wake ikilinganishwa na ile ya takwimu elezi. Muundo mseto ulitumika ili kumwezesha mtafiti kupata taswira kamili ya data ya takwimu elezi kisha kutumia data ya kithamano kutoa ufanuzi zaidi kuhusu utafiti husika.

3.3 Eneo la utafiti

Kitaaluma utafiti huu ulijikita katika kuchunguza mitazamo ya wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango ya ukimwi kwa kupambanua namna wanavyofasiri ujumbe unaopatikana kwenye mabango haya, kuchanganua mitindo ya lugha iliyotumika pamoja na kutathmini changamoto zinazodhihirika katika kuelewa ujumbe huo na wanafunzi wa vyuo vikuu. Utafiti huu ulifanyika katika chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia na chuo kikuu cha Maseno. Mtafiti alizuru vyuo hivi viwili

na kupata mitazamo kutoka kwa vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili pamoja na wale ambao ni wakufunzi rika kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ugonjwa wa ukimwi. Vyuo hivi viliteuliwa kama kiwakilishi cha vyuo vikuu vya umma nchini Kenya. Vyuo vikuu vya umma husajili wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali nchini Kenya (JAB 2016). Kulingana na Gakahu (2015) ugonjwa wa ukimwi ungali changamoto kubwa katika vyuo vikuu nchini Kenya licha ya mabango kutumika kuwahamasisha vijana kuhusu ugonjwa wa ukimwi katika vyuo hivi.

3.4 Kundilengwa

Alreck na Settle (1995) wanapendekeza kuwa ni muhimu kwa mtafiti kuhakikisha kuwa kundi lengwa linasheheni watu au elementi ambazo tayari zina ujumbe ambao utamfaa mtafiti. Utafiti huu ulilenga mabango ya matangazo ya ukimwi yaliyokuwa yameandikwa katika lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi na ya taifa, na pia ndiyo lugha ambayo hutumiwa na Wakenya wengi katika mawasiliano. Kwa upande mwengine utafiti huu ulilenga vijana walio katika vyuo vikuu. Sababu ni kuwa, licha ya mabango kutumika kuwahamasisha vijana katika vyuo vikuu kuhusu ugonjwa wa ukimwi, ugonjwa huu umeendelea kuwa changamoto kubwa katika vyuo hivi. Jambo ambalo lilizua haja ya kufanya uchunguzi kuhusu mtazamo wa vijana hawa kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Utafiti huu vile vile ulihusisha vijana walio na umri wa miaka 18 hadi 24. Kulingana na Gakahu (2015) asilimia 95% ya wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Kenya wana umri kati ya miaka 18 hadi 24. Kulingana na Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu (2016), idadi jumla ya vyuo vikuu vya umma nchini Kenya ni 22. Utafiti huu ulifanyika katika chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia na chuo kikuu cha Maseno. Utafiti huu vile vile ulilenga vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili pamoja na vijana ambao ni wakufunzi rika. Idadi jumla ya wanafunzi iliyolengwa ni 3056. Vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili walilengwa kwa sababu ya tajiriba na umilisi walio nao katika lugha ya Kiswahili. Vijana hawa wanaweza kusoma na kuelewa mabango yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili. Vijana hawa pia wanaweza kutambua upungufu unaopatikana katika matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango haya pamoja na namna upungufu huo unavyokuwa kikwazo katika mawasiliano mionganoni mwa vijana wengine, haswa wale ambao hawana umilisi katika lugha ya Kiswahili. Kwa upande mwengine vijana ambao ni wakufunzi rika walilengwa kwa sababu wao hutumia mabango ya ukimwi kama nyenzo wanapotangamana na wanafunzi wengine wakati wanapowashauri kuhusu masuala ya ukimwi mionganoni mwa masuala mengine. Hivyo basi wana fursa nzuri ya kusoma mabango haya.

3.5 Usampulishaji na Sampuli

Mtafiti alitumia usampulishaji wa kimakusudi katika kuteua mabango ya matangazo ya ukimwi yaliyokuwa yameandikwa katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na mtaalamu Cresswell (2003), katika usampulishaji wa aina hii mtafiti huteua sampuli akiwa na dhamira fulani akilini ili kuondoa mapendeleo yoyote. Hapa kinachomwongoza mtafiti katika uteuzi wa sampuli zake ni sababu fulani maalumu alizo nazoz (Kothari 2003). Aidha Krueger (2000), amepambanua kwamba lengo kuu la usampulishaji wa kimakusudi huwa ni kuwalenga

wale watafitiwa pekee ambao huenda wana habari za kutosha zinazohusu madhumuni ya utafiti. Usampulishaji wa aina hii uliufaa utafiti huu. Mtafiti aliteua mabango hadi kufikia kiwango cha sampuli dabwadabwa iliyoweza kutosheleza madhumuni ya utafiti. Mabango 15 ndiyo yaliyoteuliwa kimakusudi na kutumika katika utafiti huu.

Kwa upande mwingine mtafiti alitumia usampulishaji usioratibika katika kuteua sampuli ya vijana walioshiriki katika utafiti huu. Mbinu hii iliufaa utafiti huu kwa sababu kila elementi ilipewa nafasi sawa ya kuchaguliwa katika kushiriki kwenye utafiti (Mugenda na Mugenda, 2003).

Mtafiti alitumia asilimia kumi ya idadi wakazi kama sampuli yake. Kwa mujibu wa Mugenda na Mugenda (2003) na Alreck & Settle (1995) ni vigumu kuchunguza idadi nzima ya watu inayohitajika kwa sababu ya wakati na gharama. Hivyo basi wanapendekeza asilimia kumi hadi thelathini ya idadi lengwa. Bryman (2004), anadai kuwa sampuli zinazotumiwa katika utafiti wa kiisimu ni wakilishi na matokeo yake huwa sawa kutohana na sampuli ndogo iliyoteuliwa mradi tu usampulishaji ulifanywa vyema.

Nchini Kenya vyuo vikuu vya umma ni 22. Hivyo basi asilimia kumi ya 22 ni 2. Mtafiti aliteua chuo kikuu cha Maseno na chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia kwa kuzingatia data inayodai kuwa ueneaji wa ugonjwa wa ukimwi katika chuo kikuu cha Maseno na chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia ni asilimia 10% na asilimia 9% mtawalia. (Local World Health Organization Reference Centre on HIV/AIDS, 2018). Data hii ilikuwa ithibati tosha kuwa wanafunzi katika vyuo hivi wameathiriwa na ugonjwa wa ukimwi na hivyo kusababisha utafiti huu kufanyika katika vyuo hivi.

Mtafiti alitumia usampulishaji wa kimakusudi kuteua vyuo viwili vya umma ambavyo ni chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia na chuo kikuu cha Maseno kama kiwakilishi cha vyuo vikuu vya umma nchini Kenya. Kulingana na wahadhiri wa idara ya Kiswahili katika chuo kikuu cha Maseno mwaka wa 2019 idadi jumla ya wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili ni 1,226 ambapo: katika mwaka wa kwanza ni 200, mwaka wa pili ni 330, mwaka wa tatu ni 350 na mwaka wa nne ni 386. Kwa upande mwingine, kwa mujibu wa mkuu wa idara ya Kiswahili katika chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na teknolojia mwaka wa 2019 jumla ya wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili ni 1,340 ambapo: mwaka wa kwanza ni 250, mwaka wa pili ni 300, mwaka wa tatu ni 350 na mwaka wa nne ni 440.

Kulingana na mkuu wa idara ya maslahi ya wanafunzi katika Chuo kikuu cha Maseno (2019) idadi jumla ya wanafunzi ambaao ni wakufunzi rika ni 225 ambapo: katika mwaka wa kwanza ni 65, mwaka wa pili ni 60, mwaka wa tatu ni 50 na mwaka wa nne ni 50. Kwa upande mwingine kulingana na mkuu wa idara ya maslahi ya wanafunzi katika Chuo kikuu cha Masinde Muliro (2019) idadi jumla ya wanafunzi ambaao ni wakufunzi rika ni 265 ambapo: katika mwaka wa kwanza ni 60, katika mwaka wa pili ni 70, katika mwaka wa tatu ni 75 na katika mwaka wa nne ni 65 mtawalia. Mtafiti alitumia asilimia kumi ya idadi jumla ili kupata sampuli ya utafiti wake. Uteuzi sampuli sahili usioratibiwa ultumika kuteua vijana walioshiriki katika utafiti huu. Tazama majedwali yafuatayo:

Jedwali la 1: Asilimia ya idadi ya jumla ya sampuli ya vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili (Chuo kikuu cha Maseno)

Watafitiwa		Idadi jumla (N)	Sampuli (n)	Asilimia %
Wanafunzi	wa	200	20	10
mwaka wa kwanza				
Wanafunzi	wa	330	33	10
mwaka wa pili				
Wanafunzi wa		350	35	10
mwaka wa tatu				
Wanafunzi	wa	386	38	10
mwaka wa nne				
Jumla		1,226	126	10

Jedwali la 2: Asilimia ya idadi ya jumla ya sampuli ya wanafunzi ambao ni wakufunzi rika (Chuo kikuu cha Maseno).

Watafitiwa		Idadi jumla (N)	Sampuli (n)	Asilimia (%)
Wanafunzi	wa	65	6	10
mwaka wa kwanza				
Wanafunzi	wa	60	6	10
mwaka wa pili				
Wanafunzi	wa	50	5	10
mwaka wa tatu.				
Wanafunzi	wa	50	5	10
mwaka wa nne.				
Jumla		225	23	10

Jedwali la 3: Asilimia ya idadi ya jumla ya sampuli ya vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili (Chuo kikuu Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia)

Watafitiwa		Idadi jumla (N)	Sampuli (n)	Asilimia (%)
Wanafunzi	wa	250	25	10
mwaka wa kwanza				
Wanafunzi	wa	300	30	10
mwaka wa pili				
Wanafunzi	wa	350	35	
mwaka wa tatu				
Wanafunzi	wa	440	44	10
mwaka wa nne				
Jumla		1,340	134	10

Jedwali la 3: Asilimia ya idadi ya jumla ya sampuli ya vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili (Chuo kikuu Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia)

Watafitiwa		Idadi jumla (N)	Sampuli (n)	Asilimia (%)
Wanafunzi	wa	250	25	10
mwaka wa kwanza				
Wanafunzi	wa	300	30	10
mwaka wa pili				
Wanafunzi	wa	350	35	
mwaka wa tatu				
Wanafunzi	wa	440	44	10
mwaka wa nne				
Jumla		1,340	134	10

Jedwali la 4: Asilimia ya idadi jumla ya sampuli ya vijana ambaao ni wakufunzi rika (Chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia)

Watafitiwa		Idadi jumla (N)	Sampuli (n)	Asilimia (%)
Wanafunzi	wa	60	6	10
mwaka wa kwanza				
Wanafunzi	wa	70	7	10
mwaka wa pili				
Wanafunzi	wa	75	7	10
mwaka wa tatu				
Wanafunzi	wa	65	6	10
mwaka wa nne				
Jumla		265	26	10

Wanafunzi ambaao wanasomea kozi ya Kiswahili na pia ni wakufunzi rika hawakuruhusiwa katika usampulishaji wa wakufunzi rika wao walishirikishwa tu katika usampulishaji wa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Jumla ya wanafunzi 204 walishiriki katika utafiti huu ambapo wanafunzi 106 walitoka chuo kikuu cha Maseno na wanafunzi 98 wakatoka chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia. Kati ya hawa wanafunzi 204 tulikuwemo na wakufunzi rika 57 ambapo 27 walitoka chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolijia na 30 wakatoka chuo kikuu cha Maseno. Mtafiti aliweza kuwateua watafitiwa kupitia kwa usaidizi wa viongozi wakilishi wa wanafunzi kwa kurejelea usampulishaji usioratibika. Aidha, wanafunzi 309 walitarajiwu kushiriki katika utafiti huu lakini kwa sababu zisizoepukika baadhi yao walijiuzulu.

3.6 Mbinu za Ukusanyaji Data

Data ilikusanya kuititia mbinu ya uchunzaji na majadiliano ya makundi teule.

3.6.1 Uchunzaji

Kothari (2003) anaeleza kuwa kwa kutumia mbinu ya uchunzaji, mtafiti hutafuta data kwa kushuhudia mambo yeye mwenyewe. Mtafiti alitumia mbinu hii katika kupiga picha mabango ya matangazo ya ukimwi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili. Mabango haya yalipigwa picha kutoka hospitali kuu ya Kaanti ya Kakamega, hospitali ya Maseno, mjini

Kakamega, chuo kikuu cha Maseno na chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia. Picha za mabango haya ziliwasilishwa kwa watafitiwa wakati wa majadiliano. Aidha mbinu ya uchunzaji pia ilitumika pamoja na orodha ya uchunzaji (Tazama kiambatisho 3 ukurasa wa 130) katika kuongoza kutambua mitindo ya lugha iliyotumiwa kwenye ujumbe wa mabango ya ukimwi.

3.6.2 Majadiliano ya makundi teule

Hii ni mbinu ya ukusanyaji data ambayo huhusisha kundi ndogo la watu katika majadiliano kuhusu mada fulani (Wilkinson, 2004). Kwa mujibu wa Krueger (2000) majadiliano haya ni muhimu sana katika kujadili mitazamo, maoni, mawazo na dhana kwa utondoti kuhusu masuala mbalimbali. Krueger (2000) anaendelea kusema kuwa mbinu hii ya ukusanyaji data huwa bora na ya haraka sana katika kukusanya data kutoka kwa washiriki kadha. Denzin (1970), anadai kuwa uumbaji wa mazingira yasiyo rasmi na yenye kuruhusu uhuru wa kuongea huwezesha watafitiwa kuchangia na kutoa maoni yao na mitazamo yao pasipo na uwoga wowote. Wanaendelea kusema kuwa mwingiliano kati ya watafitiwa lazima uhimizwe ili kuendeleza majadiliano. Mtafiti alihakikisha kuwa hapakuwa na aina yoyote ya urasmi wakati wa majadiliano ya makundi teule huku akiwahimiza watafitiwa kuendeleza majadiliano.

Krueger (2000), na Morgan (1997), wanapendekeza kwamba makundi teule nne hadi kumi na mbili ni toshelevu katika kufikia upeo wa data inayokusanywa iwapo makundi haya yatakutana mara kadhaa au hata mara moja. Bater na Jack (2008), wanaeleza kuwa makundi teule huhusika katika kuongoza majadiliano wazi katika makundi madogo ya washiriki kati ya 8 na 14 na hutumia mwongozo wa maswali. Dodoso ya maswali hutumika kama msingi wa orodha ya ukaguzi wa majadiliano ili kuhakikisha ujumbe sawa kuhusu kinachotafitiwa unatumika na kupatikana kutoka kwa makundi teule yote. Kwa mujibu wa haya mtafiti aliwagawanya vijana walioshiriki katika utafiti huu katika makundi teule 20, kila chuo kikiwa na makundi 10. Katika chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia makundi 8 yalikuwa na watafitiwa kumi katika kila kikundi, kundi moja likawa na watafitiwa kumi na moja kisha kundi lingine moja likawa na watafitiwa saba. Aidha katika chuo kikuu cha Maseno makundi 7 yalikuwa na watafitiwa kumi na moja katika kila kikundi, makundi mawili yakawa na watafitiwa kumi kwa kila kundi na kundi moja likawa na watafitiwa 8. Watafitiwa hawa waligawanywa katika makundi kutegemea sifa zao ambapo wale wanaosomea kozi ya Kiswahili waliunda makundi yao na kwa upande mwingine wakufunzi rika wakaunda makundi yao.

Aidha, kulingana na Creswell (2003) watu huibua maana ya hali mbalimbali na maana hizi hutokana na majadiliano pamoja na mwingiliano na watu wengine. Majadiliano ya makundi teule yalifanyika katika miezi ya Novemba na Disemba 2019. Majadiliano haya yalichukua dakika 80 hadi 105. Aidha majadiliano hayo yalifanyikia uwanjani palipo na kivuli katika vyuo husika. Ili kuhakikisha kuwa sehemu zote za utafiti zilishughulikiwa, mtafiti aliongoza utafiti akitumia dodoso ya maswali wazi aliyokuwa ameandaa hapo awali kabla ya utafiti. Maswali haya yaliundwa kutokana na madhumuni ya utafiti ili yaweze kushughulikia na

kujaza mapengo katika utafiti kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Aidha, aliwahimiza watafitiwa kushiriki vivilyo katika majadiliano haya. Majadiliano haya ndiyo yaliyounda

msingi ambamo data ilipatikana. Aidha data ya madhumuni yote matatu ilipatikana kupitia majadiliano ya makundi haya teule. Sababu ya kutumia makundi teule ni kuwa majadiliano huchochewa kuhusu mada inayoshughulikiwa na watafitiwa huweza kusema na kuelezea maoni yao na mitazamo yao. Watafitiwa walielezwa kuhusu kukubali kushiriki kwao katika utafiti mwanzoni mwa kila majadiliano na kisha kupewa fomu za kukubali kushiriki ili wasome na kisha kutia sahihi. (Tazama kiambatisho 1 ukurasa wa 126). Makundi yote yalikabidhiwa mabango sawa. Baada ya kukabidhiwa mabango mtarufi alianzisha majadiliano kwa kuongozwa na dodoso ambapo watafitiwa waliweza kutoa maoni na mitazamo yao kuhusu ujumbe unaopatikana kwenye mabango hayo. Kila kundi lilikutana mara moja. Utafiti huu ulilenga kutambua mitazamo ya wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Mwingiliano wa kawaida kati ya mtarufi na watafitiwa uliweza kuchangia katika kuwawezesha watafitiwa kushiriki wazi maoni na mitazamo yao na mtarufi. Majadiliano ya makundi teule yote yaliweza kurekodiwa kwa kutumia kinasa sauti kwa ruhusa ya watafitiwa. Utambulisho wa watafitiwa haujawekwa wazi katika utafiti huu. Ujumbe uliopatikana umesimbwa kwa kutumia nambari, kwa mfano MW23 ambapo „MW“ inaashiria mtarufiwa mwanafunzi wa Kiswahili na nambari „23“ inaashiria mshirika wa 23 katika utafiti. Aidha “MK28” inaashiria mtarufiwa mkufunzi, mshirika wa 28 katika utafiti.

3.7 Vifaa vya ukusanyaji data

Vifaa vivilyotumika katika kukusanya data ni pamoja kamera, dodoso ya maswali wazi, orodha ya uchunzaji, na kinasa sauti. Kamera ilitumiwa kunasa picha za mabango yaliyotumika katika utafiti huu. Dodoso ya maswali wazi ilitumiwa kumwongoza mtarufi katika kuendeleza majadiliano katika makundi teule. Dodoso hii ilimwezesha mtarufi kuhakikisha kuwa sehemu zote za utafiti zilishughulikiwa. Maswali haya yaliundwa kutokana na madhumuni ya utafiti ili yaweze kushughulikia na kujaza mapengo katika utafiti kwa mujibu wa madhumuni ya utafiti. Orodha ya uchunzaji ilitumiwa katika kuongoza utafiti kutambua mitindo ya lugha iliyotumiwa kwenye ujumbe wa mabango ya ukimwi. Aidha kinasa sauti kilitumika katika kunasa majadiliano ya makundi teule yote.

3.8 Ufaafu wa vifaa

Vifaa ambavyo vilitumika katika ukusanyaji data ni pamoja na kamera, orodha ya uchunzaji, dodoso ya maswali wazi yaliyoongoza majadiliano ya makundi teule kinasa sauti. Ili kuhakikisha kuwa vifaa hivi vingeafiki malengo ya utafiti, mtarufi alihakikisha kuwa vifaa hivi vilitathminiwa na kufanyiwa marekebisho na baadhi ya wahadhiri katika idara wakiwemo wasimamizi wa kazi hii. Aidha uthabiti wa vifaa hivi uliamuliwa baada ya kufanyiwa majoribio katika chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia. Majoribio haya yalimwezesha mtarufi kuwa na uhakika na vifaa vya kukusanya data ambayo ingetumiwa kufikia madhumuni ya utafiti.

Kamera ilitumiwa na mtafiti katika kupiga picha mabango ya matangazo ya ukimwi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili kwa minajili ya kutumika katika majadiliano ya makundi teule. Orodha ya uchunzaji ilitumiwa na mtafiti katika kudhibitisha matumizi ya mitindo ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango hayo baada ya watafitiwa kutambua mitindo hiyo. Mwongozo wa maswali ulimwongoza mtafiti katika kuongoza majadiliano ya makundi teule kwa kuwauliza watafitiwa maswali ili kupata maoni, mawazo na mitazamo yao kuhusu masuala husika pamoja na kuhakikisha kuwa sehemu zote zimeshughulikiwa. Kinasa sauti kilitumika katika kunasa majadiliano ya makundi teule.

3.9 Utegemezi na Ukubalifu wa Data

Utegemezi wa data unarejelea hali ambayo data inaweza kuaminika, kufungamana na kuthibitika (Baxter & Jack, 2008). Aidha, ukubalifu wa data ni uhalali wa data (Golafshani, 2003). Ili kupata data ya kutegemewa na kukubalika, mbinu ya uthibitishwaji ilitumika. Katika tafiti za kithamano, uthibitishwaji ni mbinu ambayo aghalabu hutumiwa kuhakikisha ukamilifu na uyakinishi wa data. (Shih, 1998 katika Hussein, 2009). Uthibitishwaji huchangia katika kufanya majoribio ya data ambazo zimekusanya ili kuhakikisha kuwa data hizo ni kubalifu na halali na zinaweza kutegemewa katika utafiti husika na hata tafiti nyingine (Patton, 2001 katika Golafshani, 2003). Ili kuhakikisha utegemezi na uhalali wa data ya utafiti, mtafiti alirejelea uthibitishwaji mtafiti ambapo alishirikisha wasimamizi wa kazi hii katika uchanganuzi wa data. Aidha, mtafiti alihakikisha anaelewa suala tafitiwa. Mtafiti mwenyewe ndiye alirekodi data kutoka kwa watafitiwa na kuchunguza kwa makini data hiyo.

3.9 Uchanganuzi na Uwasilishaji wa Data

Majadiliano ya makundi teule yaliyorekodiwa na kinasa sauti yalinakiliwa daftarini na mtafiti. Majadiliano haya yalinakiliwa kwa maneno jinsi yalivyosemwa bila kuongeza wala kuondoa ujumbe wowote. Utafiti huu ulirejelea uchanganuzi wa kiwingi idadi na uchanganuzi mkabala wa kithamano wa kimaelezo katika kuchanganua data iliyokuwa imenakiliwa chini.

~~Kihanga kazi yatiakididiu klezi asilimizesh Mtafiti zikubaini kiuwangga hasilinika ajiumbakh 80 kudhihirisha utukiaji. Tafiti zinazojishughulisha na uchanganuzi wa matini hutumia uchanganuzi wa takwimu elezi kuyakinisha uchanganuzi wa kithamano huku takwimu elezi ikitumiwa kusisitiza vipimo pamoja na vipengele vinavyokuwa vinatafitiwa.~~

Data iliyokusanya ilikuwa data ya kithamano. Kothari (2003), anaeleza kwamba baada ya kuisanya data inachujwa na kuchunguzwa, kisha inafasiriwa kulingana na lengo kuu la utafiti. Data katika utafiti huu ilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kithamano. Kothari (2003), anafafanua mkabala huu kama mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa kutumia maelezo. Mkabala wa kimaelezo ulitumika katika utafiti huu kwa vile data zilitokana na majibu ya kimaelezo yaliyotokana mitazamo ya watafitiwa. Hivyo basi data hizi zilihitaji kutolewa maelezo. Mkabala wa kimaelezo umetambulika kama mbinu ya kuchanganua data punde tu inapobadilishwa kwenye matini. Mkabala wa kimaelezo ulitumika katika kuchanganua data iliyokusanya. Goode na Hatt (1981), wanadai kuwa mbinu hii ya uchanganuzi huchukulia kuwa maoni ya watafitiwa huwa ya kweli na hivyo yanastahili kuchukuliwa kwa makini. Hali hii huchangia kuelewa kwetu maoni ya watu

wengine tunapoingiliana nao na kusikiliza yale wanayoutuambia. Kwa mujibu wa haya mtafiti alijitahidi kuheshimu maoni ya watafitiwa, na hivyo basi mbinu hii ilifaa katika utafiti huu. Hatua ya kwanza iliyochukuliwa na mtafiti ilikuwa ni kusoma na kuitia maoni na mitazamo ya watafitiwa iliyo kuwa sasa imenakiliwa chini. Baada ya hapo data hii ghafi ilipangwa katika kategoria tatu kurejelea madhumuni ya utafiti. Data hii iliweza kusimbwa. Baada ya hapo, data iliyo chananuliwa iliweza kufafanuliwa huku mtafiti akizingatia na kuihusisha na matokeo ya mapitio ya maandishi.

Mbinu hii ya uchanganuzi iliteuliwa kwa vile utafiti huu ultazamia kuchunguza mitazamo ya vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Kulingana na Berlson (1981) kwa kutumia mkabala wa uchanganuzi kimaelezo, mawazo yanayofanana na yanayotokana na mitazamo binafsi ya watafitiwa yanaweza kutambulika na kufafanuliwa. Muundo mseto ulitumika ili kumwezesha mtafiti kupata taswira kamili ya data ya takwimu kisha kutumia data ya kitathamano kutoa ufanuzi zaidi kuhusu utafiti husika.

Uwasilishaji wa data ulifanywa kwa kuzingatia malengo mahsus ya utafiti pamoja na maswali yaliyoambatana na malengo hayo. Data ya utafiti huu iliwasilishwa kwa kutumia maandishi yaliyoambatana na maelezo ya kiufafanuzi pamoja na picha za mabango huku mifano ya dondoo za watafitiwa zikitolewa kwa lengo la kusitiza hoja husika. za watafitiwa zikitolewa kwa lengo la kusitiza hoja husika.

Mtafiti alichanganua data kwa kuongozwa na nadharia ya umitindo (Leech na Short 2007). Matokeo na mapendekezo yalitolewa kwa misingi ya data ambazo zilichanganuliwa.

3.9 Masuala ya maadili

Masuala ya maadili ni muhimu kwa sababu yanadumisha uadilifu wa mtafiti na pia uadilifu wa utafiti wenye. (Cresswell 2003). Masuala haya hulinda haki za watafitiwa kwa kuhakikisha kuwa kuna uaminifu upande wa mtafiti na mtafitiwa. Utafiti huu ulianza punde tu mtafiti alipopewa kibali na ruhusa ya kufanya utafiti na bodi ya masuala ya maadili ya chuo kikuu cha Maseno pamoja na Halmashauri ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia ubunaji. Utafiti huu ulihusisha wanafunzi wa vyuo vikuu kama washiriki, na hivyo basi ili kuhakikisha masuala ya kimaadili ya utafiti yalizingatiwa, watafitiwa walielezwa kuwa kukubali kwao kushiriki katika utafiti huu ilikuwa ni hiari yao na uamuzi wao wa kushiriki au kutoshiriki hautawaathiri kwa namna yoyote. Mtafiti pia aliwaeleza kuhusu lengo na aina ya utafiti huu kuitia fomu ya kukubali kushiriki katika utafiti ambapo walihitaji kutia sahihi ili kuonyesha wamekubali kushiriki katika utafiti huu (Tazama kiambatisho 1 ukurasa wa 126. Watafitiwa walielezwa na kuhakikishiwa kuwa maoni na mitazamo watakayoitoa kwenye majadiliano ya makundi teule yatakuwa ya siri.

Watafitiwa hawakuuhakikishiwa hali ya kuficha utambulishaji wao kwa vile majadiliano ya makundi teule yalifanyika ana kwa ana, hata hivyo ujumbe wa kujitambulisha haukuulizwa. Mtafiti aliwaomba ruhusa ya kutumia dondoo zao halisi kwenye ripoti fainali ya utafiti huu. Ruhusa ya kunasa majadiliano yao pia iliombwa na watafitiwa wakaelezwa kuwa pia wana uhuru wa kujiiondoa kwenye majadiliano hayo wakati wowote.

Watafitiwa walielezwa kuwa kanda zilizotumika kunasa sauti ya majadiliano hayo ya makundi teule zitaharibiwa punde tu utafiti utakapokamilika. Nakala zilizonakiliwa zote zilipitiwa na ujumbe wowote ambao ungeweza kumtambulisha mtafitiwa kama vile majina, wote uliondolewa. Mtafiti aliusimba ujumbe alioupokea kwa kutumia nambari. Kwa mfano MW23 ambapo MW inaonyesha mtafitiwa mwanafunzi na nambari 23 inaonyesha yeye ni mshirika wa 23 katika utafiti na MK inaonyesha mtafitiwa mkufunzi. Mtafiti alipeana anwani na nambari yake ya simu na kuwahimiza watafitiwa kuweza kuwasiliana naye iwapo kutazuka jambo lolote linalohusiana na utafiti.

3.10 Hitimisho

Sura hii imewasilisha njia na mbinu zilizotumika katika utafiti huu. Kila njia na mbinu imeelezwa kwa undani namna ilivyotumika ili kufanikisha utafiti huu. Uchanganuzi wa kitakwimu na kitathmini ulitumika. Kwa kutumia orodha ya uchunzaji na majadiliano ya makundi teule, data ilikusanywa. Data hii ilipangwa na kuanishwa kulingana na madhumuni ya utafiti ili kuchanganuliwa. Matokeo ya utafiti yamejadiliwa katika sura ifuatayo.

SURA YA NNE

UCHANGANUZI NA UWASILISHAJI DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo na mjadala kuhusu mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi. Matokeo ya utafiti huu yamegawanywa katika sehemu tatu kuu kulingana na madhumuni ya utafiti. Sehemu ya kwanza inapambanua fasiri mbalimbali za ujumbe unaopatikana kwenye mabango ya matangazo ya ukimwi zilizotolewa na watafitiwa. Sehemu ya pili inachanganua mitindo ya lugha iliyotumika kwenye ujumbe unaopatikana kwenye mabango hayo. Sehemu ya tatu imejikita katika kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhiihikira katika kuelewa kwa ujumbe wa mabango hayo kwa vijana. Maelezo ya sehemu hizi tatu yametolewa kwa kuzingatia nadharia ya umitindo (Leech na Short 2007).

4.2 Fasiri za vijana kuhusu ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi

Data katika utafiti huu ilipangwa kwa kuzingatia madhumuni ya utafiti ambapo madhumuni ya kwanza yalihusu upambanuzi wa fasiri zilizotolewa na watafitiwa. Kulingana na kamusi ya TUKI (2004), kufasiri ni ile hali ya kutoa maana ya jambo lilofichika, ni kufafanua maana ya ujumbe. Ufasiri ni dhana muhimu sana katika mawasilano. Ili mawasiliano yatimilike vyema ni lazima ujumbe ufasiriwe vyema na anayepokea ujumbe huo. Hili litaweza tu kutokea pale ambapo maana ya ujumbe unaolengwa na mwasilishi unamfikia mpokezi pasi na utata na upotoshi. Kuwasilisha dhana fulani kwa jamii kwa njia mwafaka kunategemea lugha na ishara (Wamitila 2000). Katika kiwango hiki mabango yaliyorejelewa ni kama yafuatayo: *B1 Usilambe asali katika kila nyumba, B2 Usiogelee mto Nyando naked vaa CD, B3 Sisi tumeingia kwa network juu tunajua hali yetu ya HIV, B4 Jitambue leo, B5 Bila kondmu hakuna mapenzi, B6 Uwanja mdogo, kamdudu kako. Tuima CD, B7 Ati bila CD, afadhali ikae!, B8 Chunga usipate red card, vaa seatbelt, B9 Valia boots usidungwe na mwiba, B10 Ukimwi si ajali bali ni msiba wakujitakia B13 Jijue ubambishe life, B15 Mwanamume kamili hujua status yake ya HIV, chukua test leo.* Watafitiwa walifasiri ujumbe upatikanao kwenye mabango ya matangazo ya ukimwi kwa njia mbalimbali zinazohitilafiana jinsi inavyodhiihikira katika data ifuatayo:

B1: Usilambe asali katika kila nyumba.



Katika utafiti huu wanafunzi 44 (22%) walifasiri ujumbe huu kwa njia mbalimbali. Idadi hii ilijumlisha wanafunzi ambao ni wakufunzi rika. Wakufunzi rika walioshirikishwa katika utafiti huu hawakuwa wanaosomea kozi ya Kiswahili. Aidha kulingana na Fish (1970), msomaji hufasiri matini kwa njia tofauti kutegemea hisia na tajriba yake ya usomi na maisha. Fish aligundua haya baada ya kuchunguza jinsi wanafunzi walivyofasiri wahusika katika ngano walizozisoma. Utafiti wetu umeweza kubainisha wazi jinsi watafitiwa walivyofasiri ujumbe unaopatikana katika haya mabango ya ukimwi. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Baadhi yao waliweza kutoa fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MK101: *Kwangu ujumbe huu unatuonya kuwa tusile chakula kwa nyumba za watu ovoyovo.*

Mtafitiwa MK108: *Mimi naonelea kuwa ujumbe kwenye hii bango unatuambia kuwa ni vizuri kula chakula kwenye nyumba za watu unaowajua.*

Mtafitiwa MK114: *Kuna hatari katika kula chakula katika kila nyumba, huenda ukapewa sumu.*

Hawa watafitiwa ambao walikuwa wakufunzi rika walichukulia msamiati „asali“ kuwa chakula cha kawaida. Ufasiri wao haukutegemea muktadha husika, jambo ambalo liliwasababisha kutofasiri ujumbe jinsi ilivytarajiwa. Kulingana na Leech na Short (2007) katika kiwango cha semantiki, maana ya maneno huchunguzwa kutegemea muktadha husika. Aidha Tompkins (1980) anaeleza kuwa maarifa ya kimsingi na tajiriba aliyonayo msomaji huathiri namna ambavyo ataifasiri matini fulani.

Watafitiwa hawa (ambao ni wakufunzi rika) hawakuwa na tajiriba na umilisi katika lugha ya Kiswahili. Huenda hali hii ndiyo iliyosababisha wao kutofasiri ujumbe jinsi ilivytarajiwa. Hata hivyo vijana 160 (78%) waliweza kuufasiri ujumbe huu jinsi ilivytarajiwa. Watafitiwa 157 walikuwa na maoni sawa na ya watafitiwa hawa wafuatao:

Mtafitiwa MW41: *Ujumbe huu unatuonya kuwa tusiwe watu wa kufanya mapenzi na kila mtu.*

Mtafitiwa MW51: *Kulingana nami nahisi kuwa huu ujumbe unnatutahadharisha kuwa tuweze kudhibiti tamaa za kimwili. Tusifanye mapenzi na kila mtu.*

Mtafitiwa MW58: *Huu ujumbe una maana fiche. Kuna matumizi ya mafumbo. Mimi nasema hivi kwa sababu ya muktadha ambamo umetumiwa. Kwani asali inayozungumziwa si ya kawaida. Asali hapa inamaanisha mapenzi na kulamba ni kile kitendo cha kufanya mapenzi. Kwa hivyo mimi nakubaliana na wenzangu wanaosema kuwa ujumbe huu unamaanisha kuwa tusifanye mapenzi na kila mtu.*

Idadi hii ya watafitiwa 160 (78%) ilijumlisha vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili na walio na tajiriba na umilisi katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na Leech na Short (2007) katika kiwango cha semantiki maana ya maneno huchunguzwa kutegemea muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Watafitiwa hawa kwa kurejelea muktadha husika waliweza kutambua kuwa msamiati ‘asali’ ulimaanisha mapenzi, ‘kulamba’ ilimaanisha

kitendo cha kufanya mapenzi na ‘nyumba’ ikamaanisha mtu. Waliweza kutambua kuwa ujumbe huu ulionya vijana kuwa wasiwe watu wa kufanya mapenzi na kila mtu. Asali ni maji matamu sana na mazito yanayotengenezwa na nyuki ambaye ni mdudu anayeweza kuumaa na hata kusababisha mauti anapomshambulia binadamu. Kulamba ni kitendo cha kufuta kwa kutumia ulimi polepole. Panapo asali hapakosi nyuki. Ingawa nyuki hutengeneza asali ambayo ni tamu sana, huwa hatari pia kwa maisha ya binadamu wakati anapomuumaa kwa kumrushia mishale. Mishale hiyo huwa na sumu ambayo husababisha mauti kwa binadamu. Vile vile mapenzi huwa ni tamu, iwapo anayehusika ana virusi vya ukimwi basi ni mfano wa nyuki anayeweza kusababisha mauti, kwani atamwambukiza mwenzake ukimwi kupitia virusi hivi na hivyo kusababisha mauti jinsi mishale ya nyuki husababisha mauti kupitia kwa sumu aliyonayo.

B2: „Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.



Vijana 49 (22%) hawakufafanua ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Baadhi yao walitoa fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MK113: *Mbona tu mto Nyando pekee? Kuogelea huku nafeel si kwa kawaida kwa sababu watu wakiogelea ni lazima wavue nguo kwanza. Lazima ujumbe huu una maana fiche. Hili ni fumbo.*

Mtafitiwa MK115: *Hata mimi nahisi kuwa haya ni matumizi ya mafumbo. Ujumbe huu ni fiche, ni lazima mtu afikirie sana au aulize wenzake ili kupata maana.*

Mtafitiwa MK116: *Mimi nafeel kuwa huenda ujumbe huu unaashiria hatari iliyoko ndani ya mto Nyando na hivyo ujumbe huu unatuonya tutahadhari. Hata mimi nahisi kuwa ujumbe huu ni fumbo. Kwani kuoga huku si kwa kawaida. Ujumbe unaopashwa ni mzito.*

Mtafitiwa MK119: *Naam, nakubaliana na mwenzangu, ndani ya mto huwa tuna wanyama hatari amba wanaweza kutuvamia na hivyo kuhatarisha maisha yetu. Kwa hivyo ni muhimu kuogelea ukiwa na nguo ili kuwa tayari kutoka hatari ikitokea.*

Watafitiwa hawa walishangaa kwa sababu kulingana na wao walielewa fika kuwa mtu hastahili kuogelea akiwa amevaa nguo. Kwani kawaida mtu huogelea akiwa uchi. Walichukulia kuwa ujumbe huu uliwatahadharisha kuwa huenda watu wangepatwa na hatari

fulani wakiwa majini wakiogelea na hivyo ingekuwa rahisi wao kutoka majini kwa haraka. Vile vile walihisi kuwa ujumbe huu pia uliwatahadharisha kuwa huenda watu wangeona uchi wao kwa vile mto huwa mahali wazi panapoonekana kwa yelete apitaye. Watafitiwa hawa 50 walikuwa ni wakufunzi rika. Watafitiwa hawa walifasiri ujumbe huo jinsi walivyofahamu pasipo na kuuhusisha na muktadha husika. Leech na Short (2007) kwa upande wao, wanatetea hoja kwa kiwango cha semantiki kuwa ili ujumbe ufasiriwe vyema ni sharti maana ichunguzwe kwa kurejelea muktadha husika. Aidha, Fish (1970) anasema kuwa kila msomaji huifasiri matini kwa njia tofauti kutegemea tajiriba yake ya usomi na maisha. Wakufunzi rika ambao walihuishwa katika utafiti huu hawakuwa wanosomea kozi ya Kiswahili. Hii inamaanisha kuwa hawakuwa na tajiriba ya usomi katika lugha ya Kiswahili na hivyo kukosa kufasiri ujumbe jinsi ilivytarajiwa. Watafitiwa 5 (10%) kati ya hawa asilimia 22% walielewa fika kuwa kuogelea huku hakukuwa kwa kawaida, walisema kuwa lazima ujumbe huu ulikuwa na maana nzito ingawa hawakufafanua na kufasiri maana tarajiwa ya ujumbe huu.

Kwa upande mwingine vijana 155 (76%) waliweza kuufasiri ujumbe huu jinsi ilivytarajiwa. Watafitiwa hawa walikuwa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili na hivyo walikuwa na tajiriba na umilisi katika lugha ya Kiswahili. Watafitiwa 153 walikuwa na maoni sawa na ya mtalifiwa MW21 na mtalifiwa MW22 jinsi inavyodhahirika katika data ifuatayo:

Mtalifiwa MW21: *Kulingana nami ujumbe huu ni ujumbe ambao una maana fiche. Tukitazama bango hili pale chini kuna ujumbe ambao unatueleza kuwa tuvae CD. Nahisi kuwa kuogelea kunakozungumziwa si kwa kawaida. Kuogelea huku kuna maanisha hali ya kufanya mapenzi, na hivyo tunaonywa kuwa tusifanye mapenzi bila kinga, yaani tusioge tukiwa uchi. Haya ni matumizi ya istiari.*

Mtalifiwa MW22: *Yale mwenzangu amesema ni kweli kabisa, CD pale inamaanisha condom, yaani mpira wa kinga.*

Watafitiwa hawa waliweza kufasiri ujumbe kutegemea muktadha husika. Leech na Short (2007) kwa kurejelea kiwango cha semantiki, wanavema kuwa maana huchunguzwa kutegemea muktadha husika. Wao walitambua kuwa msamati ‘ogelea’ ulimaanisha kufanya mapenzi, ‘mto Nyando’ ulimaanisha binadamu na ‘naked’ ikamaanisha uchi. Kulingana na wao „kuogelea mto Nyando naked” ilimaanisha kufanya mapenzi bila kinga, na ujumbe unawaelekeza watu kutumia kondomu kama kinga dhidi ya ugonjwa wa ukimwi.

Kimsingi, kuogelea ni hali ya kuenda juu ya maji bila kuzama kwa kutupa mikono na miguu. Mto ni korongo lenye maji yanayotiririka wakati wote. Ni kweli kwa kawaida mto huogelea akiwa amevua nguo, lakini kwenye ujumbe huu tunashauriwa tusiogelee tukiwa uchi haswa kwenye mto Nyando. Kila mto anao uhuru wa kuogelea katika mto wowote. Mto Nyando hupatikana katika wilaya ya Nyando, kaunti ya Kisumu. Kulingana na Shirika la Afya Duniani (WHO 2011) asilimia 80.3% ya wakaazi wa Nyando wanaishi na virusi vya ukimwi. Huenda hii ndiyo sababu mto Nyando umetumika katika ujumbe huu na wala si mto mwingine. Ujumbe huu huenda unatahadharisha watu hasa wale ambao wanaishi sehemu

zilizoathiriwa na usambazaji wa ugonjwa wa ukimwi kwa kiwango cha juu. Watu hawa wawe waangalifu wanapojuhishwa kimpenzi kwani wachukue tahadhari. Aidha, wakati mwingine mto Nyando huvuja kingo zake wakati wa mafuriko na kusababisha maafa makubwa.

B3: Sisi tumeingia kwa network juu tunajua hali yetu ya HIV.



Kuhusiana na bango hili watafitiwa 203 (99%) walikosa kufasiri ujumbe kwenye bango hili jinsi ilivyokusudiwa. Baadhi ya watafitiwa walitoa maoni yafuatayo:

Mtafitiwa MK92: *Usipojua status yako hautaruhusiwa kutumia network? Network iko kila mahali. Kila mtu anaweza akatumia wakati anapoihitaji.*

Mtafitiwa MK94: *HIV na network ina uhusiano upi? Iwapo una ukimwi utanufaika namna gani? Ujumbe huu hauelezi waziwazi jinsi ya kuepukana na ukimwi.*

Mtafitiwa MK97: *Utajua je ni nani yumo ndani ya network? Kwani utatangazia kila mtu status yako?*

Mtafitiwa MW5: *Mimi niliposoma mara ya kwanza ujumbe kwenye bango hili sikuelewa unazungumzia nini, ujumbe huu haukuwa wazi hadi niliposikia wenzangu wakiujadili, hata nikajihisi kuwa mpumbavu kwa ajili ya kutoweza kufasiri ujumbe huu jinsi ilivyokusudiwa.*

Mtafitiwa MW7: *Nadhani itamchukua mtu mwerevu kuelewa ujumbe huu. Mtu aliye na kiwango cha wastani na cha chini kiakili hataelewa. Ni ngumu kuelewa ujumbe huu na hivyo sielewi kwa nini wanajisumbua kutumia mitindo hii ya lugha badala ya kutumia lugha iliyowazi yaani ya moja kwa moja.*

Mtafitiwa MW10: *Jumbe hizi haziwasiliani na hadhira na hata hivyo huwa si wazi.*

Ujumbe huu uliwakanganya watafitiwa, hawakuelewa unamaanisha nini kiasi kwamba hawakuweza kutambua uhusiano uliopo kati ya hali yao ya ukimwi na 'network' (Mtandao). Kulingana na wao ujumbe huu haukuwa unasema ukweli na wala haukuwa wazi. Kulingana nao 'network' yaani mtandao huwa kila mahali, na hivyo basi kila mtu anaweza akatumia

wakati anapouhitaji. Mtafitiwa MW7 aliongezea kwa kusema kuwa mabango hayo haya jaongezea thamani yoyote kwa vile watu wanang'ang'ana kuelewa ujumbe huo. Alisema kuwa ye ye aliweza tu kuelewa ujumbe huo baada ya kushiriki kwenye majadiliano. Mtaalamu Agu (2008) anasema kuwa kiwango cha uelewaji wa ujumbe fulani hutegemea namna ujumbe huo umewasilishwa. Wamitila (2000) anashikilia kuwa ili kuwasilisha dhana fulani kwa jamii kwa njia mwafaka kunategemea sana luga na ishara. Isitoshe, kulingana na Leech na Short (2007) matumizi ya luga yanaweza kuathiri maana ya ujumbe fulani kwa njia fulani. Mtafitiwa 1 (0.49%) pekee (MW12) ndiye aliweza kuufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Mtafitiwa huyu alitoa fasiri ifuatayo;

Mtafitiwa MW12: *Mimi naona kuwa ujumbe kwenye bango hili unatueleza kuwa vijana walioingia kwenye mtandao wako sawa kabisa kwa sababu wanaelewa hali yao kuhusiana na ukimwi. Uki jua hali yako utajua namna ya kuishi. Wanatuomba hata sisi tuweze kui jua hali yetu ili tui junge nao kwenye mtandao.*

Mtafitiwa huyu MW12 alieleza kuwa ujumbe huu ulimaanisha kuwa vijana walioingia kwenye mtandao walikuwa sawa kwa vile walielewa hali yao ya ugonjwa wa ukimwi, na hivyo walikuwa wanaomba na kuwashawishi wasomaji bango pia wao vile vile waweze kui jua hali yao ya ukimwi ili waweze kujiunga nao kwenye mtandao. Kwani ukijua hali yako utaweza kujua jinsi ya kujitunza.

Kwa sasa vijana wengi wamehusishwa na masuala ya teknolojia na mtandao. Huenda aina hii ya luga ilitumika ili kunata makini yao. Kulingana na Mutula (2003), aslimia 85% ya wanafunzi walio katika vyuo vikuu nchini Kenya hutumia mtandao kuwasiliana, kusoma na hata kufanya utafiti. Aidha mtandao ni mfumo wa mawasiliano wa kieletroniki. Mtu akiwa kwenye mtandao huwa ni rahisi kupokea habari na hata kuwasiliana. Watafitiwa walihitajika kuelewa maana msingi ya msamati 'mtandao' ndiposa waweze kufasiri ujumbe kwenye bango (B3) hili jinsi ilivyotarajiwa. Kutokana na maana msingi maneno huhusishwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani kimsingi (Leech & Short 2007). Kimsingi mtandao ni mfumo wa mawasiliano. Ujumbe kwenye bango: B3... "Sisi tumeingia kwa network juu tunajua hali yetu ya HIV"... unamaanisha kuwa vijana ambao wanajua hali yao ya ukimwi wamo katika hali fulani ya mawasiliano. Kwani wanaweza kupokea habari fulani kuhusu namna wanavyoweza kutangamana na wenzao katika jamii pasipo na kuathiriana kiafya kwa njia hasi. Ili mtu aweze kujua hali yake ya ukimwi ni lazima atembelee kituo cha ushauri ndiposa apimwe na kuelezwa kuhusu hali yake ya ukimwi. Anapokuwa katika kituo cha ushauri ye ye huweza kupata habari zaidi kuhusu ugonjwa wa ukimwi pamoja na namna anavyoweza kujitunza kutegemea hali yake ya ukimwi.

B4: *Jitambue leo.*



Watafitiwa 43 (21%) hawakuweza kuufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Watafitiwa hawa walijumuisha wakufunzi rika. Fasiri zifuatazo zilitolewa na baadhi yao:

Mtafitiwa MK83: *Sielewi kujitambua kivipi?*

Mtafitiwa MK89: *Tayari mimi nadhani ninajijua. Sielewi ujumbe huu unalenga nini?*

Mtafitiwa MK110: *Jinsi ujumbe huu ulivyowasilishwa hatuelezwi unalenga masuala yapi. Hatujui kama unazungumzia ukimwi, magonjwa mengine ya zinaa au uja uzito.*

Mtafitiwa MK123: *Huu ujumbe haupeani mwelekeo wa baada ya kujitambua. Nahisi kuwa kuna ujumbe ambao umeachwa nje, haujakamilika.*

Kwa kurejelea kiwango cha semantiki maana ya maneno inapaswa kuchunguzwa kutegemea muktadha husika (Leech & Short 2007). Watafitiwa hawa hawakuhusisha ujumbe huu na muktadha husika, wao walifasiri tu ujumbe huu kulingana na ufahamu wao. Watafitiwa hawa hawakuelewa kujitambua kivipi, hawakutambua lengo la ujumbe huu. Kulingana nao ujumbe huu haukupeana mwelekeo baada ya kujitambua. Watafitiwa hawa walifasiri ujumbe huu kwa njia tofauti tofauti. Kulingana na Tompkins (1980) maarifa ya kimsingi na tajiriba aliyonayo msomaji huathiri namna ambavyo atafasiri ujumbe fulani. Anaendelea kusema kuwa ujumbe ule ule mmoja unaweza kufasiriwa kwa njia tofauti na wasomaji tofauti. Aidha wakufunzi rika ambao walihusishwa katika utafiti huu ni wale ambao hawasomei kozi ya Kiswahili hivyo hawana tajiriba na umilisi katika lugha ya Kiswahili. Huenda hii ndiyo sababu ya wao kufasiri ujumbe huu kwa njia tofauti tofauti.

Hata hivyo kuna wanafunzi 161 (78%) ambao waliweza kufafanua ujumbe huu kulingana na muktadha husika. Hawa walijumuisha wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili, kwani walikuwa na tajiriba na umilisi wa lugha ya Kiswahili. Watafitiwa wawili mionganoni mwao walitoa maoni yafuatayo kuhusiana na ujumbe huu huku wengine 159 wakiwa na maoni sawa na yao:

Mtafitiwa MW154: *Kulingana na mimi naona kuwa ujumbe huu unamaanisha mtu kujua hali yake ya ugonjwa wa ukimwi.*

Mtafitiwa MW156: *Labda tu kwa kuongeza kwa yale ambayo mwenzangu amesema ni kuwa nahisi kuwa licha ya kujua hali ya ukimwi ujumbe huu pia unaweza kuwa unalenga hali zingine kama za uja uzito na magonjwa mengine ya zinaa.*

Watafitiwa hawa walieleza kuwa ujumbe huu ulimaanisha msomaji anastahili kujua hali yake ya afya haswa kuhusiana na ugonjwa wa ukimwi. Waliongeza kwa kusema kuwa huenda pia ujumbe huu unalenga hali zingine kama vile uja uzito na magonjwa mengine ya zinaa. Watafitiwa hawa waliweza kuhusisha muktadha husika katika fasiri zao na hivyo kufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Kutokana na fasiri zao ni wazi kuwa ili umbe uweze kufasiriwa vyema ni sharti muktadha husika uhusishwe jinsi wanavyodai Leech na Short (2007).

Kujitambua ni ile hali ya kujielewa na kujijua. Hivyo basi kujitambua huku kunamaanisha kuwa mtu anastahili kujua kama ana ugonjwa wa ukimwi au hana. Baada ya kujitambua atawea kujua namna atakavyoyalinda maisha yake na hivyo kuweza kujitunza kutegemea hali yake. Sifa mojawapo ya mabango ni kutumia maneno machache ambayo ni rahisi kueleweka (Dodd 2007, Robin 2009). Bango hili limeandikwa kwa muhtasari ili kuwezesha hadhira kusoma ujumbe, kwani ni nadra sana watu kutumia zaidi ya dakika tano kusoma mabango (Robin 2009).

B5: *Bila kondomu=Hakuna mapenzi*



Watafitiwa 50 (25%) hawakutambua maana ya ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa kwa kulingana na muktadha husika. Baadhi yao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MK82: *Huu ujumbe hausemi ukweli. Hupendi mtu kwa sababu ana kondomu.*

Mtafitiwa MK107: *Kondomu si mapenzi. Mapenzi ni kama kikohozi.*

Mtafitiwa MK109: *Na hisi kuwa ujumbe huu unamaanisha kuwa lazima pawe na kondomu ndiposa pawe na mapenzi. Huu ujumbe hausemi ukweli.*

Kulingana na watafitiwa hawa ujumbe huu ulimaanisha kuwa unampenda mtu kwa sababu ana kondomu kinyume na mawazo yao. Wao walihisi kuwa hustahili kumpenda mtu kwa sababu ana kondomu, kondomu si mapenzi, kwani mapenzi ni kama kikohozi. Waliendelea kudai kuwa, kulingana na ujumbe huu ni lazima pawe na kondomu ndiposa pawe na mapenzi, na kisha kusema kuwa ujumbe huu haukuwa unasema ukweli. Ujumbe huu ulizua mitazamo tofauti mionganoni mwa watafitiwa. Wao walichukulia ujumbe huu kumaanisha kuwa kondomu ndiyo huleta mapenzi kati ya watu. Aidha watafitiwa hawa hawakuhusisha muktadha husika na wala kutafakari jinsi maneno kwenye ujumbe yalivyotumika. Kulingana na Leech na Short (2007), maana ya maneno hutegemea matumizi yake, haitegemei namna neno linavyojoitokeza kwa kulitazama kijuujuu.

Kwa upande mwingine watafitiwa 154 (75%) waliweza kuufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Wao walikuwa na maoni sawa na ya mtafitiwa MW162 ambaye alisema haya:

Mtafitiwa MW162: *Mimi nafikiri kuwa ujumbe huu unamaanisha kuwa iwapo mtu anataka kufanya mapenzi ni lazima atumie kondomu kama kinga, la sivyo asidhubutu kufanya mapenzi.*

Watafitiwa hawa walielewa fika kuwa ujumbe huu ulimaanisha kuwa iwapo mtu atataka kufanya mapenzi ni lazima atumie kondomu kama kinga, la sivyo asidhubutu kufanya mapenzi. Watafitiwa hawa waliweza kurejelea muktadha husika walipokuwa wanafasiri ujumbe huu jinsi wanavyodai Leech na Short (2007). Ujumbe huu unashauri kuwa mtu asifanye mapenzi bila kinga. Kulingana na ujumbe huu mpira wa kinga unaweza kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi. Hata hivyo watafitiwa hawa hawakuwa makini kusoma ujumbe wote ambao ulikuwa kwenye bango hili. Kwani kuna sehemu ambayo waliiacha nje. Sehemu hii ni ile imejitokeza kama usemi halisi wa wale walio kwenye picha yaani... “nina mimba na niko na virusi vya ukimwi” ... “mtoto tunamuachia nani?” Kukosa kusoma ujumbe wote vile vile kulichangia katika wao kukosa kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa.

B6:Uwanja mdogo, kamdudu kako. Tumia CD



Kuhusu bango hili, watafitiwa walikuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu ujumbe wake. Jumla ya watafitiwa 70 (35%) hawakuweza kuufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Baadhi ya watafitiwa hawa walitoa maoni kama ifuatavyo:

Mtafitiwa MK102: *Uwanja ukiwa mdogo itakuwa ni vigumu watu kuutumia. Na kwanza wanasema kamdudu kako, si basi uwanja huu ni mbaya kwa binadamu kuchezea.*

Mtafitiwa MK103: *Hata kama uwanja ni mdogo, si unaweza kutafuta uwanja mwingine mkubwa?*

Mtafitiwa MK112: *Kamdudu ni kitu kidogo sana ambacho chaweza kuangamizwa na mtu yeoyote.*

Mtafitiwa MK117: *Ujumbe huu haueleweki waziwazi kwani uwanja, kamdudu na CD vina uhusiano upi?*

Mtafitiwa MK121: *Kwa nini hawa watu wanafanya Kiswahili kuwa ngumu? Wanafanya hata nisipende kusoma mambo kwa Kiswahili. Wanafanya lugha ya Kiswahili kuwa ngumu hata huwezi kuelewa kitu haraka.*

Mtafitiwa M125: *Ni CD ipi inayozungumziwa?*

Watafitiwa hawa hawakuchunguza maana kutegemea muktadha. Kulingana na Leech na Short (2007) kwa kurejelea kiwango cha semantiki maana ya maneno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Miongoni mwa watafitiwa hawa kuna wale ambao walihisi kuwa itakuwa vigumu uwanja huo kutumika kwa vile ulikuwa mdogo na pia uwanja huo haukuwa mzuri kwa binadamu kuchezea kwa sababu ulikuwa na wadudu, walisema kuwa hata kama uwanja ni mdogo una uhuru wa kutafuta uwanja mwingine mkubwa. Vile vile kulingana na wao mdudu ni kiumbe mdogo sana ambaye anaweza kuangamizwa na mtu yeoyote, hivyo basi hawakuelewa kwa nini kiumbe mdogo hivyo kumhangisha binadamu. Walidai kuwa ujumbe huo haukuelewa kaziwazi kwa sababu kulingana nao, hakuna uhusiano wowote kati ya uwanja, kamdudu na CD.

Watafitiwa hawa walifasiri ujumbe huu jinsi walivouelewa na hata pasipo kuulinganisha na muktadha husika kinyume na matarajio ya Leech na Short (2007), ambao wanadai kuwa ili kuelewa maana kusudiwa ni vyema ujumbe kulinganishwa na muktadha husika. Isitoshe kuna wale ambao walidai kuwa matumizi haya ya lugha yalikifanya Kiswahili kuwa kigumu kiasi cha kwamba hawawezi kuelewa ujumbe unaopashwa kwa haraka. Hali iliyowafanya kuwa na mtazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili na hivyo kuwafanya kutopenda kusoma ujumbe ulioandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Mutekwa (2013), katika utafiti wake aligundua kuwa kuna baadhi ya vijana ambao walikuwa na mtazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili na hawakupendelea kusoma mabango ya Kiswahili. Anaendelea kusema kuwa vijana hawa walikosa umakini wa kuchunguza elementi za kisanaa na za kisiimu katika fasiri zao. Kwa hivyo mtazamo huu uliathiri namna walivofasiri mabango ya Kiswahili ya afya. Dodd (2007) na Robin (2009) wanasisitiza kuwa mabango mazuri ni yale ambayo huwasilisha ujumbe kwa njia ya haraka, yanashawishi na yanavutia. Kulingana na maoni ya watafitiwa

hawa mabango haya hayalingani na matarajio ya akina Dodd (2007) na Robin (2009). Watafitiwa waliotoa maoni haya ni mionganini mwa wakufunzi rika yaani wale ambao hawasomei kozi ya Kiswahili.

Kwa upande mwingine jumla ya watafitiwa 134 (65%) waliweza kuufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Watafitiwa hawa Baadhi ya watafitiwa hawa walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW23: *Lugha hii iliyotumika katika bango hili haiangazii ujumbe unaokusudiwa moja kwa moja. Lazima mtu aeewe sajili inayorejelewa ndiposa aweze kutambua maana ya ujumbe uliokusudiwa.*

Mtafitiwa MW32: *Ujumbe huu kulingana na mimi unapotosha na kukanganya wasomaji. Kwani haueleweki moja kwa moja. Mtu huenda akadhania kuwa „uwanja mdogo“ inarejelea kuwa na wapenzi wachache. Kwani haumwelekezi msomaji kuwa na mpenzi mmoja. Ni lazima mtu atafakari kwa undani ndiposa apate maana ya ndani ya ujumbe huu.*

Mtafitiwa MW36: *Mimi naona kuwa ujumbe huu una maana ambayo ni tofauti kabisa na ile inayojitokeza kijuujuu, kwani haumrejelei mchezaji wa kawaida Ujumbe huu unatuonya kuwa tusiwe na uhusiano wa kimpenzi na watu wengi, la sivyo tutumie kinga. Mdudu hapa inamaanisha virusi vya ukimwi.*

Mtafitiwa MW40: *Labda kwa kuongezea kwa yale ambayo wenzangu wamesema ni kuwa, ‘uwanja mdogo’ huenda inamaanisha kuwa ni watu wachache sana amba hawana virusi vya ukimwi. Huu ujumbe naona bado haujalenga ndipo. Ni lazima mtu awe tu na mpenzi mmoja na wala si wachache.*

Watafitiwa hawa walieleza kuwa kamdudu ilimaanisha virusi vya ukimwi na CD ni kondomu. Hivyo basi kulingana nao ujumbe huu ulimaanisha kuwa watu watumie kondomu wanapofanya mapenzi. Kulingana nao ‘uwanja mdogo’ ilimaanisha kuwa ni watu wachache sana amba hawana virusi vya ukimwi. Hivyo basi mtu asiwe na uhusiano wa kimpenzi na watu wengi la sivyo atumie CD. Hata hivyo kikundi hiki kilihisi kuwa lugha iliyotumika katika bango hili ilipotosha baadhi ya wasomaji kwa vile haimwelekezi msomaji kuwa na mpenzi mmoja peke yake. Walihisi kuwa kwa kiwango fulani ujumbe huu haukulenga ndipo. Kimsingi uwanja ni eneo wazi la kufanya michezo. Mdudu ni kiumbe mdogo sana. Uwanja unarejelea mwanamke. Uwanja mdogo umetumika kumaanisha kuwa ni rahisi kukumbwa na hiyo hali ya kupata ukimwi. Kwani wanawake amba hawana virusi vya ukimwi ni wachache. Kamdudu hapa amelinganishwa na virusi vya ukimwi. Mdudu akiwa uwanjani si rahisi mtu kumwona jinsi tu mtu akiwa na virusi vya ukimwi si rahisi kuviona wala kugundua kuwa yuko navyo. Hivyo basi ujumbe huu unashauri kuwa watu watumie mpira wa kinga wanapojuhusisha kimpenzi na pia wasiwe na uhusiano wa kimpenzi na watu wengi.

B7: Ati bila CD Afadhali ikae!



Watafitiwa 20 (10%) hawakuelewa ujumbe huu unazungumzia nini. Hawa walikuwa ni baadhi ya wakufunzi rika. Kwani walikuwa na maoni sawa na huyu mtafitiwa:

Mtafitiwa MK81: *Sielewi wanazungumzia nini. Nini ikae? Ujumbe huu hauko wazi. Ni vizuri bango hili lingetueleza nini ikae. Mimi nahisi kuwa kuna sehemu ya ujumbe ambayo imeachwa nje.*

Kulingana na watafitiwa hawa, ujumbe haukuwa wazi. Walihisi kuwa haukuwa umekamilika huku wakisema kuwa kuna sehemu ambayo imeachwa nje. Watafitiwa hawa hawakuhusisha muktadha husika katika ufasiri wao. Kulingana na Leech na Short (2007) maana ya maneno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika.

Hata hivyo ujumbe huu uliweza kufasiriwa na watafitiwa 184 (90%) kutegemea muktadha husika. Watafitiwa hawa walikuwa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Aidha walikuwa na maoni sawa na ya mtafitiwa MW28 ambaye aliweza kutoa fasiri ifuatayo:

Mtafitiwa MW28: *Mimi nadhani kuwa huenda ujumbe huu unamaanisha kuwa mtu asikubali kufanya mapenzi bila ya CD, yaani kondomu au kinga.*

Kulingana na watafitiwa hawa ujumbe huu ulimaanisha kuwa mtu asikubali kufanya mapenzi pasipo kutumia CD. “CD” hapa inamaanisha kondomu yaani mpira wa kinga.

B8: Chunga usipate red card. Vaa seatbelt.



Japo ya kuwepo na fasiri kadhaa kuhusiana na ujumbe kwenye bango hili, watafitiwa 50 (25%) hawakuhusisha muktadha husika kwenye fasiri zao. Hawa walikuwa ni baadhi ya wakufunzi rika. Miongoni mwao kulijitokeza fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MK84: *Seatbelt huvaliwa wakati unaposafiri ili kuzuia ajali.*

Mtafitiwa MK86: *Ni vyema kuvalaa seatbelt ili kujikinga na hatari.*

Mtafitiwa MK87: *Ni kweli aliyosema mwenzangu ni vizuri kuvalaa seat belt ili kujikinga na hatari. Hatari hii inaweza kuwa ni kifo. Red card hapa lazima iwe inamaanisha ajali na kifo.*

Wafitiwa hawa hawakulenga ndipo katika ufasiri wa ujumbe huu kwa vile hawakurejelea muktadha husika. Wao walichukulia mkanda wa kujifunga kuwa mkanda wa kawaida waujuao ambao unapatikana kwenye gari. Watafitiwa hawa walifasiri ujumbe huu kulingana na ufahamu wao. Walieleza kuwa ni vyema kujifunga mkanda unaposafiri ili kuzuia ajali na hatari nyinginezo, kwani kwao ‘red card’ ilimaanisha hatari, ajali au kifo. Leech na Short (2007) wanashikilia hoja kuwa maana ya maneno kwa kiwango cha semantiki inastahili kuchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Wanaendelea kueleza kuwa maneno yaweza kuwa na maana isiyo ya kawaida au isiyozoleka, kwani huu ni ukiushi katika kiwango cha kisemantiki. Kulingana na wao maana hutegemea jinsi maneno yalivyotumika na wala si kama maneno hujitokeza kwa kuyatazama kijujuu.

Aidha kwa upande mwingine kuna watafitiwa 154 (75%) ambao waliweza kukisia maana ya ujumbe huu kutokana na mada ya utafiti. Hawa walikuwa ni wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Watafitiwa hawa walichunguza maana ya ujumbe kutegemea muktadha husika jinsi wanavyoshikilia Leech na Short (2007). Miongoni mwao kulikuwa na fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MW1: *Kulingana nami, kwa mujibu wa muktadha ambamo bango hili linatumika ujumbe huu unamaana nyingine. Kuna maana ya ndani ambayo hajitokezi wazi wazi. Seatbelt na red card inayorejelewa hapa si ya kawaida. Ni lazima mtu ajue muktadha unaorejelewa ndipo apate kuelewa ujumbe huu kwa sababu una wingi wa maana.*

Mtafitiwa MW15: *Naam, mimi nahisi kuwa ujumbe huu unamaanisha kuwa mtu anastahili kujikinga ili asiambukizwe na ugonjwa wa ukimwi. Kwani seatbelt inaashiria kinga na red card inamaanisha ugonjwa wa ukimwi.*

Ingawa watafitiwa hawa walidai kuwa maana ya ndani ya ujumbe huu haikujitokeza wazi wazi wao waliweza kukisia maana ya ujumbe huu kutokana na mada ya utafiti. Walisema kuwa ujumbe huu ulikuwa na wingi wa maana kutegemea muktadha. Walitambua kuwa mkanda wa kitu (seat belt) ulimaanisha kinga aichukuayo mtu anapofanya mapenzi, na kadi nyekundu (red card) ilimaanisha ugonjwa wa ukimwi.

Kadi nyekundu aghalabu hutumika katika mchezo wa kandanda. Kadi hii hupewa mchezaji ambaye amevunja sheria za uchezaji na hivyo kumsababisha asiruhusiwe kucheza mechii kadhaa (Ridder, Cramer & Hopstaken 1994). Aidha seat belt ni mkanda wa kitu cha gari. Kazi ya mkanda huu ni kusaida abiria asalimike kunapotokea ajali. Mkanda huu huvaliwa wakati mtu anaposafiri akitumia gari, na si wakati wowote. Hivyo basi ujumbe huu unamwonya

binadamu awe mwangalifu ili asipate ugonjwa wa ukimwi kwa kushauriwa atumie kinga kwa vile hauna tiba. Akiupata ataangamia.

B9: *Valia boots usidungwe na mwiba*.



Vijana 26 (13%) hawakufasiri ujumbe kwenye bango hili jinsi ilivyotarajiwa. Hawa walikuwa ni wakufunzi rika. Mionganini wao kulijitokeza fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MK99: *Kwangu mimi ujumbe huu unatueleza kuwa wakati tunapotembea katika sehemu zilizo na miiba ni vyema kuvali viatu aina ya boots kwa sababu viatu hivi ni vyatengenezaji, miiba haiwezi ikapita ndani.*

Mtafitiwa MK100: *By the way that's true. Hata katika somo la Kilimo huwa tunafunzwa tuvaae boots tunapolima ama tunapofyeka hasa sehemu zilizo na miiba especially kayapo.*

Kwa mujibu wa wanafunzi hawa ujumbe huu ulimaanisha kuwa msomaji avae viatu aina ya buti ili asidungwe na mwiba. Wanafunzi hawa hawakuhusisha ujumbe huu na muktadha husika. Wao walifafanua tu ujumbe huu kulingana na namna walivyoulewa. Watafitiwa hawa ni kiwalikilishi cha vijana ambao ni wakufunzi rika. Kulingana na wataalamu Leech na Short (2007), kwa kurejelea kiwango cha semantiki maana ya maneno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yanetumika. Hivyo basi wanafunzi hawa walistahili kuhusisha ujumbe huu na muktadha husika ili kuweza kuufasiri jinsi ilivyotarajiwa.

Kwa upande mwingine wanafunzi 178 (87%) walifasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Hawa walikuwa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili, kwani walikuwa na maoni yanayofanana na ya huyu mtafitiwa:

Mtafitiwa MW150: *Tukiangalia ujumbe huu kwa kurejelea muktadha wa ukimwi, „boots“ inamaanisha mpira wa kinga na „mwiba“ inarejelea ugonjwa wa ukimwi. Maana ya ndani ya ujumbe huu basi itakuwa kwamba tunashauriwa tuvaae mpira wa kinga ili tusipatwe na ugonjwa wa ukimwi. Haya ni matumizi ya mafumbo.*

Kulingana na wanafunzi hawa ujumbe huu ungeliweza kuelewaka vyema iwapo msomaji angelitambua muktadha ambamo ujumbe huo umetungiwa, jinsi wanavyodai wataalamu

Leech na Short (2007) ya kwamba maana ya maneno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika.

B10: Ukimwi si ajali bali ni msiba wa kujitakia.



Ujumbe katika bango hili ulizua mitazamo tofauti mionganoni mwa watafitiwa. Watafitiwa 117 (57%) walikuwa na maoni sawa na ya watafitiwa wafuatao:

Mtafitiwa MW195: *Maana ya ujumbe kwa kurejelea methali husika ni kuwa ukimwi ni aina ya ugonjwa ambao binadamu hujitafutia mwenyewe.*

Mtafitiwa MW198: *Kulingana nami bango hili linajaribu kutueleza kuwa ugonjwa wa ukimwi haupatikani kupitia ajali na hivyo haina haja kumhurumia mtu ambaye anaugua ugonjwa huu. Yeye ana uwezo wa kuepukana nao.*

Mtafitiwa MW199: *Ujumbe huu uko sawa kabisa. Kwani maambukizi ya ukimwi hayaji hivi hivi tu. Ni lazima mtu ajihusishe sana sana katika ngono na hivyo kuambukizwa.*

Watafitiwa hawa walisheheni wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Kulingana na wao maana ya ujumbe ni kuwa ukimwi ni aina ya ugonjwa ambao binadamu hujitafutia mwenyewe. Walieleza kuwa binadamu hapati ugonjwa huu wa ukimwi kupitia ajali na hivyo haina haja kumhurumia mtu ambaye anaugua ugonjwa wa ukimwi kwa vile ana uwezo wa kuepukana nao. Watafitiwa hawa waliweza kufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Kwani walielewa maana ya ndani ya methali hii. Walielewa kuwa ujumbe huu unamaanisha kuwa binadamu ana uwezo wa kujikinga kutokana na ugonjwa wa ukimwi. Watafitiwa hawa waliweza kung“amua maana ya ujumbe huu kwa kurejelea muktadha husika. Kulingana na Leech na Short (2007), maana ya ujumbe hupatikana kutegemea muktadha husika.

Aidha, kuna watafitiwa 87 (35%) ambao hawakukubaliana na ujumbe huu. Hawa walikuwa ni wanafunzi waosomea kozi ya Kiswahili. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Mionganoni mwao kulijitokeza mitazamo ifuatayo:

Mtafitiwa MW189: *Mimi sikubaliani na ujumbe huu. Hakuna mtu ambaye anatafuta ugonjwa wa ukimwi. Ni nani ambaye anatamani kuambukizwa ukimwi?*

Mtafitiwa MW190: *Hata mimi sikubaliani na ujumbe huu. Mtu anaweza kupata ukimwi kupidia ajali na hivyo si msiba wa kujitakia, kwani ajali haina kinga.*

Mtafitiwa: MW191: *Ni kweli kabisa anayosema mwenzangu, unaweza ukapata ukimwi hata kuptia kwa wembe uliotumika na mtu ambaye ana virusi. I mean kuna tu njia nyingi ambazo mtu anaweza kuambukizwa ukimwi.*


Mtafitiwa: MW192: *By the way hata mama aliye na ukimwi anaweza kuambukiza mtoto wake kupidia kwa maziwa. Hata mgonjwa wa ukimwi anaweza kuambukiza yule anayemlinda.*

Kulingana na fasiri za watafitiwa hawa ni wazi kuwa huenda hawakutambua lengo la ujumbe uliopatikana kwenye bango hili. Wao walirejelea tu maana ya methali hii jinsi inavyotumika tu katika hali ya kawaida pasipo kuihusisha na muktadha husika. Kwa mujibu wa Leech na Short (2007) maana ya ujumbe wowote ule huchunguzwa kutegemea muktadha ambamo ujumbe huo umetumika. Kulingana na watafitiwa hawa hakuna yejote ambaye angetamani kupatwa na ugonjwa wa ukimwi. Kwani mtu anaweza kupata ugonjwa wa ukimwi kupidia ajali, kupidia wembe uliotumika na mtu ambaye ana virusi, na hivyo si msiba

wa kujitakia kwani ajali haina kinga. Waliendelea kusema kuwa kuna njia nyingi ambazo mtu anaweza kuambukizwa ukimwi. Walieleza kuwa mama anaweza kumwambukiza mtoto wake ukimwi kupidia kunyonyesha na pia yule anayeuguza mgonjwa wa ukimwi vile vile anaweza kuambukizwa.

Aidha, kutokana na maoni ya hawa watafitiwa kuliibuka ukweli kinzani katika ujumbe huu. Ujumbe huu ulizua pande mbili ambazo zilikuwa zikipingana na pia zikawa na ukweli fulani ndani mwake. Upande mmoja uliwahimiza binadamu kuwa wana uwezo wa kuepukana na ugonjwa wa ukimwi. Kwani ugonjwa huu hauji tu, ni lazima mtu ajihushe na matendo fulani ndiposa aambukizwe, matendo haya yanaweza kuepukika. Kwa upande mwingine ukweli wa mambo ni kuwa mtu anaweza kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi kupidia kwa ajali. Aghalabu ajali haina kinga, hivyo basi ugonjwa huu si msiba wa kujitakia.

B13: Jijue ubambishe life!



Watafitiwa wote waliweza kufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Kwani wote walikuwa na maoni sawa na ya huyu mtafitiwa:

Mtafitiwa MW71: *Ujumbe huu kulingana na mimi unamaanisha kuwa ujjue ufurahie maisha. Yaani ukishajua hali yako utaweza kufurahia maisha.*

Hata hivyo kulingana na mtazamo wa watafitiwa hawa ni wazi kuwa hamna yeote ambaye alielewa maana sanifu ya msamiati „bamba.“ Watafitiwa wote walichukulia neno hili kumaanisha kufurahia. Watafitiwa hawa walifasiri ujumbe kulingana na namna walivyouelewa. Vile vile waliweza kuhusisha maana ya msamiati huu na muktadha husika. Hata hivyo kulingana na Kamusi Teule ya Kiswahili msamiati ‘bamba’ unamaanisha kubaka au kushika kwa nguvu. Msamiati ‘bamba’ umetumika katika muktadha huu kumaanisha kufurahia. Matumizi haya ya lugha yameweza kupatia msamiati “bamba” maana mpya. Hali hii inatokana na athari za matumizi ya kilugha cha sheng. Hali hii inashiria kuwa sheng hupotosha maana halisi ya maneno ya Kiswahili kwa kuyapa maana nyingine. Aidha Okoto, (2015) katika utafiti wake kuhusu matumizi ya kilugha cha sheng aligundua kuwa sheng huwafanya watu waache kutumia maneno mengine ya Kiswahili wakidhani ni sheng.

B15: Mwanaume kamili hujua status yake ya HIV. Chukua test leo.



Kuhusiana na bango hili watafitiwa wote walikosea kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Kati ya watafitiwa 204 walioshiriki katika huu utafiti, watafitiwa 150 (73%) walikuwa na mtazamo sawa na wa huyu mtafitiwa:

Mtafitiwa MW164: *Ujumbe unawahimiza wanaume kupima ili kujua iwapo wanaugua ugonjwa wa ukimwi au la. Kusema mwanaume kamili inamaanisha mwanaume aliyesawa, hana ugonjwa yaani amekamilika.*

Watafitiwa hawa walifasiri ujumbe jinsi walivyouelewa. Kulingana na watafitiwa hawa mwanamume kamili ni yule ambaye hana ugonjwa wa ukimwi. Watafitiwa hawa hawakufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Hapa palikuwa na ukiushi wa kisemantiki. Leech na Short (2007) wanaeleza kuwa ukiushi wa kisemantiki una maana ya maana zisizowazi na ambazo hazina umantiki. Ukiushi huu hudhihirisha kuwa neno laweza kuwa na maana isiyo ya kawaida au isiyozoleka. Kulingana na wao maana hutegemea matumizi yake, haitegemei

jinsi neno linavyojoitokeza kwa kulitazama kijujuuu. Aidha, “Mwanaume kamili” inarejelea mwanamume mwenye hadhi ya kukamilika katika uume, napia anaelewa hali yake ya afya na hivyo atawenza kujuu namna ya kuishi kulingana na hali yake ya afya.

Hata hivyo ujumbe kwenye bango hili ulizua mitazamo mbalimbali miongoni mwa watafitiwa 54 (27%) jinsi inavyodhiihikira katika data ifuatayo:

Mtafitiwa MW134: *Mwanaume ni mwanaume tu! Jinsia haiwezi kubadilika kulingana na hali ya mtu.*

Mtafitiwa MW135: *Mbona ujumbe huu unazungumzia mwanaume kamili, kwani wengine huwa nusu?*

Mtafitiwa MW136: *Ujumbe huu nao umezidi, ndiyo ni vizuri kuijua hali yako lakini haimaanishi kuwa wale wasiojua hali yao ni wanaume nusu.*

Watafitiwa hawa walitilia shaka ujumbe huu kwani walishangaa mbona ujumbe ulilenga tu jinsia ya kiume. Kulingana na watafitiwa hawa mwanamume ni mwanamume tu. Watafitiwa hawa vile vile hawakung“amua kuwa “mwanaume kamili” ilitumika kwa maana ya mwamume mwenye hadhi ya kukamilika katika uume, kwani hii ndiyo sifa ya kukamilika. Hata hivyo huenda ujumbe huu umelenga mwanamume kwa sababu huenda yeze ndiye chanzo cha maambukizi au yeze hujiali sana.

Jedwali la 5: Fasiri za vijana kuhusu ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi.

BANGO	Idadi/asilimiaya vijana waliofasiri ujumbe kwenye mabango jinsi ilivyotarajiwa.	Idadi/asilimiaya vijana waliokosa kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa.
B1	160 (78%)	44 (22%)
B2	155 (76%)	49 (24%)
B3	1 (0.49%)	203 (99.51%)
B4	161 (78%)	43 (21%)
B5	154 (75%)	50 (25%)
B6	134 (65%)	70 (35%)
B7	184 (90%)	20 (10%)
B8	154 (75)	50 (25%)
B9	178 (87%)	26 (13%)
B13	204 (100%)	0 (0%)
B15	0 (0%)	204 (100%)
JUMLA	1331 (76%)	420 (24%)

Chanzo: Uchanganuzi wa mtafiti.

4.2.1 Hitimisho

Katika sehemu hii tulipambanua fasiri zilizotolewa na watafitiwa na hivyo tuliegemea upande wa kiwango cha semantiki kwa sababu ndicho kiwango ambacho huchunguza lugha katika kiwango cha maana. Kiwango hiki huchunguza maana ya maneno yanayopatikana katika lugha (Leech & Short, 2007). Watafitiwa walifasiri jumbe kulingana na ufahamu wao. Kutokana na data ya fasiri zilizotolewa na watafitiwa imebainika wazi kuwa watafitiwa

walifasiri ujumbe kwa njia mbalimbali zinazohitilafiana. Kila mmoja alifasiri ujumbe kulingana na ufahamu wake. Barthes (1984), katika utafiti alioufanya kuhusu matangazo ya biashara aligundua uwepo wa fasiri tata na polisemi za maana. Utafiti huu vile vile umeweza kufichua fasiri tata katika jumbe zinazopatikana kwenye mabango ya ukimwi. Kuna fasiri duni na fasiri bora kutegemea tajriba ya mpokezi. Matumizi ya lugha fiche iliyofumba maana kadha yalisababisha uibuaji wa fasiri nyingi za maana. Matumizi ya lugha tata yaliweka wazi uchangamano uliokuwa changamoto kubwa kwa watafitiwa. Aidha Tompkins (1980) na Fish (1970) wanatetea hoja kuwa maarifa ya kimsingi na tajiriba ya usomi aliyonayo msomaji huathiri namna ambavyo atafasiri ujumbe fulani. Asilimia 24% ya watafitiwa walitoa fasiri zilizotofautiana. Asilimia hii ilijumuisha watafitiwa amba o walikuwa ni wakufunzi rika. Wakufunzi rika hawa hawakuwa na tajiriba na umilisi katika lugha ya Kiswahili. Huenda hali hii ndiyo iliyochangia katika uwepo wa fasiri zilizohitilafiana. Fasiri hizi tofauti tofauti zilisababisha ujumbe kupata maana tofauti. Jambo hili linapotokea jukumu la ujumbe huwa halijatimilika. Aidha tofauti kati ya fasiri hizi ilijitokeza wakati ambapo watafitiwa pia walikosa kuhusisha ujumbe na muktadha husika.

Kulingana na Leech na Short (2007) katika kiwango cha semantiki maana ya ujumbe huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo ujumbe huo umetumika. Wanaendelea kueleza kuwa ukiushi wa kisemantiki una maana ya maana zisizo wazi na ambazo hazina umantiki. Ukiushi huu hudhihirisha kuwa neno laweza kuwa na maana isiyo ya kawaida au isiyozoleka. Maana hutegemea matumizi yake, haitegemei namna neno linavyojitokeza kwa kulitazama kijujuu.

4.3 Mitazamo ya vijana kuhusu mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi

Mitindo ya lugha ni jumla ya mbinu au sifa zinazomwezesha mwandishi kuuwasilisha ujumbe wake (Wamitila 2000). Dhana hii inarejelea sifa maalum za maandishi. Mabango yaliyorejelewa katika sehemu hii ni pamoja na *B2: Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD, B1: Usilambe asali katika kila nyumba, B8: Chunga usipate red card. Vaa seatbelt, B9: Valia boots usidungwe na mwiba, B6; Uwanja mdogo kamdudu kako. Tumia CD, B10: Ukimwi si ajali bali ni msiba wa kujitakia, B11: Mwanangu, ngoja kwanza, la sivyo jikinge kila wakati. Fungua roho yako, Ongea, B12: Si hu-test regularly kujua status yetu. Bila worries life inabamba, B3: Sisi tumeingia kwa network juu tunajua hali yetu ya HIV, B14; Mwanzo na mwisho wa mawazo G-jue hali yako ya HIV. Tu-meet VCT Centre au Hosi karibu na mtaa, B15; Mwanamume kamili hujua status yake. Chukua test leo, B7: Ati bila CD Afadhali ikae!, B13: Jijue ubambishe life.* Watafitiwa waliweza kubainisha matumizi ya mitindo mbalimbali ya lugha katika mabango haya. Mitindo iliyobainishwa ni pamoja na stiari, jazanda, mafumbo, majazi, methali, taharuki, sheng, kinaya, tasfida, kuchanganya ndimi na taswira. Watafitiwa walikuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu matumizi ya mitindo hii kama inavyodhihirika katika data ifuatayo:

4.3.1 Sitiari

Kwa mujibu wa Wamitila (2003) sitiari ni ulinganisho usiokuwa wazi. Sifa ya kitu kimoja inahamishwa kwa kingine bila ya kuwepo kwa viungo. Wamitila (2003) anaendelea kusema

kuwa sitiari huwasilisha ujumbe kwa njia bora na toshelevu inapotumika katika maandishi. Brieley (1995) naye anasema kuwa sitiari ni ulinganisho ambapo kitu kimoja hulinganishwa na wazo ambalo linarejelewa. Kulingana naye sitiari hutumika kwenye matini ili kuwasilisha ujumbe kwa njia ya kuboresha kumbukizi za wasomaji kuhusu ujumbe unaotangazwa kwa vile wao hulazimika kutafakari kuhusu sitiari zilizotumika. Watafitiwa walibaini matumizi ya sitiari katika mabango yafuatayo:

B2: *Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.*



Kuhusu bango hili watafitiwa 152 kwa 204 (75%) walitambua matumizi ya sitiari katika ujumbe huu. Kati ya watafitiwa hawa kuna wanafunzi 5 ambao walikuwa ni wakufunzi rika na wanafunzi 147 ambao walikuwa wanasomea kozi ya Kiswahili. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Mmoja wao alielezea haya huku wenzake 151 wakiwa na maoni sawa na yake.

Mtafitiwa MW14: *Kulingana nami ujumbe huu ni ujumbe ambao una maana fiche. Tukitazama bango hili pale chini kuna ujumbe ambao unatueleza kuwa tuvae CD. Na hisi kuwa kuoga huku si kwa kawaida. Kuoga huku kuna maanisha hali ya kufanya mapenzi, na hivyo tunaonywa kuwa tusifanye mapenzi bila kinga, yaani tusioge tukiwa uchi. Haya ni matumizi ya istiari pamoja na mafumbo.*

Watafitiwa hawa walitambua kuwa bango hili limetumia mtindo wa sitiari katika kuwasilisha ujumbe. Kulingana na watafitiwa hawa, „kuogelea mto Nyando naked“ kumelinganishwa na masuala ya mapenzi. Watafitiwa waliendelea kusema kuwa ujumbe huu unawaonya wasomaji kuhusu ugonjwa wa ukimwi. Kwani wanashauriwa kutumia mpira wa kinga.

Matumizi ya sitiari katika bango hili iliathiri maana ya ujumbe. Kwani msamati uliotumika katika ujumbe huu una maana ambayo si ya kawaida. Mathalani “kuogelea mto Nyando” imetumika kurejelea masuala ya mapenzi. Mto Nyando imetumika kurejelea binadamu.

Aidha kuna watafitiwa 52 (25%) ambao hawakutambua matumizi ya sitiari katika bango hili. Watafitiwa hawa walikuwa ni wakufunzi rika. Mmoja wao alitoa maoni yafuatayo huku watafitiwa 51 wakiwa na maoni sawa na yake.

Mtafitiwa MK119: Naam, nakubaliana na mwenzangu, ndani ya mto huwa tuna wanyama hatari ambao wanaweza kutuvamia na hivyo kuhatarisha maisha yetu. Kwa hivyo ni muhimu kuogelea ukiwa na nguo ili kuwa tayari kutoka hatari ikitokea.

Watafitiwa hawa walifasiri ujumbe huu kulingana na maana ya kawaida ya msamiati uliotumika kwenye ujumbe. Sababu ni kuwa hawakutambua matumizi ya sitiari katika ujumbe kwenye bango hili. Kulingana na Leech na Short (2007) matumizi ya lugha huathiri maana kwa njia fulani. Wanaendelea kusema kuwa ukiushi katika kiwango cha kisemantiki unahusu matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali ya kawaida. Aghalabu huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Maneno yaliyotumika kwenye ujumbe huu yamehusishwa na maana ambayo si ya kawaida. Hivyo basi ili ujumbe huu uweze kufasiriwa jinsi ilivyotarajiwa msomaji anahitaji kutambua matumizi ya sitiari, na hata kuhusisha ujumbe husika na muktadha husika.

B1: Usilambe asali katika kila nyumba.



Kuhusiana na ujumbe katika bango hili watafitiwa 140 (67%) walitambua matumizi ya sitiari. Hawa walikuwa ni wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Baadhi ya watafitiwa hawa walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW51: *Ujumbe huu unatuonya kuwa tusiwe watu wa kufanya mapenzi na kila mtu.*

Mtafitiwa MW58: *Kulingana nami nahisi kuwa huu ujumbe unatutahadharisha kuwa tuweze kudhibiti tama za kimwili. Tusifanye mapenzi na kila mtu.*

Mtafitiwa MW59: *Kwangu, naona kuna matumizi ya sitiari katika ujumbe huu, yaani ile hali ya kulinganisha vitu viwili na usitumie kiunganishi. Neno „„asali““ limelinganishwa na mapenzi. Ama nyinyi mnaonaje?*

Hawa watafitiwa walitambua kuwa msamiati „asali“ ulilinganishwa na suala la mapenzi. Waliweza kufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa kwa sababu walielewa maana ya matumizi ya mbinu ya sitiari. Kulingana na Leech na Short (2007), ukiushi katika kiwango cha semantiki unahusu matumizi ya maneno na jinsi maana hiyo inavyofasiriwa katika hali za kawaida. Aidha huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Katika matumizi ya sitiari maneno hulinganishwa na maana ambazo si za kawaida.

Aidha kuna watafitiwa 64 (31%) ambao hawakutambua matumizi haya ya sitiari katika ujumbe huu. Miongoni mwa watafitiwa hawa 14 (6 .5%) walikuwa ni wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili huku watafitiwa 50 (24.5%) wakiwa ni wakufunzi rika. Baadhi ya watafitiwa hawa walikuwa ni wanafunzi waosomea kozi ya Kiswahili. Miongoni mwao kulijitokeza maoni haya:

Mtafitiwa MK101: *Kwangu ujumbe huu unatuonya kuwa tusile chakula kwa nyumba za watu ovoyovo.*

Mtafitiwa MK108: *Mimi naonelea kuwa ujumbe kwenye hii bango unatuambia kuwa ni vizuri kula chakula kwenye nyumba za watu unaowajua.*

Mtafitiwa MK114: *Kuna hatari katika kula chakula katika kila nyumba, huenda ukapewa sumu.*

Kutoweza kutambua matumizi ya sitiari katika ujumbe huu na watafitiwa hawa kuliwasababisha kushindwa kufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Kulingana na Leech na Short (2007), kuna ukiushi katika kiwango cha kisemantiki ambapo maneno huhusishwa na maana ambazo si kawaida. Sitiari aghalabu huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huu ni ukiushi katika kiwango cha kisemantiki. Maneno yaliyotumika kwenye ujumbe huu yamehusishwa na maana ambayo si ya kawaida. Msomaji alihitajika kutambua matumizi ya sitiari ndiposa aweze kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Asilimia kubwa ya watafitiwa hawa walikuwa ni wakufunzi rika, hivyo hawana tajiriba na umilisi katika lugha ya Kiswahili. Huenda hali hii ndiyo iliyochangia kwa wao kukosa kufasiri ujumbe kwenye bango hili jinsi ilivyotarajiwa.

Aidha mtaalamu Iser (1974) anasema kuwa msomaji hufasiri ujumbe au matini kulingana na tajiriba yake ya usomi. Kwa kawaida asali ni kitu kiowevu na kitamu sana. Mwonja asali haonji mara moja, aidha fuata nyuki ule asali. Msamati asali umelinganishwa na masuala ya kimapenzi kwa vile huenda mapenzi ni tamu mithili ya asali na anayeyaonja hataonja tu mara moja na hivyo yumo katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi.

4.3.2 Mafumbo

Mafumbo kwa mujibu wa Wamitila (2003) hutumiwa kueleza kauli ambazo huficha maana fulani. Huwa kuna jambo ambalo limefumbwa ambalo msomaji anahitajika kufumbua. Momanyi (2001) anaongezea kwa kusema kuwa mafumbo huwa na ujumbe ambao umefumba mambo fulani ambayo msomaji anastahili kuyafumbua ndiposa aweze kuelewa ujumbe huo. Aidha, Leech na Short (2007) wanaeleza jinsi matumizi ya lugha yanavyoathiri maana kwa njia fulani. Ukiushi wa aina hii mara nyingi huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Katika matumizi ya mafumbo maneno huhusishwa na maana ambazo si za kawaida. Watafitiwa waliweza kutambua matumizi ya mafumbo katika mabango yafuatayo:

B8: Chunga usipate red card. Vaa seat belt.



Watafitiwa 144 (71%) walitambua matumizi ya mafumbo katika usimbaji wa ujumbe huu. Kwani watafitiwa 151 walikuwa na maoni sawa na ya hawa watafitiwa MW33 na MW34 ambao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW33: *Tukiangalia muktadha ambamo bango hili limetumika maana inayojitokeza ni tofauti kabisa, Kwani „chunga usipate red card“ ina maanisha kuwa uchunge usipate ugonjwa wa ukimwi. „Red card“ inamaanisha ugonjwa wa ukimwi ambao ni hatari sana. „vaa seatbelt“ nayo inamaanisha kucaa mpira wa kinga.*

Mtafitiwa MW34: *Ni kweli asemayo mwenzangu, hili kweli ni fumbo, lazima mtu afikirie kweli kweli ndiyo apate kufumbua.*

Watafitiwa hawa walitambua kuwa ujumbe huu una maana tofauti. Kwa mujibu wa Brieley (1995) mafumbo ni matumizi ya lugha yenyе maana fiche. Kulingana na wao, maana ya ujumbe huu ni kuwa mtu anastahili kujichungu ili asiambukizwe ugonjwa wa ukimwi. Kwani “red card” iliimaanisha ugonjwa wa ukimwi na “vaa seat belt” ilimaanisha kucaa mpira wa kinga. Kulingana na Leech na Short (2007) mafumbo huhushishwa na matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Huu ni ukiushi katika kiwango cha kisemantiki.

Isitoshe, kwa upande mwingine kuna watafitiwa 60 (29%) ambao hawakutambua matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Kati ya hawa watafitiwa 3 (1.4%) walikuwa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili, na 57 (27.6%) walikuwa ni wakufunzi rika. Hawa walikuwa na maoni yanayofanana. Mmoja wa watafitiwa hawa alisema haya:

Mtafitiwa MK63: *Ujumbe ulio kwenye bango hili unaeleweka tu kwa yule ambaye anatambua na kuelewa maana ya mitindo ya lugha iliyotumika, kwa wale ambao hatutambui wala kuelewa mitindo hii hatuwezi kufasiri maana ya ujumbe huu jinsi ilivyokusudiwa.*

Matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu yaliwasababisha watafitiwa hawa kutoelewa ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Kuna wale ambao walitambua matumizi haya ya mafumbo lakini hawakuja namna ya kuufasiri ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Kulingana na mtafitiwa mmoja msamiati „red card“ ulimaanisha kifo, kwani alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MK87: Ni kweli aliyosema mwenzangu ni vizuri kuvala seat belt ili kujikinga na hatari. Hatari hii inaweza kuwa ni kifo. Red card hapa lazima iwe inamaanisha kifo.

Mtafitiwa huyu alitambua kuwa msamiati „red card“ ilikuwa na maana nyingine licha ya kutoweza kuufasiri jinsi ilivyotarajiwa hata baada ya kuelezwu kuhusu mada ya utafiti. Hii inamaanisha kuwa baadhi ya watafitiwa hawakuweza kutambua maana ya msamiati fulani kutegemea muktadha ambamo maneno haya yalitumika. Kulingana na Leech na Short (2007) maana ya maneno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Aidha mtindo wa mafumbo huhusisha matumizi ya maneno kwa njia ambazo si za kawaida kimaana. Hali hii inahusishwa na ukiushi katika kiwango cha kisemantiki kwa vile maneno yaliyotumika kwenye ujumbe yamehusishwa na maana ambayo si ya kawaida.

Ili kufasiri ujumbe jinsi inavyotarajiwa ni sharti msomaji aweze kufumbua fumbo husika na pia kuhusisha ujumbe na muktadha husika. Vijana hawa waliweza kufasiri ujumbe huu kulingana na namna walivyoulewa na wala si kulingana na muktadha ambao ulihusika, jambo lililowasababisha kutofasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa.

Kadi nyekundu mara nyingi hutumika katika michezo ya kandanda wakati mchezaji huwa amevunja sheria za uchezaji ili kumsimamisha kucheza mechili kwa muda fulani. Aidha, kabla mchezaji kupewa kadi nyekundu, yeche hupewa onyo kuitia kadi ya manjano na iwapo ataendelea kuvunja marsharti ya michezo ndipo anapopewa kadi nyekundu. Aidha seat belt ni mkanda wa kiti cha gari. Kazi ya mkanda huu ni kusaidia abiria asalimike kunapotoka ajali. Mkanda huu huvaliwa wakati mtu anaposafiri akitumia gari, na si wakati wowote. Hivyo basi ujumbe huu unamwonya binadamu awe mwangalifu ili asipate ugonjwa wa ukimwi kwa kushauriwa atumie kinga kwa vile hauna tiba. Akiupata ataangamia.

B9: Valia boots usidungwe na mwiba.



Watafitiwa 178 (87%) walitaja matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Kati ya watafitiwa hawa 147 (72%) walikuwa wanafunzi wanosomea kozi ya Kiswahili na 31 (15%) walikuwa wakufunzi rika. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa na ya huyu mtafitiwa.

Mtafitiwa M150: Tukiangalia ujumbe huu kwa kurejelea muktadha wa ukimwi, 'boots' inamaanisha mpira wa kinga na 'mwiba' inarejelea ugonjwa wa ukimwi. Maana ya ndani ya

ujumbe huu basi itakuwa kwamba tunashauriwa tuvae mpira wa kinga ili tusipatwe na ugonjwa wa ukimwi. Haya ni matumizi ya mafumbo.

Kulingana nao, ujumbe unaopatikana katika bango hili una maana ya juu na maana batini. Walieleza maana ya juu inayojitokeza katika ujumbe huu ni kuwa msomaji avae viatu aina ya buti ili asidungwe na mwiba. Watafitiwa hawa walirejelea muktadha husika. Maana batini ndiyo iliyokusudiwa katika ujumbe huu. Maana ya msamiati ‘boots’ ilichunguzwa kutegemea muktadha ambamo neno hili lilikuwa limetumika. Ili ujumbe huu uweze kuelewaka ni lazima msomaji aweze kuhusisha dhana ya kuvalaa viatu na kutodungwa na mwiba na ile hali ya kujikinga na ugonjwa wa ukimwi. Kwa mujibu wa watafitiwa, katika muktadha huu msamiati ‘boots’ ulimaanisha mpira wa kinga na msamiati ‘mwiba’ ukamaanisha ugonjwa wa ukimwi. Kulingana nao maana batini ya ujumbe huu ni kuwa msomaji anaambiwa avae mpira wa kinga ili asipate ugonjwa wa ukimwi. Tukirejelea Leech na Short (2007), maana ya maneno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika. Aidha, Lawal (1997), anasema kuwa semantiki huchunguza maana ya kimuktadha lakini yenye kuwa na msingi kuhusiana na maana msingi. Kutohama na maana msingi, maneno huhushishwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi. Aidha, watalamu Andrew Bennet na Nicolas Royle (1995) wanatetea hoja kuwa jamii hushiriki mfumo wa kanuni na taratibu zinazokubalika na jamii husika. Jamii moja huweza kutumia ishara za aina sawa na kuelewana katika ufasiri wa maana ya ujumbe. Hata hivyo ufasiri hutofautiana kwa watu binafsi.

Buti ni aina ya kiatu kilicho na sifa za kipekee. Ni kiatu kikubwa hasa cha ngozi. Katika jamii nyingi hapa nchini buti ni aina ya kiatu ambacho huweza kufunika kisigino na wakati mwingine huweza kufikia sehemu ya chini ya muundi na huvaliwa katika mazingira yaliyo na


hatari ili kiweze kuukinga mguu ili usumizwe. Muktadha ambaa umehusika katika utungaji wa ujumbe huu ni udhibiti wa ugonjwa wa ukimwi.

Hata hivyo kuna baadhi ya watafitiwa 26 (13%) ambaa hawakuelewa maana batini ya ujumbe huu. Hawa walikuwa ni wakufunzi rika. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Wawili wao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MK99: *Kwangu mimi ujumbe huu unatueleza kuwa wakati tunapotembea katika sehemu zilizo na miiba ni vyema kuvalaa viatu aina ya boots kwa sababu viatu hivi ni vya nguvu, miiba haiwezi ikapita ndani.*

Mtafitiwa MK100: *By the way that “s true. Hata katika somo la Kilimo huwa tunafunzwa tuvae boots tunapolima ama tunapofyeka hasa sehemu zilizo na miiba especially kayapo.* Watafitiwa hawa hawakutambua wala kuelewa matumizi ya mafumbo na hata kutambua maana ya ujumbe huu kulingana na muktadha ambamo umetungiwa. Wao waliufafanua kulingana na namna walivyoulewa .Watafitiwa hawa ni kiwalikilishi cha wanafunzi ambaa ni wakufunzi rika.

B6: Uwanja mdogo, kamdudu kako. Tumia CD.



Kuhusu ujumbe kwenye bango hili, watafitiwa 134 (65%) waligundua matumizi ya mafumbo. Hawa walikuwa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Baadhi yao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW16: *Ni kweli, mwenzangu amesema ukweli. Hata pia kuna matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Uwanja unaozungumziwa hapa si uwanja wa kawaida. Wanamaanisha masuala ya mapenzi.*

Mtafitiwa MW36: *Mimi naona kuwa ujumbe huu una maana ambayo ni tofauti kabisa na ile inayojitokeza kijuujuu, kwani haurejelei uwanja wa kawaida. Ujumbe huu unatuonya kuwa tusiwe na uhusiano wa kimapenzi na watu wengi, la sivyo tutumie kinga. Mdudu hapa inamaanisha virusi vya ukimwi.*

Mtafitiwa MK40: *Labda kwa kuongezea kwa yale ambayo wenzangu wamesema ni kuwa, „uwanja mdogo“ huenda inamaanisha kuwa ni watu wachache sana ambao hawana virusi vya ukimwi; na naona bado haujalenga ndipo. Ni lazima mtu awe tu na mpenzi mmoja na wala si wachache.*

Mafumbo, kwa mujibu wa Brieley (1995) ni mtindo wa kuficha maana ya kinachoelezwa ambapo neno lililotumika linaweza kuwa na maana zaidi ya alichokieleza ambacho hakionekani wazi. Watafitiwa hawa walieleza kuwa kamdudu ilimaanisha virusi vya ukimwi na CD ni kondomu. Hivyo basi kulingana nao, ujumbe huu ulimaanisha kuwa watu watumie kondomu wanapofanya mapenzi. Kulingana nao „uwanja mdogo“ ulimaanisha kuwa ni watu wachache sana ambao hawana virusi vya ukimwi. Hivyo basi mtu asiwe na uhusiano wa kimapenzi na watu wengi la sivyo atumie CD. Hata hivyo kikundi hiki kilihisi kuwa lugha iliyotumika katika bango hili ilipotosha baadhi ya wasomaji kwa vile haimwelekezi msomaji kuwa na mpenzi mmoja pekee yake. Walihisi kuwa kwa kiwango fulani ujumbe huu haukulenga ndipo. Uwanja huwa ni eneo wazi la kufanya michezo. Mdudu ni kiumbe mdogo sana. Uwanja unarejelea mwanamke. Uwanja mdogo umetumika kumaanisha kuwa wanawake ambao hawana virusi vya ukimwi ni wachache. Kamdudu hapa amelinganishwa na virusi vya ukimwi. Mdudu akiwa uwanjani si rahisi mtu kumwona kama vile mtu akiwa

na virusi vya ukimwi si rahisi kuviona wala kugundua kuwa yuko navyo. Hivyo basi, ujumbe huu unashauri kuwa watu watumie mpira wa ukimwi wanapoijishisha kimpenzi na pia wasiwe na uhusiano wa kimpenzi na watu wengi. Kwa upande mwingine kuna watafitiwa 70 (35%) ambao hawakutambua matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Kati yao kulikuwa na watafitiwa 13 (6.4%) ambao walikuwa wanaomea kozi ya Kiswahili na watafitiwa 57 (28.6%) walikuwa ni wakufunzi rika. Asilimia kubwa ya watafitiwa hawa walikuwa ni wakufunzi rika, yaani wale ambao hawasomei kozi ya Kiswahili. Baadhi yao walitoa maoni yafuatayo:

Mtafitiwa MK102: *Uwanja ukiwa mdogo itakuwa ni vigumu watu kuutumia. Na kwanza wanasema kamdudu kako, si basi uwanja huu ni mbaya kwa binadamu kuchazea.*

Mtafitiwa MK103: *Hata kama uwanja ni mdogo, si unaweza kutafuta uwanja mwingine mkubwa?*

Mtafitiwa MK117: *Kamdudu ni kitu kidogo sana ambacho chaweza kuangamizwa na mtu yeyote.*

Mtafitiwa MK121: *Ujumbe huu haueleweki waziwazi kwani uwanja, kamdudu na CD vina uhusiano upi?*

Mtafitiwa MK125: *Ni CD ipi inayozungumziwa?*

Watafitiwa hawa hawakutambua matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Wao walijikita katika maana ya juu ya ujumbe huu. Baadhi yao walisema kuwa uwanja huo ulikuwa mdogo na pia ulikuwa umevamiwa na wadudu na hivyo haungekuwa mzuri kutumiwa na binadamu. Aidha walihisi kuwa mja ana uhuru wa kutafuta uwanja mwingine mkubwa. Vile vile kulingana na wao mdudu ni kiumbe mdogo sana ambaye anaweza kuangamizwa na mtu yeyote, hivyo basi haukuelewa kwa nini kiumbe mdogo hivyo kumhangisha binadamu. Walidai kuwa ujumbe huo haukueleweka waziwazi kwa sababu kulingana nao, hakuna uhusiano wowote kati ya uwanja, kamdudu na CD. Watafitiwa hawa haukurejelea muktadha husika katika ufasiri wa ujumbe huu. Leech na Short (2007) wanasema kuwa maana ya ujumbe huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo ujumbe huo umetumika.

B1: Usilambe asali katika kila nyumba.



Watafitiwa 160 (78%) waliweza kutambua matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Watafitiwa 147 (72%) walikuwa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili na watafitiwa 21 (10%) walikuwa ni wakufunzi rika. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Miongoni mwao kulijitokeza fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MW41: *Ujumbe huu unatuonya kuwa tusiwe watu wa kufanya mapenzi na kila mtu.*

Mtafitiwa MW51: *Kulingana nami nahisi kuwa huu ujumbe unatutahadharisha kuwa tuweze kudhibiti tamaa za kimwili. Tusifanye mapenzi na kila mtu.*

Mtafitiwa MW58: *Huu ujumbe una maana fiche. Kuna matumizi ya mafumbo. Mimi nasema hivi kwa sababu ya muktadha ambamo umetumiwa. Kwani asali inayozungumziwa si ya kawaida. Asali hapa inamaanisha mapenzi na kulamba ni kile kitendo cha kufanya mapenzi. Kwa hivyo mimi nakubaliana na wenzangu wanaosema kuwa ujumbe huu unamaanisha kuwa tusifanye mapenzi na kila mtu.*

Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Walisema kuwa ujumbe huu ulikuwa na maana fiche huku wakieleza kuwa maana ya ndani ya ujumbe huu ni kuwa msomaji asifanye ngono na kila mtu. Kulingana na watafitiwa hawa „asali“ ilimaanisha mapenzi na kitendo cha „Kulamba asali“ kilimaanisha kufanya mapenzi, na „kila nyumba“ ilitumika kumaanisha kila mtu. Walieleza kuwa ujumbe huu umetumika kuonya wasomaji dhidi ya tabia ya kuwa na uhusiano wa kimapenzi na kila mtu ovyo ovyo. Watafitiwa hawa walitambua matumizi ya

mafumbo na hivyo kuweza kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajija. Kulingana na Leech na Short (2007), aghalabu maneno huhushwa na maana ambazo si za kawaida. Aidha maana ya maneno hutegemea matumizi yake na wala si namna neno linavyojitokeza kwa kulitazama kijuujuu. Katika matumizi ya mafumbo maneno huhushwa na maana ambazo si za kawaida, huu ni ukiushi katika kiwango cha kisemantiki. (Leech & Short, 2007). Kwani maneno huhushwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi.

Aidha, watafitiwa hawa walieleza kuwa huenda mbinu ya mafumbo ilitumika katika bango hili kuashiria mambo ambayo hayazungumzwi wazi wazi katika jamii kwa minajili ya heshima. Mtafitiwa mmoja alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW43: *Mimi nadhani aina hii ya lugha imetumika kwa sababu ya kuwaheshimu watu. Wajua kuna mambo fulani katika jamii ambayo watu hawayasemi wazi wazi, yaani wanaona aibu kuyazungumzia.*

Watafitiwa 102 (50%) walihisi kuwa ujumbe huu ulisimbwa kwa mafumbo kwa vile ulilenga kundi fulani la watu katika jamii. Mmoja wa watafitiwa hawa alikuwa na haya ya kusema huku watafitiwa wenzake wakiwa na maoni sawa na yake.

Mtafitiwa MW46: *Kwa upande wangu mimi nadhani kuwa mafumbo yametumika kwa vile aliyeandika ujumbe huu huenda hakutaka watu fulani waelewe ujumbe huu hasa watoto. Nadhani yeye amelenga tu vijana.*

Kutokana na majadiliano haya, utafiti huu ultambua kuwa katika mabango ya ukimwi huenda mitindo ya mafumbo ilitumika kwa kiwango fulani ili kudhibiti hadhira. Baadhi ya mabango haya yalilenga hadhira fulani katika jamii hasa vijana. Matokeo haya ni sawa na maoni ya Guowen (2008) ambaye anadai kuwa mitindo ya lugha ilitumika kwenye mabango kama hila ya kudhibiti hadhira fulani.

Kwa upande mwingine kuna watafitiwa 44 (22%) ambao hawakutambua matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu jinsi inavyodhahirika katika data ifuatayo, watfitiwa hawa walikuwa ni wakufunzi rika.

Mtafitiwa MK101: *Kwangu ujumbe huu unatuonya kuwa tusile chakula kwa nyumba za watu ovoyovyo.*

Mtafitiwa MK108: *Mimi naonelea kuwa ujumbe kwenye hii bango unatuambia kuwa ni vizuri kula chakula kwenye nyumba za watu unaowajua.*

Mtafitiwa MK114: *Kuna hatari katika kula chakula katika kila nyumba, huenda ukapewa sumu.*

Mtafitiwa MK122: *Lakini mimi naona kuwa hii bango inamaanisha kuwa hata kama asali ni tamu namna gani ni vizuri tuwe watu wa kujicontrol, tusiwe watu wa kurukiarukia mambo ya watu wengine ovyoovyo.*

Watafitiwa hawa hawakutambua kuwa ujumbe huu ulikuwa na maana fiche na hivyo kushindwa kuelewa jinsi ilivyotarajiwa. Kutokana na maoni ya watafitiwa hawa mafumbo yalikuwa kikwazo katika kuelewa kwao kwa ujumbe huu jinsi ilivyotarajiwa. Watafitiwa hawa walikuwa kiwakilishi cha wanafunzi ambao ni wakufunzi rika.

B2: *Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD*



Watafitiwa 155 (75.98%) walitambua matumizi ya mafumbo katika bango hili. Kati ya hawa watafitiwa 130 (63.73%) walikuwa ni wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili na watafitiwa 25 (12.25%) walikuwa ni wakufunzi rika. baadhi yao walitoa maoni yafuatayo:

Mtafitiwa MK113: *Mbona tu mto Nyando pekee? Kuogelea huku nafeel si kwa kawaida kwa sababu watu wakiogelea ni lazima wavue nguo kwanza. Lazima ujumbe huu una maana fiche. Hili ni fumbo.*

Mtafitiwa MK115: *Hata mimi nahisi kuwa haya ni matumizi ya mafumbo. Ujumbe huu ni fiche, ni lazima mtu afikirie sana au aulize wenzake ili kupata maana iliyokusudiwa na hatuna wakati wa mambo kama haya. Mambo kama haya ndiyo hutufanya kupuzilia mbali kusoma mabango.*

Mtafitiwa MK116: *Mimi nafeel kuwa huenda ujumbe huu unaashiria hatari iliyoko ndani ya mto Nyando na hivyo ujumbe huu unatuonya tutahadhari. Hata mimi nahisi kuwa ujumbe huu ni fumbo. Kwani kuoga huku si kwa kawaida. Ujumbe unaopashwa ni mzito.*

Mtafitiwa MW14: *Kulingana nami ujumbe huu ni ujumbe ambao una maana fiche. Tukitazama bango hili pale chini kuna ujumbe ambao unatueleza kuwa tuvae CD. Nahisi kuwa kuoga huku si kwa kawaida. Kuoga huku kuna maanisha hali ya kufanya mapenzi, na hivyo tunaonywa kuwa tusifanye mapenzi bila kinga, yaani tusioge tukiwa uchi. Haya ni matumizi ya istiari pamoja na mafumbo.*

Kutokana na majadiliano haya tunatambua kuwa watafitiwa walihisi kuwa ujumbe huu ulikuwa ni fumbo na maana yake ni fiche. Walisema kuwa ni lazima mtu afikirie kwa undani sana au atafiti ili kupata maana iliyokusudiwa ilhali muda haupo, jambo ambalo lulisababisha wao kupuuzilia mbali mabango hayo. Kulingana na Wamitila (2003) mafumbo hutumiwa

kueleza kauli ambazo huficha maana fulani. Anaendelea kusema kuwa huwa kuna jambo ambalo limefumbwa ambalo msomaji anahitajika kulifumbua ili kuweza kutoa maana inayotarajiwa. Aidha, mmoja wa watafitiwa hawa aliweza kutambua maana ya ujumbe huu kwa kurejelea muktadha husika jinsi tu Leech na Short (2007) wanavyodai kuwa maana huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo ujumbe huo umetumika.

Kwa upande mwengine watafitiwa 49 (24%) hawakutambua matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Baadhi yao walikuwa na maoni sawa na huyu mtafitiwa:

Mtafitiwa MK119: *Naam, nakubaliana na mwenzangu, ndani ya mto huwa tuna wanyama hatari ambao wanaweza kutuvamia na hivyo kuhatarisha maisha yetu. Kwa hivyo ni muhimu kuogelea ukiwa na nguo ili kuwa tayari kutoka hatari ikitokea.*

Watafitiwa hawa hawakuweza kufumbua maana fiche ya ujumbe huu hata baada ya kueleza kuhusu mada ya utafiti huu. Walichukulia kuwa ujumbe huu uliwatahadharisha kuwa huenda watu wangepatwa na hatari fulani wakiogelea na hivyo ingekuwa rahisi wao kutoka majini kwa haraka. Watafitiwa hawa walifasiri ujumbe huu jinsi walivyoufahamu.

Kwa upande mwengine Leech na Short (2007), wanaeleza kuwa kuna ukiushi wa kisemantiki ambapo maana za maneno huhushishwa na maana ambazo si za kawaida, na hivyo ni sharti maana ichunguzwe kwa undani na kwa kurejelea muktadha husika. Mathalan maneno katika bango hili yamehusishwa na maana ambayo si ya kawaida.

4.3.3 Majazi

Kulingana na Wamitila (2003) majazi ni mbinu ambayo mwandishi husawiri vifaa, wahusika, mahali na mandhari na kuyapa majina yenyenye maana fulani ambayo yanahusiana na tabia yao, mitazamo yao, matabaka yao, na maumbile yao. Matumizi ya majazi yalibainika katika bango lifuatalo;

B9: *Valia boots usidungwe na mwiba.*



Watafitiwa 145 (71%) walitaja matumizi ya majazi katika ujumbe huu. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Mmoja wa watafitiwa hawa alisema haya

Mtafitiwa MW152: *Labda tu kwa kuongeza mimi naona pia kuna matumizi ya majazi katika ujumbe huu. Msamiati „boots“ umetumika kimajazi. Ukiangalia sifa ya hivi viatu vya boots utagundua kwamba ni sawa na sifa ya mpira wa kinga. Viatu hivi vina sifa fulani ya kipekee ambayo inavifanya viwe tofauti na viatu vingine na pia vile vile hutumika katika mazingira fulani sana sana yenyenye hatari fulani ambapo usipovaa viatu vya aina hii unaweza kuumia. Tukiangalia matumizi ya mpira wa kinga pia tunatambua kuwa hutumika tu katika mazingira maalumu ambapo iwapo mtu atakosa kutumia huenda pia akaumia kwa kuambukizwa ugonjwa wa ukimwi.*

Watafitiwa hawa waliweza kubaini maana ya ujumbe huu kutegemea muktadha ambamo ujumbe umetungiwa. Kulingana na Leech na Short (2007) maana ya neno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo neno hilo limetumika. Watafitiwa hawa walisema kuwa msamiati „boot“ ultumika kimajazi. Kulingana na maoni yao walidai kuwa viatu aina ya buti ni viatu ambavyo vina sifa za kipekee ikilinganishwa na viatu vya kawaida na pia hutumika katika mazingira yenyenye hatari fulani ambapo visipovaliwa kwenye mazingira hayo mtu anaweza kuumia mguu. Hivyo basi viatu hivi hupeana kinga kwa mguu ili kuepuka hatari fulani jinsi mpira wa kinga unavyotumika ili kumuepusha mja dhidi ya ugonjwa wa ukimwi. Kulingana nao viatu aina ya „boots“ vina maumbile sawa na mpira wa kinga. Watafitiwa hawa waliweza kulinganisha maana msingi ya msamiati buti na jinsi msamiati huu hutumika katika jamii. Kulingana na Lawal (1997) maneno huhushisha na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi. Hata hivyo kuna watafitiwa 59 (29%) ambao hawakutambua matumizi ya majazi na hata maana ya ndani ya msamiati

„boots“ licha ya kuelezoa kuhusu mada ya utafiti. Hawa walikuwa ni wakufunzi rika. Miongoni mwao kulijitokeza maoni yafuatayo:

Mtafitiwa MK99: *Kwangu mimi ujumbe huu unatueleza kuwa wakati tunapotembea katika sehemu zilizo na miiba ni vyema kuvali aina ya boots kwa sababu viatu hivi ni vya nguvu, miiba haiwezi ikapita ndani.*

Mtafitiwa MK100: *By the way that's true. Hata katika somo la Kilimo tunafunzwa tuvae boots tunapolima ama tunapofyeka hasa zilizo na miiba especially kayapo.*

Watafitiwa hawa walichukulia msamati buti kumaanisha buti ya kawaida. Kwani hawakuhusisha ujumbe huu na muktadha husika ili kuweza kupata maana tarajiwa.

4.3.4 Methali

Watafitiwa walitambua matumizi ya methali katika bango hili;

B10: Ukimwi si ajali bali ni msiba wa kujitakia.



Watafitiwa 180 (88%) walitambua kuwa haya yalikuwa ni matumizi ya methali katika ujumbe huu. Watafitiwa 147 (72%) walikuwa ni wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili na watafitiwa 33 (16%) walikuwa ni wakufunzi rika. Watafitiwa wafuatao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW194: *Mimi ninaona kuwa kuna matumizi ya methali katika ujumbe huu. Methali iliyotumika hapa ni; msiba wa kujitakia hauna kilio.*

Mtafitiwa MW195: *Maana ya ujumbe kwa kurejelea methali husika ni kuwa ukimwi ni aina ya ugonjwa ambao binadamu hujitafutia mwenyewe.*

Mmoja wa watafitiwa hawa alisema kuwa ujumbe huu umeundwa kutokana na methali ‘Msiba wa kujitakia hauna kilio’ huku wengine wakiwa na mawazo sawa na yake. Methali kwa mujibu wa Wamitila (2003) ni msemo wa kimapokeo ambao una muundo fulani mahsusini unaokumbukika na unao kusudiwa kuelekeza, kuadibu, kusuta, kulaumu, na kushauri. Methali huweza ikatumiwa moja kwa moja au hata kwenye mdokezo. Sehemu ya methali imechopekwa kwenye ujumbe huu ili kuwashimiza binadamu kuwa wana uwezo wa

cuepukana na ugonjwa wa ukimwi. Kwani ugonjwa huu hauji tu, ni lazima mtu ajihusishe na matendo fulani ndiposa aambukizwe. Matendo haya yanaweza cuepukika.

Kwa upande mwingine kuna watafitiwa 24 (12%) ambao hawakutambua lengo la matumizi ya methali katika ujumbe huu. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Hawa walikuwa ni wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Miiongoni mwao kulijitokeza mitazamo ifuatayo:

Mtafitiwa MW189: *Mimi sikubaliani na ujumbe huu. Hakuna mtu ambaye anatafuta ugonjwa wa ukimwi. Ni nani ambaye anatamani kuambukizwa ukimwi?*

Mtafitiwa MW190: *Hata mimi sikubaliani na ujumbe huu. Mtu anaweza kupata ukimwi kuitia ajali na hivyo si msiba wa kujitakia, kwani ajali haina kinga.*


Mtafitiwa: MW191: *Ni kweli kabisa anayosema mwenzangu, unaweza ukapata ukimwi hata kuptia kwa wembe uliotumika na mtu ambaye ana virusi. I mean kuna tu njia nyingi ambazo mtu anaweza kuambukizwa ukimwi.*

Watafitiwa hawa waliamini fika kuwa ugonjwa wa ukimwi waweza kapatikana kuitia njia nyingi. Maoni ya watafitiwa hawa yalikuwa kweli kabisa ila hawakuelewa lengo la matumizi ya methali katika ujumbe huu. Asilimia 92% ya maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi husababishwa na ngono (WHO, 2011). Methali hii imetumika ili kuwashamasisha binadamu kuwa wanaweza cuepukana na ugonjwa wa ukimwi. Hata hivyo watafitiwa walistahili kuhusiha matumizi ya methali hii na muktadha husika ndiposa waweze kubaini lengo la matumizi ya methali hii katika bango hili. Leech na Short (2007) wanaeleza kuwa ili kubaini maana ya maneno ni vyema kuhusisha maneno hayo na muktadha ambamo yametumiwa.

4.3.4 Kinaya

Kulingana na Wamitila (2003) kinaya ni tamathali ya usemi inayomaanisha kinyume cha matarajio. Watafitiwa walitambua matumizi ya kinaya katika bango hili.

B6: *Uwanja mdogo, kamdudu kako. Tumia CD*



Watafitiwa 77 (38%) walidai kuwa kuna matumizi ya kinaya katika bango hili. Hawa walikuwa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa. Baadhi yao walisema haya:

Mtafitiwa MW53: *Mimi ninashangaa kwa nini ukimwi unalinganishwa na „kamdudu“. Neno „kamdudu“ linatupa hisia ya madharau. Hii inatufanya tuchukulie ugonjwa wa ukimwi kuwa kama kitu kidogo sana ambacho si cha muhimu.*

Mtafitiwa MW56: *Kwa upande wangu masuala ya ukimwi ni masuala mazito sana katika jamii ambayo hayastahili kulinganishwa na vitu kama kamdudu. Laiti wangelinganisha ugonjwa huu na zimwi. Ukimwi ni jinamizi, umeua watu wengi sana.*

Mtafititwa MW57: *Wajua nini, ujumbe kama huu ndio unaowafanya vijana wengi kutoshtuka na ukimwi. Unawafanya wachukulie ugonjwa huu kuwa kama magonjwa mengine ya kawaida, hata siku hizi wanasema kuwa ukimwi ni fashoni.*

Mtafitiwa MW60: *Hiki ni kinaya, kinyume cha matarajio. Huwezi ukalinganisha ugonjwa wa ukimwi na kiumbe kama mdudu. Kamdudu ni kitu kidogo sana ambacho kinaweza kuangamizwa na mtu ye yote hata mtoto mdogo.*

Watafitiwa hawa walidai kuwa ulinganisho wa ugonjwa wa ukimwi na „kamdudu“ ni kinyume cha matarajio. Walisema kuwa laiti ugonjwa huu ungalilinganishwa na zimwi.

Zimwi ni mnyama mkubwa anayeogofya. Waliendelea kusema kuwa ugonjwa huu ni jinamizi kwa sababu umeangamiza watu wengi sana, na hivyo basi kuulinganisha na kiumbe mdogo kama mdudu ni kinyume cha matarajio. Walikuwa na maoni kuwa ujumbe huu unamaanisha kuwa ugonjwa wa ukimwi si hatari kwa sababu umelinganishwa na „kamdudu.“ Kulingana nao ugonjwa wa ukimwi umechorwa kama kitu kisicho cha muhimu kwa vile umelinganishwa na kamdudu. Kwao neno kamdudu liliashiria kitu kilichodharauliwa. Walisema kuwa masuala ya ukimwi ni mazito sana katika jamii na hivyo hayastahili kulinganishwa na kiumbe mdogo kama mdudu. Waliendelea kusema kuwa ujumbe huu unawapotosha wenzao kwa kuwafanya wachukulie ugonjwa wa ukimwi kama jambo jepesi katika jamii na hivyo kutolitilia maanani. Aidha, watafitiwa hawa waliweza tu kuzingatia maumbile ya mdudu, yaani kimaumbile na wala si madhara yake. Vile vile hawakuelewa maana ya neno „mdudu“ kwa kuzingatia muktadha husika. Walichukulia mdudu anayezungumziwa kuwa yule mdudu wa kawaida. Leech na Short (2007) wanasema kuwa maana ya maneno huchunguzwa kwa kurejelea muktadha unaohusika. Kwa kawaida wadudu huwa na madhara mengi sana ambapo wasipodhibitiwa wanawenza kusababisha hasara kubwa kabisa. Aidha udogo wa maumbile ya mdudu ni mfano wa udogo wa maumbile ya virusi vya ukimwi na hata virusi ni ndogo sana kimaumbile hata kushinda wadudu kwani haviwezi kuonekana kwa macho hadi mpaka hadubini itumike. Ingawa watafitiwa hawa walidai kuwepo kwa matumizi ya kinaya kwenye ujumbe huu, kinaya hiki hakijitokezi hasa baada ya kuchunguza maana ya msamiati „mdudu“ kwa kina. Hata hivyo kwa upande mwininge kuna watafitiwa 127 (62%) ambao walihisi kuwa ujumbe huo ulikuwa sawa kabisa. Hawa walikuwa na maoni sawa. Kwani mmoja wao alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW54: *Mimi nina maoni tofauti sana na ya haya wenzangu. Kwangu mimi msamiati kamdudu umetumika kuonyesha kuwa ugonjwa wa ukimwi husababishwa na mdudu mdogo yaani „kirusi“ ambaye huenda usiweze kumwona lakini madhara yake ni makuu.*

Watafitiwa hawa walichukulia kuwa neno „mdudu“ limelinganishwa na neno ‘kirusi’ ambapo kirusi inamaanisha kiini kinachosababisha ugonjwa na si rahisi kuonekana. Kwa mujibu wa Kamusi Teule ya Kiswahili (TUKI, 2013) msamiati ‘kirusi’ hasa hutumika katika wingi wake kwa maana ya vijidudu vidogo mno ambavyo husababisha maradhi.

4.3.6 Tasfida

Kulingana na Wamitila (2003), tasfida ni matumizi ya maneno ya kupunguza ukali au uzito fulani katika ujumbe husika. Anaendelea kusema kuwa lugha inayotumika ni ya heshima na adabu kwa minajili ya kutoliweka wazi jambo au hali fulani ambayo inaweza kuwaathiri wapokezi. Kwa kuongezea, Maweja (2002), anasema kuwa katika tamaduni za Kiafrika kuna kauli ambazo sio vizuri kuzitamka mbele ya hadhira. Ili kusema alilokusudia mzungumzaji anatakiwa kutumia mbinu faafu ya kistaha. Mionganoni mwa mbinu hizo ni matumizi ya tasfida. Watafitiwa walitambua matumizi ya tasfida katika mabango yafuatayo:

B11: *Mwanangu ngoja kwanza, la sivyo jikinge kila wakati. Fungua roho yako, ongea.*



Watafitiwa 112 (55%) waligundua matumizi ya tasfida katika ujumbe huu. Hawa walikuwa wanfunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni sawa, baadhi yao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW34: *Hatuelezwi mwana anastahili kungoja nini au kujikinga dhidi ya nini.*

Mtafitiwa MW35: *Mm, ni kweli, ujumbe huu haujakamilika, kuna mambo ingine ambayo imewachwa nje. Sijui mbona hatuambiwi wazi wazi.*

Mtafitiwa MW36: *Unajua nini, kama ni mambo na ngono na ukimwi, watu wengi hawapendi kuzungumzia vitu hivi mbele ya watu. Si unaona? Ujumbe huu unarejelea mzazi na mtoto wake na ni kama mzazi anaona aibu kumwambia mambo fulani kwa kuyataja waziwazi. Labda mambo hayo yakitajwa itakuwa ni ukosefu wa heshima.*

Mtafitiwa MW37: *Naam mimi nakubaliana na wenzangu, mzazi hasemi mambo yote wazi wazi kwa sababu kuna mambo ambayo hayapaswi kuzungumzwa wazi wazi mbele ya watu.*

Ukiyasema wazi wazi itakuwa ni ukosefu wa heshima haswa mambo kuhusiana na ngono na ukimwi. Haya ni matumizi ya tasfida jinsi tu wenzangu wanasema.

Mtafitiwa MW42: *Wajua nini katika jamii nyingi utagundua kuwa si rahisi wazazi kuzungumza na watoto wao mambo kuhusiana na ngono na ukimwi na pia vijana wengi huwa hawashiriki kwa urahisi na wazazi wao kuhusu ngono na hata ukimwi. Wengi wao hushiriki na marafiki zao.*

Watafitiwa hawa walieleza kuwa masuala kuhusu ngono yalielezwa kwa kutumia mbinu ya tasfida yaani lugha ya heshima. Kwa mujibu wa watafitiwa hawa ugonjwa wa ukimwi ni mojawapo ya maswala ambayo hayakuzungumziwa wazi wazi katika jamii.

Kutokana na majadiliano haya watafitiwa waligundua kuwa ilikuwa ni wazi kuwa katika ujumbe huu kuna mambo fulani ambayo hayajaelezwa wazi wazi. Walisema kuwa ujumbe hauelezi msichana anastahili kungoja nini au kujikinga dhidi ya nini. Watafitiwa hawa walichukulia ujumbe huu jinsi ulivyokuwa bila ya kuuhusisha na muktadha husika na hivyo kukosa kukisia kile kilichokuwa kikizungumziwa. Leech na Short (2007) wanaeleza kuwa ili kuelewa ujumbe ni vyema kuuchunguza kulingana na muktadha ambamo ujumbe huo umetungiwa. Aidha kulingana na mtafitiwa MW36, masuala yanayohusiana na ngono ni masuala ambayo huonewa haya katika jamii. Kulingana na mtafitiwa MW35 ujumbe huu ulihitaji ufahamu wa awali. Kuna watafitiwa waliosema kuwa jambo lilozungumziwa katika ujumbe huu halikueleweka wazi wazi kwa sababu halikutajwa. Fauka ya haya kuna baadhi ya watafitiwa ambao walitambua kuwa jambo lilozungumziwa lilikuwa ni ngono. Wao walielewa fika kuwa masuala ya ngono hasa kati ya vijana wa kike na kiume ni mambo ambayo watu wengi hawajazoea kuzungumzia hadharani. Waliendelea kueleza kuwa vijana huona haya kuyazungumzia mambo haya mbele ya wazazi wao na wazazi vile vile huona haya kuyazungumzia mambo haya mbele ya watoto wao kwa sababu ya heshima. Matokeo haya ni sawa na maoni ya Maweja (2002) ambaye anadai kuwa tamaduni nyingi za Kiafrika zina miiko ya kiisimu ambapo maneno na misemo fulani hairuhusiwi kutajwa hadharani na iwapo itatajwa itakuwa ni kuwakosea wanajamii heshima.

B1: Usilambe asali katika kila nyumba.



Watafitiwa 108 (53%) walitambua matumizi ya tasfida katika bango hili. Hawa walikuwa ni wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Mtafitiwa mmoja alikuwa na haya ya kusema huku wengine wakiwa na maoni sawa na yake:

Mtafitiwa MW43: *Mimi nadhani kuwa aina hii ya lugha imetumika kwa sababu ya kuwaheshimu watu. Wajua kuna mambo fulani katika jamii ambayo watu hawayasemi waziwazi, yaani wanaona aibu kuyazungumzia.*

Mtafitiwa huyu alieleza kuwa huenda lugha fiche ilitumika katika bango hili kuashiria mambo ambayo hayazungumzwi waziwazi katika jamii kwa minajili ya heshima. Watafitiwa 101 walikuwa na maoni sawa na yake. Kulingana nao lugha fiche aghalabu ilitumika kwa ajili ya tasfida. Kwani walihisi kuwa matumizi ya lugha wazi ingeashiria ukosefu wa heshima. Mtafitiwa mmoja alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW137: *Ukiangalia mabango haya utagundua kuwa wametumia lugha fiche. Hakuna matumizi ya lugha wazi, lugha ya moja kwa moja haijatumika. Nadhani ni kwa sababu ya heshima. Kuna mambo fulani ambayo huwezi kuzungumza tu ovyo ovyo mbele ya watu sana sana katika jamii hizi zetu za Kiafrika.*

Watafitiwa hawa walihisi kuwa mbinu ya mafumbo ilitumika kwa ajili ya tasfida. Maweja (2002) anadai kuwa tamaduni nyingi za Kiafrika zina miiko ya kiisumu ambapo maneno na misemo fulani hairuhusiwi kutajwa hadharani na iwapo itatajwa itakuwa ni kuwakosea wanajamii heshima. Ukiushi wa kisemantiki umebainika katika ujumbe huu. Maneno katika ujumbe huu yamepewa maana ambayo si ya kawaida. Maana ya ujumbe huu haijajitokeza moja kwa moja. Leech na Short (2007), wanaeleza kuwa katika ukiushi wa kisemantiki maana ya maneno huwa haijitokezi moja kwa moja, kwani maneno huwa yanahuishwa na maana isiyo ya kawaida.

Aidha mabango mengine ambayo watafitiwa walisema kuwa yalitumia lugha ya tasfida ni haya yafuatayo:

Jedwali la 6: Idadi ya watafitiwa walitambua matumizi ya tasfida katika mabango haya.

Bango	Idadi ya walitambua matumizi ya mbinu ya Tasfida
<i>B2: Usiogelee mto Nyando naked</i>	130 (64%)
<i>B8: Chunga usipate red card, vaa seatbelt</i>	128(63%)
<i>B9: Valia boots usidungwe na mwiba</i>	115(56%)

Mbinu ya tasfida imetumiwa zaidi katika mabango yenye dhana fiche. Katika mbinu hii linalokusudiwa huwa halitajwi moja kwa moja. Inachukuliwa kuwa yanayowasilishwa yanadokeza yanayokusudiwa. Mtindo wa aina hii hutumia adabu katika lugha ili kuficha hali fulani ambayo inahisika kuwa yaweza kuwa na athari fulani iliyohasi kwa wapokezi (Wamitila 2003). Adabu ni jambo la muhimu sana katika maingiliano ya jamii yoyote ile na hivyo hudhibiti ushirikiano katika mawasiliano. Kulingana na Maweja (2002), adabu

huwa na vipimo vyake na huongezeka pindi mawasiliano yanapohusisha dhana fiche kwa kutumia mafumbo, tasfida na sitiari.

Mbinu hii imetumika katika mabango ya ukimwi kuwasilisha maswala yaliyohusisha dhana zinazobainika kuwa mwiko kutajwa wazi katika jamii hususan swala la ngono ili kudhihirisha heshima na adabu katika mawasiliano. Dhana hizo zilitajwa kwa njia ya kimafumbo ili mpokezi ajikakamue kubaini maana ya ujumbe.

4.3.7 Kuchanganya Ndimi

Watafitiwa walibainisha mbinu hii katika mabango yafuatayo:

B12: Si hu-test regularly kujua status yetu. Bila worries life inabamba.



Matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi yalitambuliwa katika bango hili na watafitiwa 204 (100%) wote. Mmoja wao alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW156: *Kuna matumizi ya lugha mbili katika ujumbe huu.
Wamechanganya ndimi. Lugha ya Kiswahili na Kiingereza imetumiwa.*

Watafitiwa wote walikuwa na maoni sawa na ya huyu mtafitiwa. Kulingana na Wamitila (2003) kuchanganya ndimi ni ile hali ya kuchopeka maneno, kirai, kishazi, au sentensi ya lugha moja ndani ya lugha nyingine. Kwa kurejelea kiwango cha mofolojia (Leech & Short 2007), ni wazi kuwa maneno katika ujumbe huu ni mchanganyiko wa msamiati wa Kiswahili na Kiingereza. Watafitiwa walieleza namna lugha ya Kiswahili imechanganywa na lugha ya Kiingereza katika ujumbe huu jinsi ifuatavyo:

Si – Kiswahili

Hu- Kiswahili

Test-Kiingereza

Regularly- Kiingereza

Kujua - Kiswahili

Status - Kiingereza

Yetu - Kiswahili


Bila - Kiswahili

Worries – Kiingereza

Life - Kiingereza

Inabamba- Kiswahili

B3:Sisi tumeingia kwa network juu tunajua hali yetu ya HIV.



Kuhusiana na bango hili, watafitiwa wote 204 (100%) walieleza kuwa kuna hali ya kuchanganya ndimi. Mtafitiwa mmoja alieleza haya:

Mtafitiwa MW168: *Pia kuna kuchanganya ndimi katika bango hili. Lugha ya Kiingereza imetumika pamoja na lugha ya Kiswahili. Si unaona hapa eh, ‘network’ ina maanisha tandabui na ‘HIV’ ni ukimwi katika lugha ya Kiswahili.*

Watafitiwa walieleza jinsi kuna matumizi ya msamiati wa Kiingereza ‘network’ badala ya „tandabui“ katika lugha ya Kiswahili na ‘HIV’ badala ya ‘virusi vya ukimwi’ katika lugha ya Kiswahili. Neno ‘network’ ni mojawapo ya istilahi za watumizi wa simu za rununu kurejelea uwepo wa mawasiliano. Licha na matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi, makosa ya kisarufi pia yamejitokeza. Kwani msamiati ‘juu’ katika ujumbe huu umetumika visivyo. Katika lugha ya Kiswahili neno mbadala ambalo linastahili kutumika ni ‘kwa sababu.’ Hata hivyo ujumbe huu umewalenga wao kama vijana. Ukiushi wa kimofolojia umejitokeza hapa. Kuna ukiukaji katika kanuni za sarufi tukirejelea namna maneno yalivyotumika katika ujumbe huu. Mathalan, kifungu ‘Si hu-test regularly kujua status yetu’ hakijarejelea kanuni za lugha ya Kiswahili. Kulingana na Leech na Short (2007), katika ukiushi wa kimofolojia maneno huundwa kwa njia isiyo ya kawaida kwa mujibu wa lugha ya Kiswahili. Kwani matini fulani inaweza kujiamulia kanuni zake kando na zile za kawaida. Matini hiyo inaweza kujitenga na ikawa tofauti na namna matini hiyo inavyostahili kuwa.

B8: Chunga usipate red card. Vaa seat belt.



Watafitiwa wote 204 (100%) pia walitambua matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi katika bango hili. Watafitiwa hawa walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW199: *Mimi naona matumizi ya kuchanganya ndimi katika bango hili. Msamiati „red card“ na „seat belt“ ni maneno ya lugha ya Kiswahili.*

Mtafitiwa MW200: *Naam, aliyosema mwenzangu ni kweli kabisa. „Red card“ inamaanisha kadi nyekundu na „seat belt“ inamaanisha mkanda wa usalama.*

Watafitiwa hawa waliweza kueleza jinsi lugha ya Kiswahili pamoja na lugha ya Kiingereza zilivytumika kwenye ujumbe huu ambapo msamiati ‘red card’ na ‘seat belt’ ni msamiati wa Kiingereza unaomaanisha kadi nyekundu na mkanda wa usalama mtawalia. Huu ni ukiushi wa kimofolojia kwa mujibu wa Leech na Short (2007).

B9: *Valia boots usidungwe na mwiba.*



Watafitiwa wote 204 (100%) waliweza kugundua matumizi ya kuchanganya ndimi katika ujumbe huu. Wote walikuwa na maoni sawa na huyu mtafitiwa:

Mtafitiwa MW153: *Naam licha na matumizi ya mafumbo pia kuna matumizi ya kuchanganya ndimi. Nasema hivi kwa sababu ya neno boots, hili ni neno la Kiingereza kumaanisha aina ya viatu.*

B14: *Mwanzo na mwisho wa mawazo G-jue hali yako ya HIV. Tu-meet VCT centre au hosi karibu na mtaa.*



Watafitiwa wote 204 (100%) waliweza kutambua matumizi ya kuchanganya ndimi katika ujumbe kwenye bango hili. Walieleza jinsi lugha ya Kiingereza ilivyotumika pamoja na lugha ya Kiswahili. Watafitiwa hawa waligundua kuwa matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi yamejitokeza katika msamiati ‘Tu-meet.’ Ambapo kiambishi ‘Tu-’ ni kiambishi cha lugha ya Kiswahili kinachorejelea nafsi ya kwanza wingi, neno ‘Meet’ ni neno la lugha ya Kiingereza linalomaanisha kukutana, ‘VCT Centre’ ni msamiati wa Kiingereza unaomaanisha kituo cha ushauri. Mmoja wa watafitiwa hawa alisema haya:

MW157: *Kuna kuchanganya ndimi katika bango hili. Neno Tu-meet limetumia Kiingereza na Kiswahili. Kwani ‘Tu-’ ni Kiswahili na ‘meet’ ni Kiingereza. Inamaanisha kukutana. Pia ‘VCT Centre’ ni neno la Kiingereza.*

Ukiushi katika kiwango cha kimofolojia umedhihirika katika ujumbe kwenye bango hili. Kuna ukiukaji katika maumbo ya baadhi ya maneno kama vile ‘Tu-meet’. Leech na Short (2007), wanaeleza kuwa ukiushi katika kiwango cha kimofolojia huelezea kuhusu maumbo ya maneno yasiyo ya kawaida kwa mujibu wa Lugha ya Kiswahili. Muundo wa msamiati ‘Tu-meet’ si wa kawaida kwa mujibu wa lugha ya Kiswahili. Aidha vile kuna ukiushi katika kiwango cha grafolojia, kuna matumizi ya herufi kubwa yasiyo ya kawaida. Herufi “G” imetumika kwa njia isiyo ya kawaida. Herufi hii imetumika badala ya kiambishi ‘ji’. Leech na Short (2007), wanaeleza kuwa ukiushi katika kiwango cha grafolojia huwa ni matumizi ya mbinu za kimuundo zinazokiuka uandishi wa kawaida kwa lengo la kukifanya kipengele fulani kionekane zaidi ya kingine.

B2: Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.



Watafitiwa wote 204 (100%) walitambua matumizi ya kuchanganya ndimi katika ujumbe huu. Wote walikuwa na maoni sawa na huyu mtafitiwa:

Mtafitiwa MW17: *Naona pia kuna matumizi ya kuchanganya ndimi, kwani lugha ya Kiswahili imetumika pamoja na lugha ya Kiingereza. Neno naked ni neno la Kiingereza linalomaanisha uchi na CD ni akronimu inayotokana na neno la Kiingereza condom.*

Watafitiwa hawa walieleza jinsi lugha ya Kiswahili imetumika pamoja na lugha ya Kiingereza katika kuwasilisha ujumbe huu. Huu ni ukiushi wa kimofolojia, kwani maneno haya yametumika kwa njia ambayo si ya kawaida. Katika matini haya kanuni zilizotumika ni tofauti na zile za kawaida. Kulingana na Leech na Short (2007), ukiushi wa kimofolojia unahusu maswala ya ukiukaji katika jinsi maneno yanavyotumika kwa mujibu wa lugha ya Kiswahili. Kulingana na wao ukiushi hujitokeza kwenye misimbo ya lugha. Sifa hii hujitokeza kama ruwaza za kimaandishi ambapo matini fulani inaweza kujiamulia kanuni zake kando na zile za kawaida. Matini hiyo inaweza kujitenga na ikwa tofauti na namna matini hiyo inavyostahili kuwa.

B15: Mwanaume kamili hujua status yake.



Watafitiwa wote 204 (100%) walitambua matumizi ya kuchanganya ndimi katika bango hili. Mmoja wao alikuwa na haya ya kusema huku wengine wakikubaliana naye.

Mtafitiwa MW165: *Naam kuna matumizi ya kuchanganya ndimi katika bango hili. Kwani kuna matumizi ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiingereza. Neno status ni neno la Kiswahili ambalo linaamanisha hali, HIV ni ukimwi kwa Kiswahili, na Test ni kupimwa.*

Miongoni mwa watafitiwa hawa vijana 59 (29%) walipendelea aina hii ya lugha. Kwani mmoja wao alikuwa na haya ya kusema huku wenzake wakimuunga mkono.

Mtafitiwa MK124: *Mazee, hii si ni lugha poa, saa ngapi kujikaza kaza ati na Kiswahili mufti kila wakati jo. Si bora mtu ameelewa kile anachoambiwa. Huu si mtihani.*

Watafitiwa hawa waliendelea kusema kuwa matumizi ya lugha hii yanawavutia wengi na kuwasababisha kujaribu kusoma mabango. Miongoni mwao kuna mmoja aliyesema haya:

Mtafitiwa MK127: *Ni kweli kabisa aliyosema mwenzangu. Aina hii ya lugha ndiyo inayovuta nadhari yetu na kutusababisha kusoma mabango haya.*

Hali hii ya kuchanganya ndimi ilisaidia vijana 27 (13%) kuelewa ujumbe jinsi ilivyokusudiwa kama alivyodai mmoja wao:

Mtafitiwa MK128: *Matumizi haya ya kuchanganya ndimi ni mazuri sana, kwani inatusaidia sana kuelewa ujumbe kwa haraka sana.*

Hawa watafitiwa walihisi kuwa matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi uliwalenga wao kama vijana na hata kufanya ujumbe huo kuwa wa kuvutia na kueleweka kwa haraka sana. Huu ni ukiushi katika kiwango cha kileksia. Maneno katika ujumbe huu yametumika kwa njia ambayo si ya kawaida. Leech na Short (2007) wanaeleza kuwa ukiushi huu unaweza kuwa na athari chanya au hasi. Katika muktadha huu ukiushi huu umekuwa na athari chanya kwa vile tunaona watafitiwa 59 (29%) wakidai kuwa matumizi ya aina hii ya lugha yanafanya ujumbe kuwa wa kuvutia na kueleweka kwa haraka. Aidha, kulingana na Shitemi (2001), uchanganyaji ndimi sio matumizi ya lugha yanayojitokeza kwa bahati mbaya, bali ni mojawapo ya mitindo ya kimawasiliano yenyе lengo maalumu kutegemea muktadha. Anaendelea kusema kuwa uchanganyaji ndimi hutumiwa ili kuleta maana.

Kwa upande mwingine ukiushi huu umesababisha athari hasi. Kuna watafitiwa 145 (71%) ambao walikuwa na maoni tofauti kabisa kuhusu matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi. Hawa walikuwa na maoni sawa na ya hawa watafitiwa:

Mtafitiwa MW75: *Mitindo hii ya lugha ya kuchanganya na kubadilisha msimbo imeathiri sana lugha sanifu ya Kiswahili kwani lugha hii imechanganywa na lugha ya Kiingereza kwa kiwango kikubwa. Vijana wengi wameiga matumizi haya ya lugha na kuharibu lugha sanifu.*

Mtafitiwa MW134: *Hata mimi namuunga mkono mwenzangu, mara nyingi hali hii ya kuchanganya ndimi husababishwa na sheng, na sheng huchukuliwa kama lugha ya mzaha na kwa hivyo huwafanya watu kutotilia maanani yanayosemwa.*

Watafitiwa hawa walihisi kuwa matumizi ya kuchanganya ndimi yaliathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu kwa njia hasi na kwa kiwango kikubwa sana. Wao walisema kuwa vijana wengi waliiga matumizi haya ya lugha na hivyo kupotosha matumizi ya lugha sanifu ya

Kiswahili. Watafitiwa hawa hawakuunga mkono matumizi ya mbinu hii ya kuchanganya ndimi. Watafitiwa hawa waliendelea kulalamika kuwa matumizi ya aina hii ya lugha kwenye mabango ya ukimwi yameathiri usanifu wa lugha ya Kiswahili mionganoni mwao. Watafitiwa hawa walikuwa wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Maoni ya watafitiwa hawa yanatofautiana na maoni ya Partington (2009) ambaye anasema kuwa lengo kuu la mabango ni kuteua mbinu za lugha ambazo hunasa nadhari ya hadhira lengwa pamoja na kusuluuhisha utata katika matumizi ya lugha. Kinyume ni kuwa mbinu hii ya matumizi ya lugha katika mabango ya ukimwi licha ya kunasa nadhari ya vijana ili waweze kusoma mabango hayo, imezua utata katika matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Kutokana na mtazamo wa watafitiwa hawa ni wazi kuwa matumizi ya lugha isiyo sanifu inaathiri matumizi ya lugha mionganoni mwa baadhi ya vijana. Huenda ndiyo sababu ya baadhi ya vijana kutomudu katika lugha sanifu ya Kiswahili katika vyuo vikuu. Matokeo ya utafiti

huu yanaoana na matokeo ya utafiti wa Hashim (2010) ambapo alitambua kuwa mitindo hii ya kuchanganya ndimi huathiri lugha yoyote husika kwa kiwango kikubwa.

Matumizi ya lugha kwa kawaida huhusisha uteuzi wa maneno au msamiati maalumu katika kiwango cha kileksia (Leech na Short 2007). Kiwango hiki huchunguza maumbo ya maneno. Kiwango hiki pia huhusu kuchanganya ndimi, kuhamisha ndimi na matumizi ya maneno ya kigeni kama Kiingereza au Kilatini. Kutokana na maelezo ya watafitiwa ni wazi kuwa tungo hizi zimechanganya ndimi. Aidha mabango mengi ya matangazo ya ukimwi yamewasilisha maana kwa kuchanganya ndimi. Hata hivyo aina hii ya lugha imetumika ili kuwavutia vijana kusoma mabango ya ukimwi.

4.3.8 Taswira

Taswira kwa mujibu wa Wamitila (2008) ni picha ambazo humjia msomaji akilini anaposoma matini fulani. Anaendelea kusema kuwa picha hizo hujengwa kutokana na maelezo ya mwandishi au tamathali za usemi anazozitumia. Kuna aina mbalimbali za taswira kama vile taswira za uoni, mwonjo, usikivu, mguso, mnuso, joto na mwendo. Mbinu hii ilibainika katika mabango yafuatayo:

B2: *Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.*



Watafitiwa 182 (90%) walidai kuwa ujumbe huu uliwapa wasomaji taswira ya jambo linalorejelewa. Watafitiwa hawa walikuwa na maoni yanayofanana. Baadhi yao walisema yafuatayo:

Mtafitiwa MW20: *Labda kwa kuongeza tu kwa yale wenzangu wamesema, naona pia taswira imejitokeza katika ujumbe huu, I mean ile hali ya kuwa na picha akilini mwako ya mtu akiswim.*

Mtafitiwa MW24: *Kulingana na mimi huyu msanii amelinganisha masuala ya ngono na kuogelea. Anataka mtu akisoma bango hili aweze mwenyewe kujijazia. Huu ujumbe unaonya watu kuhusu ugonjwa wa ukimwi. Na hivyo watumie mpira wa kinga.*

Watafitiwa walieleza kuwa picha ya mtu anayeogelea inajichora akilini mwa mtu anaposoma ujumbe huu. Kwani msanii alilinganisha kitendo cha kuogelea na ngono. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) taswira hutumiwa ili kuunda picha akilini mwa msomaji.

Watafitiwa waliendelea kusema kuwa ujumbe huu unawaonya wasomaji kuhusu ugonjwa wa ukimwi. Kwani wanashauriwa kutumia mpira kama kinga. Kando na haya, makosa mengi ya sarufi yalidhahirika mionganoni mwa baadhi ya watafitiwa jinsi inavyodhahirika katika usemi wa mtafitiwa MW20. Hata hivyo kwa hali ya kawaida mtu huwa haogelei akiwa amevaa nguo jinsi ujumbe huu unavyoelekeza. Hii inaashiria kuwa kuogelea huku si kwa kawaida. Kuvalaa nguo inarejelea hali ya kutumia kinga.

B1: Usilambe asali katika kila nyumba.



Watafitiwa 152 (75%) walikuwa na maoni kuwa ujumbe huu uliwapa wasomaji taswira ya mtu anayesonja asali. Mionganoni mwao kulijitokeza mitazamo ifuatayo:

Mtafitiwa MW59: *Hata kama mnasema kuwa ujumbe huu ni fumbo, mimi pia ninaona matumizi ya taswira yakijitokeza katika ujumbe huu. Kile kitendo cha kulamba asali kinajenga picha safi sana akilini mwangu. Yaani jamaa ambaye ameshindwa kujizuia kulamba asali. Si mnajua asali huwa tamu sana.*

Mtafitiwa MW60: *Kweli kabisa, hapo umegonga ndipo. Taswira imejitokeza wazi wazi kabisa mm! Ile hali ya kuonja onja mpaka asali iishe bana! Hapa wamejaribu kulinganisha kulamba asali na kufanya mapenzi.*

Watafitiwa hawa walisema kuwa asali ilikuwa ni tamu sana na iwapo mtu angedhubutu kuionja haingekuwa rahisi kujizuia kuendelea kuonja. Kulingana na wao ujumbe huu ulijenga taswira katika akili ya binadamu. Watafitiwa hawa walisema kuwa asali ilikuwa ni tamu sana na hivyo kile kitendo cha mtu kulamba asali kiliweza kujenga taswira akilini mwa msomaji. Watafitiwa hawa walielewa fika kuwa ujumbe huu ulilinganisha kitendo cha ‘kulamba asali’ na kitendo cha kufanya mapenzi. Kwani ujumbe uliwaonya wasomaji dhidi ya tabia ya kuwa na uhusiano wa kimpenzi na kila mtu ovyo ovyo. Taswira inayojitekeza hapa ni taswira ya mwonjo, kwani inatupatia dhana ya hisia ya kuonja asali. Wamitila (2008) anaeleza kuwa taswira ya mwonjo hulenga kwenye hisia za kuonja.

4.3.9 Taharuki

Matumizi ya mbinu ya taharuki yalibainshwa na watafitiwa katika mabango yafuatayo:

B11: Mwanangu ngoja kwanza, la sivyo jikinge kila wakati. Fungua roho yako, ongea.



Ujumbe huu ulizua maswali yafuatayo mionganoni mwa watafitiwa jinsi inavyodhihirika kuititia data ifuatayo:

Mtafitiwa M76: *Jameni, huyu mtoto anafaa angoje nini kwanza?*

Mtafitiwa M77: *Mbona kujikinga kila wakati? Lazima pana hatari fulani.*

Mtafitiwa M78: *Mbona mwana huyu hataki kuongea?*

Watafitiwa 165 (80%) walikuwa na mtazamo sawa na ya hawa watafitiwa. Maswali haya yanaashiria matumizi ya mtindo wa taharuki katika ujumbe huu. Ujumbe huu uliwaacha watafitiwa hawa katika hali ya kutaka kujua mzazi anamweleza mwana nini, sababu za kutaka kusubiri, za kujikinga kila wakati na dhidi ya nini. Wamitila (2008), anasema kuwa taharuki ni utumiaji wa mbinu ya msukumo pofu kadhaa na ni hali ya kuvichelewesha visa katika masimulizi fulani. Anaendelea kusema kuwa taharuki hutumiwa kama chombo cha kunata hisia ambapo matokeo hayajulikani. Kutokana na maswali ya watafitiwa ni wazi kwamba taharuki humsukuma msomaji kuwa na hamu ya kutaka kujua zaidi na hivyo hata kumsababisha kutafakari kwa undani kuhusu ujumbe huo.

B7: Ati bila CD Afadhali ikae!



Taharuki vile vile ilijitokeza katika bango hili. Watafitiwa 20 (10%) hawakuelewa ujumbe huu unazungumzia nini. Kwani walikuwa na maoni sawa na huyu mtafitiwa:

Mtafitiwa MK81: *Sielewi wanazungumzia nini. Nini ikae? Ujumbe huu hauko wazi. Ni vizuri bango hili lingetueleza nini ikae. Mimi nahisi kuwa kuna sehemu ya ujumbe ambayo imeachwa nje.*

Kutokana na maoni ya watafitiwa hawa ni wazi kuwa ujumbe huu uliwaacha katika hali fulani ya taharuki, kwani walihisi kuwa kuna ujumbe fulani ambao walitaka kujua sana. Walitaka kujua ni nini walichokuwa wakizungumzia kwenye ujumbe ambao ulikuwa kwenye bango hili.

4.3.10 Matumizi ya Sheng

Watafitiwa walibainisha matumizi ya sheng katika mabango yafuatayo:

B14: Mwanzo na mwisho wa mawazo G-jue hali yako ya HIV. Tu-meet VCT centre au hosi karibu na mtaa.



Watafitiwa wote 204 (100%) waliweza kutambua matumizi ya sheng katika ujumbe kwenye bango hili. Baadhi yao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW73: *Naam haya ni matumizi ya sheng. Kwanza namna lugha ya Kiswahili ilivyotumika pamoja na Kiswahili ni sheng tu. Hebu angalia kiambishi ‘tu’ ni kiambishi cha Kiswahili. Neno ‘hosí’ si Kiswahili wala Kiingereza. Ni sheng.*

Mtafitiwa MW199: *Naam, kwenye ujumbe huu, mimi naona mbinu mpya ya kuunda maneno. Kwani herufi ‘G’ imetumika badala ya kiambishi ‘ji’. Kwa kawaida mbinu ambazo zinajulikana sana katika uundaji wa maneno ni zile za kuongezea viambishi awali na tamati kwenye shina au mzizi wa neno, yaani zile mbinu ambazo zinahusiana na mnyambuliko wa vitenzi. Hii mbinu ambayo imetumika hapa haipatikani katika lugha ya Kiswahili. Katika lugha ya Kiswahili, hili neno linastahili kuwa ‘jijue.’ Haya ni matumizi tu ya sheng.*

Watafitiwa hawa walieleza jinsi lugha ya Kiingereza ilivyotumika pamoja na lugha ya Kiswahili. Hii ni sifa mojawapo ya sheng. Walieleza kuwa kiambishi ‘Tu-’ ni kiambishi cha lugha ya Kiswahili na msamiati ‘hosí’ si neno la Kiswahili wala la lugha ya Kiingereza, bali ni neno lipatikanalo katika kilugha cha sheng. Neno hili lilitumika kumaanisha hospitali. Maumbo ya maneno haya si ya kawaida katika lugha ya Kiswahili. Huu ni ukiushi katika kiwango cha kileksia. Leech na Short (2007), wanaeleza kuwa ukiushi wa kileksia unahu su kuelezea maswala ya ukiukaji katika jinsi maneno yanavyoundwa, maumbo ya maneno yasiyo ya kawaida kwa mujibu wa lugha ya Kiswahili.


Aidha, kwa mujibu wa watafitiwa ‘G-jue’ ni neno ambalo limeundwa kwa mtindo amba si wa kawaida katika lugha ya Kiswahili. Kulingana na wao mtindo huu haupatikani katika lugha ya Kiswahili. Hali hii kulingana na Leech na Short (2007) ni ukiushi katika kiwango cha grafolojia. Ukiushi wa kiwango hiki unahu su kubadilisha matamshi ya maneno, matumizi ya herufi kubwa kwa njia isiyo ya kawaida. Leech na Short (2007) wanasema kuwa matumizi ya vipengele hivi vya kigrafolojia katika maandishi huwa na athari ya uchimuzi. Wanafanua uchimuzi kama dhana yenyé maana ya matumizi ya mbinu za kumuundo zinazokiuka uandishi wa kawaida kwa lengo la kukifanya kipengele fulani kionekane zaidi ya kingine. Katika ujumbe ulio kwenye bango hili, herufi kubwa ‘G’ imetumika kwa njia ambayo si ya kawaida. Katika neno ‘G-jue,’ kulingana na watafitiwa, herufi ‘G’ imetumika badala ya kiambishi ‘ji’, na neno hili katika Kiswahili sanifu lilitahili kuwa ‘jijue.’ Mbinu hii imekiuka uandishi wa kawaida. Huenda lengo ni kupunguza idadi ya maneno, yaani kuandika ujumbe kwa njia ya muhtasari. Kulingana na Dodd (2007) mabango mazuri ni yale ambayo yameandikwa kwa muhtasari na huangazia mambo muhimu pekee. Partington (2009) anasema kuwa uundaji wa maneno kwa njia ya kipekee hunasa nadhari ya hadhira. lugha, kwani mmoja wao alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW134: *Hata mimi namuunga mkono mwenzangu, mara nyingi hali hii ya kuchanganya ndimi husababishwa na sheng, na sheng huchukuliwa kama lugha ya mzaha na kwa hivyo huwafanya watu kutotilia maanani yanayosemwa.*

Kulingana na wao, kilugha cha sheng hutumika kimzaha mionganoni mwa vijana na hivyo matumizi yake katika kuwasilisha ujumbe wa ukimwi yalipunguza uzito wa ujumbe huo na hivyo kuwafanya wao kuchukulia ujumbe huu kimzaha.

Aidha kuna watafitiwa 135 (66%) amba hawakufurahishwa na matumizi ya aina hii ya

B13: Jijue ubambishe life.



Hakuna mtafitiwa hata mmoja aliyetambua matumizi ya sheng katika bango hili. Wote hawakuelewa maana sanifu ya msamiati ‘bamba.’ Wawili hawa walitoa maelezo yafuatayo huku wenzao wakiwa na maoni sawa na yao.

Mtafitiwa MW71: *Ujumbe huu kulingana na mimi unamaanisha kuwa ujijue ufurahie maisha. Yaani ukishajua hali yako utaweza kufurahia maisha.*

Mtafitiwa MW72: *Ni kweli ni rahisi mtu kustarehe na kufanya anasa kama anajua hali yake ya afya. Kwani anaweza kuchukua tahadhari.*

Watafitiwa wote 204 (100%) walielewa fika kuwa neno „bamba“ lilimaanisha kufurahia. Kulingana na Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI 2004), msamiati ‘bamba’ unamaanisha ‘baka.’ **Kulingana na Okoto (2015), sheng hupotosha maana halisi ya maneno katika lugha ya Kiswahili.** Msamiati ‘bamba’ katika muktadha huu umepewa maana mpya ambayo ni ‘furahia.’ Kulingana na mtazamo wa watafitiwa ujumbe huu ulimaanisha kuwa ukijua hali yako ya ukimwi, una uhuru wa kujilingiza katika raha na anasa za maisha ili kufurahia maisha. Kwani kulingana na Charon (2009) binadamu hufasiri ujumbe kulingana na jinsi anavyoolewa.

B6: *Uwanja mdogo, kamdudu kako. Tumia CD.*



Watafitiwa 179 (88%) walitambua matumizi ya sheng katika bango hili. Mtindo huu wa matumizi ya lugha katika usemi huu ‘kamdudu kako’ katika bango hili ulizua mitazamo tofauti mionganoni mwa vijana. Watafitiwa wafuatao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW51: *Je, na kamdudu kako? Hiki ni Kiswahili sanifu kweli?*

Mtafitiwa MW52: *Ah! Wapi! Haya ni makosa ya kisarufi. Sarufi hii imefinyangwa. Ni sheng. Kama ingekuwa Kiswahili sanifu ingekuwa ‘kijidudu kiko’ na wala si ‘kamdudu kako’.*

Kutokana na majadiliano haya tunatambua kuwa watafitiwa hawa waliweza kutambua matumizi ya kufinyanga sarufi katika bango hili. Huu ni ukiushi katika kiwango cha kileksia.

Umbo la msamiati ‘kamdudu’ limekiuka uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili. Umbo hili si la kawaida kwa mujibu wa lugha ya Kiswahili. Kulingana na kanuni za lugha sanifu ya Kiswahili neno hili linastahili kuwa “kijidudu au kidudu”. Leech na Short (2007), wanaeleza kuwa ukiushi katika kiwango cha kileksia unahu maswala ya ukiukaji wa namna maneno yalivoundwa, maumbo ya maneno yasiyo ya kawaida kwa mujibu wa lugha ya Kiswahili, myambuliko usio sahihi mionganoni mwa maswala mengine ya kileksia. Kulingana na wao ukiushi huu hujitokeza kwenye misimbo ya lugha. Watafitiwa walitambua kuwa hiki hakikuwa Kiswahili sanifu kwani ni sheng. Kwa mujibu wa watafitiwa hawa ambaa ni mionganoni mwa vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili, sehemu hii haijazingatia kanuni za sarufi ya lugha ya Kiswahili. Kulingana na wao kiambishi ‘ka’ kimetumika kuonyesha udogo wa mdudu. Kiambishi mbadala katika lugha ya Kiswahili ambacho kinafaa kutumika kuonyesha udogo ni „ki” ambapo neno mdudu katika hali ya udogo ingekuwa ‘kidudu’ hivyo basi sehemu hii ilistahili kuwa ‘kidudu Kiko.’

Kwa kuongezea kuna watafitiwa 117 (57%) ambaa walihisi kuwa matumizi ya aina hii ya lugha yalichangia katika kuzua changamoto katika matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili mionganoni mwao. Mmoja wao alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa Mw195: *Mimi kama mwanaisimu, naona kuwa matumizi ya aina hii ya lugha yanachangia pakubwa katika kuzua changamoto zinazoathiri matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili haswa mionganoni mwa vijana. Vijana wengi hapa chuoni wanaiga matumizi haya ya lugha na hata kuyatumia kwenye maandishi. Na hata sasa hivi tunapoongea sheng imeanza kupewa hadhi ya juu sana kushinda lugha sanifu ya Kiswahili mionganoni mwa vijana.*

Ongechi (2002) na Shitemi (2001), wanasema kuwa ingawa muundo wa lugha ya sheng wa kisarufi ni ule wa Kiswahili, sheng hupuuza sarufi ya Kiswahili katika matumizi yake na hivyo imelaumiwa kwamba inasababisha vijana kutozingatia kanuni za sarufi na tahajia. Hata hivyo ni vyema kuelewa kuwa si lazima mabango yatumie lugha sanifu katika uwasilishaji wa ujumbe kwa vile lengo ni mawasiliano.

4.3.11 Matumizi ya ishara

Watafiti walitambua matumizi ya ishara katika ujumbe ulio kwenye bango hili.

B15: Mwanaume Kamili hujua status yake ya HIV. Chukua test leo.



Watafitiwa wote 204 (100%) walitambua matumizi ya ishara katika bango hili, walikuwa na maoni sawa na ya huyu mtarufi:

Mtarufi MW166: *Naam pia tunaweza kusema kuwa kuna matumizi ya ishara katika bango hili. Herufi „a“ katika neno mwanaume imeashiriwa na ishara ya mchoro inayorejelea uhamasishaji dhidi ya ugonjwa wa ukimwi.*

Mtindo wa matumizi ya ishara si wa kawaida katika lugha ya Kiswahili. Huu ni ukiushi wa kigrafologija. Kiwango hiki kinahusu jinsi maneno yanavyotamkwa na kuandikwa. Ukiushi wa kiwango hiki unahusu kubadilisha matamshi na uendelezaji wa maneno. Leech na Short (2007) wanasema kuwa matumizi ya vipengele hivi vya kigrafologija katika maandishi huwa na athari ya uchimuzi. Wanafafanua uchimuzi kama dhana yenyé maana ya matumizi ya mbinu za kimuundo zinazokiuka uandishi wa kawaida kwa lengo la kukifanya kipengele fulani kionekane zaidi ya kingine. Ogasiji (2007) anasema kuwa kando na matumizi ya maneno, mwandishi anaweza kutumia alama zingine zisizo maneno katika kuiendeleza kazi yake, na kwamba alama hizi zisipuuze kwa vile huwa zimebeba ujumbe fulani na hivyo huwa na athari fulani kwa msomaji wa ujumbe huo. Mathalani katika msamiati “mwanaume” kuna matumizi ya alama ambayo imetumika kurejelea sauti ‘a.’ Aidha, kulingana na Leech na Short (2007) grafologija inahusu utaratibu wa mpangilio wa sauti katika msamiati wa lugha. wanaendelea kusema kuwa kila lugha ina utaratibu wake wa mpangilio wa sauti ambao unatumika kuunda mofimu ambacho ni kipashio kidogo kabisa cha maana katika neno. Ishara aghalabu hutumika kuwasilisha ujumbe mrefu kwa njia ya mkato. Mchoro uliotumika katika ujumbe huu unaashiria uhamasishaji dhidi ya ugonjwa wa ukimwi.

Jedwali la 7: Idadi ya watafitiwa waliotambua matumizi ya mitindo ya lugha kwenye mabango ya ukimwi na idadi ya wale ambao walikosa kutambua matumizi haya ya mitindo ya lugha.

Mitindo ya lugha	Bango	Idadi/asilimia ya Watafitiwa Waliotambua matumizi ya mitindo ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango.	Idadi /asilimia ya watafitiwa waliokosa kutambua matumizi ya mitindo ya lugha Kiswahili kwenye mabango
Istiari	B2 B1	152 (75%) 160 (78%)	52 (25%) 44 (22%)
Mafumbo	B8 B9 B6 B1 B2	152 (75%) 178 (87%) 134 (65%) 160 (78%) 155 (75%)	52 (25%) 26 (13%) 70(35%) 44 (22%) 49 (24%)
Majazi	B9	178 (87%)	26 (13%)
Methali	B10	180 (88%)	24 (12%)
Kinaya	B6	77 (38%)	127 (62%)
Tasfida	B11 B1 B2 B8 B9	112 (55%) 108 (53%) 130 (64%) 128 (63%) 115 (56%)	92 (45%) 96 (47%) 74 (36%) 76 (37%) 89 (44%)
Kuchanganya ndimi	B12 B3 B8 B9 B14 B2 B15	204 (100%) 204 (100%) 204 (100%) 204 (100%) 204 (100%) 204 (100%) 204 (100%)	0 (0%) 0 (0%) 0 (0%) 0 (0%) 0 (0%) 0 (0%) 0 (0%)
Taswira	B2 B1	182 (89%) 152 (75%)	22 (11%) 52 (25%)
Taharuki	B11 B7	165 (80%) 184 (90%)	39 (19%) 20 (10%)
Sheng	B14 B13 B6	204 (100%) 0 (0%) 179 (88%)	0 (100%) 204 (100%) 25 (12%)
Ishara	B15	204 (100%)	0 (100%)
JUMLA	15	4408 (75%)	1473 (25%)

Chanzo: Uchanganuzi wa mtafiti.

4.3.12 Hitimisho

Kwa kurejelea mitazamo ya watafitiwa, sehemu hii ilijikita katika uchanganuzi wa mitindo ya lugha iliyotumika katika mabango ya matangazo ya ukimwi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili. Ili kuchanganua mitindo hii tulizingatia viwango vya semantiki, leksia, na grafolojia (Leech & Short, 2007). Tulishughulikia jinsi ujumbe ulivyokiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kuleta maana mbalimbali. Mitindo ya lugha iliyobainishwa na watafitiwa katika mabango haya ni pamoja na *istiari, mafumbo, majazi, methali, kinaya, tasfida, kuchanganya ndimi, taswira, taharuki, sheng na ishara*.

4.4 Changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhiihika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.

Kutokana na majadiliano ya watafitiwa katika makundi teule, ilibainika wazi kuwa walikumbana na changamoto si haba wakati walipokuwa wanafasiri ujumbe upatikanao kwenye mabango. Changamoto hizi ziliwasababisha kufasiri ujumbe kwa njia mbalimbali zinazohitilafiana. Kila mmoja alifasiri ujumbe kulingana na namna alivyouelewa. Fasiri hizi zilisababisha ujumbe kupata maana tofauti. Aidha, mionganoni mwao kuna wale ambao hawakupendelea kusoma mabango ya Kiswahili kama inavyodhiihika katika data ifuatayo:

Mtafitiwa MK91: *Mbona kutuletea mabango ya Kiswahili. Si ungeleta ya Kiingereza. Kiswahili does not attract to read. Hata ukiuliza hawa wenazangu watakuambia.*

Mtafitiwa MK93: *Sure Kiingereza ni rahisi kusoma na kuelewa. E! Kiswahili ni ngumu sana. Anyway tutacooperate.*

Watafitiwa hawa walichukulia kuwa Kiswahili ni kigumu na hakieleweki kwa haraka. Walikuwa na mtazamo hasi kuhusu lugha ya Kiswahili na hivyo kuathiri jinsi walivyofasiri ujumbe kwenye mabango ya ukimwi. Matokeo haya yanawiana na matokeo ya utafiti wa Mutekwa (2013). Kulingana na utafiti wa Mutekwa (2013) baadhi ya vijana hawakupendelea kusoma mabango ya Kiswahili. Aidha walengwa hao walikosa umakini wa kuchunguza elementi za kisanaa na za kiisimu katika fasiri zao. Baadhi ya changamoto walizokumbana nazo zimejadiliwa katika data ifuatayo.

4.4.1 Mitindo ya lugha


Vipengele vya kimtindo vilivyotumika katika kuwasilisha ujumbe kwenye mabango ya matangazo ya ukimwi vilizua maana anuwai. Mitindo hii ilisababisha kuwepo kwa fasiri mbalimbali. Watafitiwa walitoa fasiri mbalimbali na hivyo kusababisha ujumbe kupata maana tofauti. Baadhi ya watafitiwa walihisi kuwa siyo kila mtu aliweza kutambua mitindo ya lugha iliyotumika katika mabango haya. Mmoja kati ya hawa watafitiwa alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa M30: *Jamani si kila mtu ataweza kuielewa mitindo mbalimbali katika lugha ya Kiswahili, mimi nahisi kuwa kuna wale ambao wataitambua lakini ikija kwa kufasiri watashindwa, sana sana wale ambao si wakufunzi wa lugha Kiswahili.*

Kulingana na hawa watafitiwa kuna wale ambao wangetambua matumizi ya mbalimbali ya lugha ingawa hawangejua namna ya kuifasiri. Namna mitindo ya lugha na ishara za kiisimu zilivyotumika kuusimba ujumbe kwenye mabango ya matangazo ya ukimwi zimeweza kuchangia kusababisha fasiri mbalimbali mionganoni mwa vijana na hata kusababisha changamoto katika kuelewa kwa ujumbe wa mabango haya kwa vijana.

Watafitiwa 160 (80%) walihisi kuwa matumizi ya mitindo mbalimbali ya lugha kwenye mabango haya yalisababisha uwepo wa fasiri mbalimbali. Kutokana na fasiri za watafitiwa hawa, tunatambua kuwa baadhi yao walifasiri ujumbe uliopatikana kwenye mabango hayo visivyo jinsi inavyodhiihika katika data ifuatayo:

B1: *Usilambe asali katika kila nyumba.*



Watafitiwa 45 (22%) hawakutambua matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Wao hawakutambua kuwa ujumbe huu ulikuwa na maana fiche na hivyo kuufasiri jinsi inavyodhihirika katika data ifuatayo:

Mtafitiwa MK101: *Kwangu ujumbe huu unatuonya kuwa tusile chakula kwa nyumba za watu ovyyovyo.*

Mtafitiwa MK108: *Mimi naonelea kuwa ujumbe kwenye hii bango unatuambia kuwa ni vizuri kula chakula kwenye nyumba za watu unaowajua.*

Mtafitiwa MK114: *Kuna hatari katika kula chakula katika kila nyumba, huenda ukapewa sumu.*

Mtafitiwa MK122: *Lakini mimi naona kuwa hii bango inamaanisha kuwa hata kama asali ni tamu namna gani ni vizuri tuweze kujicontrol, tusiwe watu wa kurukiarukia mambo ya watu wengine ovyyovyo.*

Kutokana na majadiliano haya ni wazi kuwa ukosefu wa utambuzi wa matumizi ya mtindo wa mafumbo uliotumika katika kuwasilisha ujumbe umesababisha watafitiwa kukosea katika kufasiri ujumbe. Matumizi ya mtindo huu yamekuwa kikwazo katika uelewaji wa ujumbe na watafitiwa tukilinganisha na muktadha husika. Huenda itabidi lugha ya moja kwa moja kutumika katika uwasilishaji wa aina hii ya ujumbe. Ukiushi wa kisemantiki umedhihirika katika matumizi ya aina hii ya lugha. Maneno katika ujumbe huu yana maana isiyo wazi. Leech na Short (2007), wanaeleza ukiushi wa kisemantiki kuwa na maana ya maana zisizo wazi. Aidha, wanaeleza kuwa ukiushi huu hudhihirisha kuwa neno laweza na maana isiyo ya kawaida ua isiyozoleka. Kwani kulingana na wao maana hutegemea matumizi yake, hategemei namna neno linavyojitokeza kwa kulitazama kijuujuu.

B2: „Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.



Vijana 50 (25%) hawakuelewa maana ya matumizi ya mafumbo katika ujumbe huu. Walisema kuwa ujumbe huu ulikuwa ni mfano wa fumbo ingawa hawakulifumbua. Baadhi yao walisema haya:

Mtafitiwa MK113: *Mbona tu mto Nyando pekee? Kuogelea huku nafeel si kwa kawaida kwa sababu watu wakiogelea ni lazima wavue nguo kwanza. Lazima ujumbe huu una maana fiche. Hili ni fumbo.*

Mtafitiwa MK115: *Hata mimi nahisi kuwa haya ni matumizi ya mafumbo. Ujumbe huu ni fiche, ni lazima mtu afikirie sana au aulize wenzake ili kupata maana iliyokusudiwa na hatuna wakati wa mambo kama haya. Mambo kama haya ndiyo hutufanya kupuzilia mbali kusoma mabango.*

Mtafitiwa MK116: *Mimi nafeel kuwa huenda ujumbe huu unaashiria hatari iliyoko ndani ya mto Nyando na hivyo ujumbe huu unatuonya tutahadhari. Hata mimi nahisi kuwa ujumbe huu ni fumbo. Kwani kuoga huku si kwa kawaida. Ujumbe unaopashwa ni mzito.*

Mtafitiwa MK119: *Naam, nakubaliana na mwenzangu, ndani ya mto huwa tuna wanyama hatari ambao wanaweza kutuvamia na hivyo kuhatarisha maisha yetu. Kwa hivyo ni muhimu kuogelea ukiwa na nguo ili kuwa tayari kutoka hatari ikitokea.*

Mtafitiwa MK120: *Ah! Kila mtu ana nafasi ya kuogelea mtoni. Mbona tu mto Nyando? Labda onyo ni kwa watu wa Nyando.*

Watafitiwa hawa walishangaa kwa sababu kulingana na wao walielewa fika kuwa mtu hastahili kuogelea akiwa amevaa nguo. Kwani kawaida mtu huogelea akiwa uchi. Walichukulia kuwa ujumbe huu uliwatahadharisha kuwa huenda watu wangepatwa na hatari fulani wakiwa majini wakiogelea na hivyo ingekuwa rahisi wao kutoka majini kwa haraka. Vile vile walihisi kuwa ujumbe huu pia uliwatahadharisha kuwa huenda watu wangeona uchi wao kwa vile mto huwa mahali wazi panapoonekana kwa yejote apitaye. Watafitiwa 5 (10%) kati ya hawa asilimia 25% walielewa fika kuwa kuoga huku hakukuwa kwa kawaida, walisema kuwa lazima ujumbe huu ulikuwa na maana nzito ingawa hawakufafanua na kufasiri maana iliyokusudiwa na ujumbe huu.

Watafitiwa hawa walihisi kuwa lugha hiyo ni fiche na hivyo nzito kuelewaka. Kulingana na Bryne (1992) mlengwa huwa na jukumu la kufasiri maana ya inayokusudiwa na tangazo na hivyo tangazo moja linaweza kupata fasiri idadi sawa na ya wapokezi. Mawazo haya ya Bryne yanaoana na matokeo ya utafiti huu kwani watafitiwa hawa walifasiri ujumbe kwa njia mbalimbali kulingana na jinsi walivyoelewa ujumbe huo.

Kwa kawaida kila mtu ana nafasi ya kuogelea mtoni. Swali ni; Mbona tu mto Nyando? Matumizi ya mto Nyando katika bango hili yalisababisha watu wengine kufikiri kuwa onyo ni kwa watu wa Nyando peke yao. Aidha, baadhi ya watu watachukulia ujumbe huu kuwa wa watu wa Nyando pekee na hivyo kukosa kuutilia maanani. Hata hivyo ujumbe katika bango hili unatahadharisha watu wasifanye mapenzi kiholela, yaani bila kujali. Kuogelea mto Nyando uchi inamaanisha kufanya mapenzi bila kinga. Watu wengi hupenda kuogelea mtoni kiholela wakiwa uchi kumaanisha kuwa kuna uwezekano wa watu kujuhusisha kimpenzi kiholela bila kinga yoyote na hivyo kuhatarisha maisha yao.

Kwa upande mwingine kutoptaka na maana msingi maneno huhusishwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi (Leech na Short 2007). Ili kuelewa maana ya ujumbe huu ni lazima watafitiwa wachunguze maana ya ujumbe kulingana na muktadha ambamo ujumbe huu umetumika kwa kujuhusisha na maana msingi. Watafitiwa hawa hawakuweza kujuhusisha ujumbe huu na muktadha ambamo ujumbe huu ulitumika. Kulingana na mtafitiwa MK129, mabango haya hayakupasha ujumbe kwa njia wazi alipogundua kuwa hangelewa maana ya baadhi ya mitindo ya lugha iliyotumika. Alisema kuwa yeche angelipenda kuona mabango ambayo ujumbe wake ni wa moja kwa moja. Kwani alisema haya:

Mtafitiwa MK129: *Nadhani itamchukua mtu mwerevu kuelewa ujumbe huu. Mtu aliye na kiwango cha wastani na chini kiakili hataelewa. Ni ngumu kuelewa ujumbe huu na hivyo sielewi kwa nini wanajisumbua kutumia mitindo hii ya lugha badala ya kutumia lugha iliyo wazi yaani ya moja kwa moja. Kwanza hata mabango haya hayaongezi thamana yoyote kwa vile watu watang "ang" ana kuelewa ujumbe. Mimi kwanza nimeweza tu kuelewa ujumbe huu baada ya kushiriki katika haya majadiliano.*

Kutokana na majadiliano ya makundi teule imebainika wazi kuwa matumizi ya mitindo ya lugha yaliweza kusababisha kutoelewaka kwa ujumbe na uibuaji wa maana zilizotofautiana wakati ambapo msomaji alikosa kutambua matumizi na maana ya mitindo hiyo. Watafitiwa hawa walidai kuwa matumizi ya lugha katika mabango haya yalilenga watu wenye upeo wa juu katika kuielewa lugha ya Kiswahili na wala si watu wa kawaida amba wana upeo wastani wa kuielewa lugha ya Kiswahili. Mathalani mtafitiwa MW33 alisema haya:

Mtafitiwa MW33: *Ujumbe upatikanao kwenye mabango haya ni sawa kwangu, na ninadhani pia ni sawa kwa yeyote yule ambaye amehitimu kiwango sawa na hiki changu cha elimu hasa kwenye somo la Kiswahili, kwa vile wanaweza kuelewa kwa undani ujumbe huu. Mtu mwingine aliye na kiwango cha chini kwenye masomo huenda asiuelewe ujumbe huu vilivyo kwa sababu ya kiwango chake cha masomo.*

Kwa mujibu wa maoni ya mtafitiwa MW33 ni wazi kuwa watu amba wanaelewa ujumbe unaowasilishwa kuitia mabango haya ni wale amba wanatajiriba katika lugha ya Kiswahili.

Hii inamaanisha kuwa haya mawasiliano ya kupitia mabango hayajaweza kufikia kila mtu katika jamii. Ujumbe katika mabango ya ukimwi umefasiriwa kwa njia mbalimbali na hivyo mabango haya hayajatimiza wajibu wayo. Ukiushi wa kisemantiki umedhihirika katika matumizi ya lugha kwenye mabango haya. Maneno katika jumbe kwenye mabango haya yana maana isiyo wazi. Leech na Short (2007), wanaeleza ukiushi wa kisemantiki kuwa na maana ya maana zisizo wazi. Aidha, wanaeleza kuwa ukiushi huu hudhihirisha kuwa neno laweza na maana isiyo ya kawaida ua isiyozoleka. Kwani kulingana na wao maana hutegemea matumizi yake, hategemei namna neno linavyojitokeza kwa kulitazama kijuujuu. Aidha, kulingana na Bankole, Aderinokun na Denloye (2005) mabango lazima yawe wazi ili yawewe kueleweka vema bila usaidizi wowote. Iwapo mabango haya yangelikuwa wazi basi yangelieleweka vema bila usaidizi wowote. Watafitiwa waliposoma mabango walieleza namna ambavyo walifahamu ujumbe. Ujumbe kwenye mabango ulipewa maana mbalimbali kulingana na msomaji binafsi. Hali hii ilisababisha mitazamo tofauti kuhusu matumizi ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi. Ufasiri wa ujumbe ulitegemea lugha iliyotumika katika kuwasilisha ujumbe huo.

4.4.2 Maana ya umaanisho

Changamoto nyininge iliyojitokeza katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana ni kuhusiana na maana ya umaanisho. Maana ya umaanisho ni ile ambayo mtu husema kitu na kumaanisha kingine (Leech na Short (2007). Ukosefu wa kutambua maana ya umaanisho ndiyo iliyojitokeza kama changamoto katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana jinsi ilivyokusudiwa. Ujumbe uliopatikana katika mabango mengi ulisema mambo fulani na kumaanisha mambo mengine. Tazama jedwali lifuatalo.

Jedwali la 8: Maana ya umaanisho ya ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi.

Ujumbe kwenye mabango.	Maana ya umaanisho.
Usiogeleee mto Nyando naked. Vaa CD	Usifanye mapenzi bila kinga. Tumia kondomu. Usifanye mapenzi ovyo ovyo kama watu wengine.
Usilambe asali katika kila nyumba.	Usifanye mapenzi na kila mtu ovyo.
Uwanja mdogo, kamdudu kako. Tumia CD.	Ni watu wachache sana amba hawana virusi vya ukimwi, usifanye mapenzi na kila mtu na pia utumie kondomu.
Chunga usipate red card. Vaa seat belt.	Tahadhari usipate ukimwi, tumia kinga.
Valia boots usidungwe na mwiba.	Tumia kinga usije ukaambukizwa ugonjwa wa ukimwi.

Kuna watafitiwa amba hawakuweza kutambua maana ya umaanisho ya ujumbe uliowasilishwa katika mabango haya na hivyo kuyafasiri vingine kama inavyojitokeza katika data ifuatayo:

B1: *Usilambe asali katika kila nyumba.*



Watafitiwa 45 (22%) hawakutambua maana ya umaanisho ya ujumbe huu. Wao hawakutambua kuwa ujumbe huu ulikuwa na maana fiche na hivyo kuufasiri jinsi inavyodhihirika katika data ifuatayo:

Mtafitiwa MK101: *Kwangu ujumbe huu unatuonya kuwa tusile chakula kwa nyumba za watu ovyyovyo.*

Mtafitiwa MK108: *Mimi naonelea kuwa ujumbe kwenye hii bango unatuambia kuwa ni vizuri kula chakula kwenye nyumba za watu unaowajua.*

Mtafitiwa MK114: *Kuna hatari katika kula chakula katika kila nyumba, huenda ukapewa sumu.*

Mtafitiwa M122: *Lakini mimi naona kuwa hii bango inamaanisha kuwa hata kama asali ni tamu namna gani ni vizuri tuweze kujicontrol, tusiwe watu wa kurukiarukia mambo ya watu wengine ovyyovyo.*

Watafitiwa hawa hawakueleza maana iliyotarajiwa katika ujumbe kwani ujumbe ulisema mambo fulani na kumaanisha mambo mengine. Hawa watafitiwa hawakutambua maana ya umaanisho ya ujumbe huu. Kulingana na wanaisimu Habwe na Karanja (2004) maana ya umaanisho ni maana ya mse maji yaani yule aliyeandika ujumbe husika. Si maana ya kawaida ya lugha fulani. Kwani mse maji husema kitu fulani na kumaanisha kitu tofauti kabisa. Maana hii inafasiriwa tu kulingana na muktadha. Muktadha humfanya msikilizaji au msomaji kuzua umaanisho wa kile ambacho kimeandikwa na mwandishi.

Kutokana na maelezo ya watafitiwa hawa ni wazi kuwa hawakuhusisha muktadha wa ujumbe huu na hivyo kukosa kuelewa ujumbe kulingana na muktadha husika.

Aidha, kulingana na Leech na Short (2007), kwa kurejelea kiwango cha semantiki watafitiwa walihitaji kutambua maana ya msamiati kulingana na muktadha ambamo msamiati huo umetumika. Kulingana na McMahon (1994), maana mpya ya maneno huibuliwa kutegemea miktadha mbalimbali. Hii ina maanisha kuwa maneno ya kawaida yanaweza kutumika katika miktadha mahususi kuzua maana mpya.

B2: „Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.



Vijana 50 (25%) hawakulenga ndipo katika kufafanua ujumbe huu. Baadhi yao walieleza haya:

Mtafitiwa MK113: *Mbona tu mto Nyando pekee? Kuogelea huku nafeel si kwa kawaida kwa sababu watu wakiogelea ni lazima wavue nguo kwanza. Lazima ujumbe huu una maana fiche. Hili ni fumbo.*

Mtafitiwa MK115: *Hata mimi nahisi kuwa haya ni matumizi ya mafumbo. Ujumbe huu ni fiche, ni lazima mtu afikirie sana au aulize wenzake ili kupata maana iliyokusudiwa na hatuna wakati wa mambo kama haya. Mambo kama haya ndiyo hutufanya kupuzilia mbali kusoma mabango.*

Mtafitiwa MK116: *Mimi nafeel kuwa huenda ujumbe huu unaashiria hatari iliyoko ndani ya mto Nyando na hivyo ujumbe huu unatuonya tutahadhari. Hata mimi nahisi kuwa ujumbe huu ni fumbo. Kwani kuoga huku si kwa kawaida. Ujumbe unaopashwa ni mzito.*

Mtafitiwa MK119: *Naam, nakubaliana na mwenzangu, ndani ya mto huwa tuna wanyama hatari ambao wanaweza kutuvamia na hivyo kuhatarisha maisha yetu. Kwa hivyo ni muhimu kuogelea ukiwa na nguo ili kuwa tayari kutoka hatari ikitokea.*

Watafitiwa hawa hawakutambua maana ya umaanisho ya ujumbe huu. Hawakutambua kuwa maana iliyolengwa ilikuwa tofauti kabisa na jinsi ujumbe ulivyokuwa ukisema. Kwani ujumbe huu ulilenga masuala kuhusiana na mapenzi na wala si kuogelea. Watafitiwa hawa walichukulia tu maana ya ujumbe jinsi ulivyokuwa bila kuuhusisha na muktadha husika.

Tunatambua kuwa ni muhimu kuchunguza maana ya ujumbe kulingana na muktadha ambamo ujumbe huo umetumika jinsi wanavyoeleza Leech na Short (2007) kwa kurejelea kiwango cha semantiki, kwa vile kuna ukiushi wa kisemantiki. Maneno katika ujumbe huu yana maana ambayo si ya kawaida na hivyo lazima muktadha uhushishwe. Lawal (1997) anaongezea anaposema kuwa maana za maneno huchunguzwa kutohakana na uhusiano wa maneno katika muundo wa tungo za lugha inayohusika. Anaendelea kusema kuwa maana

huchunguzwa kimuktadha lakini yene kuwa na msingi kuhusiana na maana msingi. Kutohana na maana msingi maneno huhushwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi. Watafitiwa hawa walistahili kuchunguza maana ya ujumbe kutegemea muktadha uliohusika na vile vile kutegemea maana msingi ya maneno yaliyotumika katika kuwasilisha ujumbe ili kuweza kupata maana faafu ya ujumbe huo.

B5: *Bila kondomu=Hakuna mapenzi*



Watafitiwa 50 (25%) hawakutambua maana ya umaanisho ya ujumbe huu. Baadhi yao walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MK82: *Huu ujumbe hausemi ukweli. Hupendi mtu kwa sababu ana kondmu.*

Mtafitiwa MK107: *Kondomu si mapenzi. Mapenzi ni kama kikohozi.*

Mtafitiwa MK109: *Na hisi kuwa ujumbe huu unamaanisha kuwa lazima pawe na kondomu ndiposa pawe na mapenzi. Huu ujumbe hausemi ukweli.*

Watafitiwa hawa walichukulia ujumbe huu kumaanisha kuwa kondomu ndiyo huleta mapenzi kati ya watu. Kulingana nao ujumbe huu ulimaanisha kuwa unampenda mtu kwa sababu ana kondomu kinyume na mawazo yao.

B6: *Uwanja mdogo, kamdudu kako. Tumia CD.*



Kuhusu bango hili, watafitiwa walikuwa na mitazamo mbalimbali kuhusu ujumbe wake. Baadhi ya watafitiwa walitoa maoni yafuatayo:

Mtafitiwa MK102: *Uwanja ukiwa mdogo itakuwa ni vigumu watu kuutumia. Na kwanza wanasema kamdudu kako, si basi uwanja huu ni mbaya kwa binadamu kuchezea.*

Mtafitiwa MK103: *Hata kama uwanja ni mdogo, si unaweza kutafuta uwanja mwingine mkubwa?*

Mtafitiwa MK112: *Kamdudu ni kitu kidogo sana ambacho chaweza kuangamizwa na mtu yeyote.*

Mtafitiwa MK117: *Ujumbe huu haueleweki waziwazi kwani uwanja, kamdudu na CD vina uhusiano upi?*

Mtafitiwa MK121: *Kwa nini hawa watu wanafanya Kiswahili kuwa ngumu? Wanafanya hata nisipende kusoma mambo kwa Kiswahili. Wanafanya lugha ya Kiswahili kuwa ngumu hata huwezi kuelewa kitu haraka.*

Mtafitiwa MK125: *Ni CD ipi inayozungumziwa?*

Jumla ya watafitiwa 70 (35%) vile vile hawakuweza kutambua maana ya umaanisho ya ujumbe kutegemea muktadha husika. Watafitiwa hawa hawakuchunguza maana kutegemea muktadha. Kwa kurejelea kiwango cha semantiki maana ya maneno huchunguzwa kulingana na muktadha ambamo maneno hayo yametumika kwani huwa kuna ukiushi wa kisemantiki. Kulingana na Leech na Short (2007), kiushi wa kisemantiki ni ile hali ambapo maneno huwa na maana isiyo ya kawaida. Aghalabu maana huwa fiche, na ili kubaini maana lengwa ni sharti muktadha husika uhushishwe. Baadhi ya watafitiwa walihisi kuwa itakuwa vigumu uwanja huo kutumika kwa vile ulikuwa mdogo na pia ulikwa umevamiwa na wadudu. Wengine walisema kuwa hata kama uwanja ni mdogo una uhuru wa kutafuta uwanja mwingine mkubwa. Vile vile kulingana na wao mdudu ni kiumbe mdogo sana ambaye anaweza kuangamizwa na mtu yeyote na hivyo kwa nini kumsumbuu binadamu. Kulingana na wao ujumbe huo haukueleweka waziwazi kwa sababu hakuna uhusiano wowote kati ya uwanja, kamdudu na CD. Watafitiwa hawa walihitajika kuhusisha ujumbe huu na muktadha husika.

B8: *Chunga usipate red card. Vaa seatbelt.*



Kuhusiana na ujumbe wa bango hili watafitiwa vile vile hawakutambua maana ya umaanisho ya ujumbe huu. Kwani walikuwa na mitazamo tofauti kuhusu ujumbe huu. Miongoni mwa fasiri zilizotolewa ni kama zifuatazo:

Mtafitiwa MK84: *Seatbelt huvaliwa wakati unaposafiri ili kuzuia ajali.*

Mtafitiwa MK86: *Ni vyema kuvaliwa seatbelt ili kujikinga na hatari.*

Mtafitiwa MW1: *Kulingana nami, kwa mujibu wa muktadha ambamo bango hili linatumika ujumbe huu unamaana nyingine. Kuna maana ya ndani ambayo haijitokezi wazi wazi. Seatbelt na red card inayorejelewa hapa si ya kawaida. Ni lazima mtu ajue muktadha unaorejelewa ndipo apate kuelewa ujumbe huu kwa sababu una wingi wa maana.*

Watafitiwa 50 (25%) hawakulenga ndipo katika ufasiri wa ujumbe huu. Wao walichukulia mkanda wa kujifunga kuwa mkanda wa kawaida waujuao ambao unapatikana kwenye gari. Walieleza kuwa ni vyema kujifunga mkanda unaposafiri ili kuzuia ajali na hatari nyinginez. Walidai kuwa maana ya ndani ya ujumbe huu haikujitokeza wazi wazi. Kwa upande mwingine watafitiwa 152 (75%) waliweza kukisia maana ya ujumbe huu kutokana na mada ya utafiti. Walisema kuwa ujumbe huu ulikuwa na wingi wa maana kutegemea muktadha.

4.4.3 Kutosoma sehemu zote za ujumbe au mabango

Hali ya kutosoma sehemu zote za ujumbe pia ilichangia pakubwa katika kusababisha watafitiwa kukosa kuelewa ujumbe katika mabango haya. Namna watafitiwa walivyofasiri ujumbe kwenye mabango inaonyesha kuwa walilenga sehemu fulani za ujumbe, kuashiria kuwa walichagua sehemu ambazo walitaka kusoma huku wakipuza kusoma sehemu zingine za ujumbe uo huo. Mtazamo huu ulisababisha baadhi ya watafitiwa kufasiri ujumbe kwa namna tofauti kwa sababu hawakusoma ujumbe wote mzima. Baadhi ya watafitiwa walidai kuwa aghalabu hawakuwa na wakati wa kusoma mabango, madai ambayo yanaoana na maoni ya Robin (2009). Kulingana na Robin (2009) ni nadra sana kwa watu kutumia zaidi ya dakika tano kusoma mabango, kwani aghalabu watu huchukua tu dakika moja kuyasoma mabango iwapo watasimama kuyasoma. Watu wengi hawana muda wa kusoma mabango. Dondoo zifuatazo zinaashiria kuwa watafitiwa walizingatia kusoma sehemu fulani za ujumbe kwenye mabango husika. Jumla ya watafitiwa 50 (25%) walisoma na kuzingatia tu sehemu ya kwanza ya ujumbe. Hawakusema chochote kuhusiana na sehemu ya pili ya ujumbe jinsi inavyodhihirika katika data ifuatayo:

B2: *Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.*



Mtafitiwa MK111: *Maana inayotokana na ujumbe huu ni kuwa ukiogelea mto Nyando hakikisha umeava mavazi kwa sababu watu huenda wakaona uchi wako.*

Mtafitiwa MK113: *Mbona tu mto Nyando pekee? Kuogelea huku nafeel si kwa kawaida kwa sababu watu wakiogelea ni lazima wavue nguo kwanza. Lazima ujumbe huu una maana fiche. Hili ni fumbo.*

Mtafitiwa MK115: *Hata mimi nahisi kuwa haya ni matumizi ya mafumbo. Ujumbe huu ni fiche, ni lazima mtu afikirie sana au aulize wenzake ili kupata maana iliyokusudiwa na hatuna wakati wa mambo kama haya. Mambo kama haya ndiyo hutufanya kupuzilia mbali kusoma mabango.*

Mtafitiwa MK116: *Mimi nafeel kuwa huenda ujumbe huu unaashiria hatari iliyoko ndani ya mto Nyando na hivyo ujumbe huu unatuonya tutahadhari. Hata mimi nahisi kuwa ujumbe huu ni fumbo. Kwani kuoga huku si kwa kawaida. Ujumbe unaopashwa ni mzito.*

Mtafitiwa MK119: *Naam, nakubaliana na mwenzangu, ndani ya mto huwa tuna wanyama hatari amba wanaweza kutuvamia na hivyo kuhatarisha maisha yetu. Kwa hivyo ni muhimu kuogelea ukiwa na nguo ili kuwa tayari kutoka hatari ikitokea.*

Kutokana na maelezo ya watafitiwa hawa ni wazi kuwa hawakusoma ujumbe mzima kwenye bango hili. Walizingatia kusoma sehemu ya kwanza pekee ambayo ni: „Usiogelee mto Nyando naked.“ Sehemu ya pili ambayo ni: „Vaa CD“ hawakuisoma.

4.4.4 Kudharau na kupuuza lugha ya Kiswahili

Kudharau na kupuuza lugha ya Kiswahili kulisababisha hali ya kukosa kuelewa kwa ujumbe wa mabango ya matangazo ya ukimwi na wanafunzi. Kulingana na taasisi ya BAKITA (2004) kumekuwa na kudharau lugha ya Kiswahili nchini Tanzania na nchini Kenya kutokana na utandawazi, ambapo lugha hii inaonekana kuwa lugha duni ya watu wa tabaka la wasionacho. Baadhi ya watafitiwa hawakupendelea kusoma mabango ya Kiswahili haswa wale amba hawasomei kozi ya Kiswahili. Wao walihisi kuwa Kiswahili ni kigumu na hakieleweki kwa haraka. Kukosa kwao kuelewa ujumbe kwenye mabango haya kulitokana na mtazamo hasi waliokuwa nao kuhusu lugha ya Kiswahili. Walikosa umakini wa kuchunguza namna ambavyo ishara za kiisimu zilitumika kuusimba ujumbe kwenye mabango na hivyo kusababisha wao kukosa kuelewa ujumbe. Baadhi yao walisema yafuatayo:

Mtafitiwa MK91: *Mbona kutuletea mabango ya Kiswahili. Si ungeleta ya Kiingereza. Kiswahili does not attract to read. Hata ukiuliza hawa wenzangu watakuambia.*

Mtafitiwa MK93: *Sure Kiingereza ni rahisi kusoma na kuelewa. E! Kiswahili ni ngumu sana. Anyway tutacooperate.*

Mmoja wao alikuwa na haya ya kusema kuhusu bango la B6: *Uwanja mdogo, Kamdudu kako. Tumia CD*

Mtafitiwa MK121: *Kwa nini hawa watu wanafanya Kiswahili kuwa ngumu? Wanafanya hata nisipende kusoma mambo kwa Kiswahili. Wanafanya lugha ya Kiswahili kuwa ngumu hata huwezi kuelewa kitu haraka.*

Kulingana na utafiti wa Mutekwa (2013) vijana japo wameelimika hawapendelei kusoma mabango ya Kiswahili. Anasema kuwa mionganini mwao kuna wale walio na mtazamo hasi na wanachukulia kuwa Kiswahili ni kigumu na hakieleweki haraka. Katika utafiti huu mtazamo hasi uliathiri namna walivyofasiri mabango ya Kiswahili kwani walikosa umakini wa kuchunguza elementi za kiisimu katika ujumbe na hivyo kukosa kuelewa ujumbe jinsi ilivyokusudiwa. Matokeo ya utafiti huu yameoana na matokeo ya utafiti wa Mutekwa kwani baadhi ya watafitiwa walihisi kuwa Kiswahili ni kigumu sana kueleweka na hali hii inatokana na ule mtazamo hasi walio nao kuhusu lugha ya Kiswahili.

4.4.5 Uhitaji wa ufhamu wa ujumbe wa awali

Kutokana na majadilano ya watafitiwa ilibainika wazi kuwa baadhi ya mabango yalihitaji ufhamu wa ujumbe wa awali kama vile

B11: *Mwanangu ngoja kwanza, la sivyo jikinge kila wakati. Fungua roho yako. Ongea.*



Kulingana na watafitiwa kuna ujumbe ambao umeachwa nje kwenye bango hili. Watafitiwa hawa walikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW34: *Hatuelezwi mtoto anastahili kungoja nini au kujikinga dhidiya nini.*

Mtafitiwa MW38: *Jameni, huyu mtoto anafaa angoje nini kwanza?*

Kulingana na watafitiwa hawa jambo linalozungumziwa katika ujumbe huu halijatajwa. Mtu anahitaji kuwa na ujumbe wa awali ndiposa aweze kuelewa jambo linalozungumziwa. Iwapo jambo linalozungumziwa halijatajwa basi itakuwa changamoto kufasiri ujumbe vilivyo na yeoyote anayesoma ujumbe huo.

B7 : *Ati bila CD Afadhali ikae!*



Kuhusiana na bango hili watafitiwa walihisi kuwa kuna ujumbe ambao ulikuwa umeachwa nje. Hawakuelewa ujumbe huu ulikuwa unazungumzia nini. Haya yanajidhihirisha kutohana na majadiliano yao. Mmoja wa watafitiwa alisema haya:

Mtafitiwa MK81: *Sielewi wanazungumzia nini. Nini ikae? Ujumbe huu hauko wazi. Ni vizuri bango hili lingetueleza nini ikae. Mimi nahisi kuwa kuna sehemu ya ujumbe ambayo imeachwa nje.*

Kutohana na majadiliano ya wahusika hawa ni wazi kuwa kuna mabango ambayo hayakuwaslisha ujumbe vikamilifu. Dhana ya uchukulio ilijitokeza hapa. Habwe na Karanja (2004) wanaeleza dhana ya uchukulio kuwa mtazamo wa maana ambapo msomaji au mwandishi huwa anachukulia kuwa msikilizaji au msomaji anajua mambo yanayojadiliwa. Kutohana na maelezo haya ni wazi kuwa aliyeanda mabango haya alichukulia kuwa walengwa walikuwa wanajua mambo aliyokuwa akiyashughulikia. Kwa upande mwingine tunatambua kuwa walengwa hawakuwa na ufahamu wa awali kuhusu mambo yaliyokuwa yakishughulikiwa hali ambayo ilichangia wao kutoweza kuelewa ujumbe. Ili ujumbe uweze kueleweka vyema ni vizuri uwasilishwe vikamilifu. Mwandishi asichukulie tu kuwa msomaji atawea kujua mambo anayoyajadili. Pasiwe na dhana ya uchukulio katika masuala nyeti katika jamii.

4.4.6 Masuala ya utamaduni

Masuala ya utamaduni vile vile yalichangia katika kusababisha vijana kukosa kuelewa ujumbe katika mabango husika jinsi ilivyo kusudiwa. Kulingana na Maweja (2002) katika tamaduni nyingi za Afrika kuna miiko ya kiisimu ambapo maneno na misemo fulani hairuhusiwi kutajwa hadharani, na iwapo itatajwa itakuwa ni kuwakosea wanajamii heshima. Hivyo basi ili mja kusema alilokusudia anatakiwa kutumia mbinu faafu ya kistaha.

Maweja (2002) anaendelea kusema kuwa masuala yanayohusiana na ngono katika jamii nyingi za Kiafrika ni mwiko kuyataja. Mawazo haya ya Maweja (2002) yameoana na baadhi ya mitazamo ya watafitiwa. Kwani mmoja wao alikuwa na haya ya kusema:

Mtafitiwa MW36: *Unajua nini, kama ni mambo na ngono na ukimwi, watu wengi hawapendi kuzungumzia vitu hivi mbele ya watu. Si unaona? Ujumbe huu unarejelea mzazi na mtoto wake na ni kama mzazi anaona aibu kumwambia mambo fulani kwa kuyataja wazi wazi.*

Kwa sababu ya masuala haya ya utamaduni, lugha fiche imetumika katika kuashiria masuala ya ngono kuwasilisha ujumbe katika mabango mengi ya matangazo ya ukimwi na hivyo kusababisha changamoto katika kuelewa ujumbe na hadhira lengwa. Mambo yanayohusiana na ngono ndiyo yanayosababisha usambazaji wa ugonjwa wa ukimwi mionganoni mwa vijana. Mambo haya yanastahili kuwekwa wazi ili kila mtu aelewewe na hivyo kuchukua au kuweka mikakati inayofaa katika maisha yao.

4.4.7 Wingi wa maana

Wingi wa maana huashiria ile hali ambapo ujumbe kwenye bango huzua zaidi ya maana moja. Hali hii hujulikana kama polisemia. Habwe na Karanja (2004) wanaeleza polisemia kuwa hali ambapo maneno huwa na maana zaidi ya moja. Yaani kuna umbo moja la neno lenye maana mbalimbali. Katika utafiti huu tulitambua kuwa kuna mabango ambayo

yalikuwa na ujumbe ambao ulizua zaidi ya maana moja kwa kurejelea fasiri za watafitiwa. Wingi wa maana ulijitokeza katika mabaungo yafuatayo:

B8: *Chunga usipate red card. Vaa seat belt.*



Bango hili liliwasilisha maana zaidi ya moja. Miogoni mwa watafitiwa kulijitokeza fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MK90: *Naam, red card pia hutumiwa katika hali ya kucheza mpira sana sana wakati ambapo mchezaji huwa amevunja masharti ya mchezo. Nadhani ujumbe huu pia unaonya wachezaji wawe waangalifu.*

Mtafitiwa M86: *Ni vyema kuvalaa seat belt ili kujikinga na hatari.*

Mtafitiwa M87: *Ni kweli aliyosema mwenzangu ni vizuri kuvalaa seat belt ili kujikinga na hatari. Hatari hii inaweza kuwa ni kifo. Red card hapa lazima iwe inamaanisha kifo.*

Mtafitiwa MW1: *Kulingana nami, kwa mujibu wa muktadha ambamo bango hili linatumika ujumbe huu una maana nyingine. Kuna maana ya ndani ambayo haijitokezi wazi wazi. Seatbelt na red card inayorejelewa hapa si ya kawaada. Ni lazima mtu ajue muktadha unaorejelewa ndipo apate kuelewa ujumbe huu kwa sababu una wingi wa maana.*

Data hii inadhibitisha jinsi bango hili lina wingi wa maana. Kutokana na fasiri zilizotolewa na watafitiwa tulitambua kuwa „red card“ iliashiria dhana tofauti ambazo ni: onyo, hatari, ajali na kifo. Mtafitiwa MK1 ailitambua dhana hii ya wingi wa maana. Hali ya wingi wa maana ni changamoto ambayo ilisababisha watafitiwa kufasiri ujumbe kwa njia tofauti. Hali hii inapojitokeza huwa ni ngumu kuabainisha maana iliyotarajiwa ya ujumbe husika. Watafitiwa hawa walifasiri huu ujumbe jinsi walivouelewa. Kila mmoja wao aliridhika kuwa alikuwa sawa.

B2: „Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.



Wingi wa maana ulisababisha watafitiwa 50 (25%) kufasiri ujumbe huu kwa njia tofauti. Baadhi yao walitoa fasiri zifuatazo huku wenzao wakikubaliana nao.

Mtafitiwa MK10: *Maana inayotokana na ujumbe huu ni kuwa ukiogelea mto Nyando hakikisha umeava mavazi kwa sababu watu huenda wakaona uchi wako.*

Mtafitiwa MK116: *Mimi nafeel kuwa huenda ujumbe huu unaashiria hatari iliyoko ndani ya mto Nyando na hivyo ujumbe huu unatuonya tutahadhari. Hata mimi nahisi kuwa ujumbe huu ni fumbo. Kwani kuoga huku si kwa kawaida. Ujumbe unaopashwa ni mzito.*

Mtafitiwa MK119: *Naam, nakubaliana na mwenzangu, ndani ya mto huwa tuna wanyama hatari ambao wanaweza kutuvamia na hivyo kuhatarisha maisha yetu. Kwa hivyo ni muhimu kuogelea ukiwa na nguo ili kuwa tayari kutoka hatari ikitokea.*

Ujumbe huu unaashiria zaidi ya maana moja. Kuna maana ya juu na maana ya ndani. Watafitiwa hawa wajikita katika maana ya juu. Kwani wao walichukulia kuwa ujumbe huu uliwatahadharisha kuwa huenda watu wangepatwa na hatari fulani wakiogelea na hivyo ingekuwa rahisi wao kutoka majini kwa haraka. Vile vile walihisi kuwa ujumbe huu pia uliwatahadharisha kuwa huenda watu wangeona uchi wao kwa vile mto huwa mahali wazi panapoonekana kwa yejote apitaye. Kutokana na majadiliano ya watafitiwa hawa tunatambua kuwa walirejelea maana msingi ya ujumbe huu ambayo ni maana ya juu badala ya kurejelea maana ya ndani ambayo hujitokeza kwa kurejelea muktadha husika. Leech na

Short (2007) wanaeleza kuwa kutokana na maana msingi maneno huhusishwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi. Watafitiwa walihitaji kutambua maana ya msamiati kulingana na muktadha ambamo msamiati huo umetumika na wala siyo kutegemea maana msingi. Maana, kwa mujibu wa Leech na Short (2007), hutegemea matumizi yake na wala si namna neno linavyojitokeza kwa kulitazama kijuujuu. Kulingana McMahon (1994), maana mpya ya maneno huibuliwa katika miktadha mbalimbali ya lugha. Hali hii ilisababisha utata katika kufasiri ujumbe na watafitiwa.

B9: *Valia boots usidungwe na mwiba.*



Ujumbe kwenye bango hili ulizua maana zaidi ya moja. Vile vile kulikuwa na maana ya juu na maana ya ndani. Kuna watafitiwa 26 (13%) ambao hawakutambua maana ya ndani ya msamiati „boots.“ Miiongoni mwao kulijitokeza fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MK99: *Kwangu mimi ujumbe huu unatueleza kuwa wakati tunapotembea katika sehemu zilizo na miiba ni vyema kuvali viatu aina ya boots kwa sababu viatu hivi ni vya nguvu, miiba haiwezi ikapita ndani.*

Mtafitiwa MK100: *By the way that's true. Hata katika somo la Kilimo huwa tunafunzwa tuvae boots tunapolima ama tunapofyeka hasa sehemu zilizo na miiba especially kayapo.*

Watafitiwa hawa walichukulia msamiati ‘boot’ kumaanisha ‘boot’ ya kawaida. Kutokana na majadiliano haya ni wazi kuwa hawa watafitiwa walirejelea maana ya juu ya ujumbe huu na wala si maana ya ndani. Maana ya ndani ndiyo iliyotarajiwa katika ujumbe huu. Kwa sababu ya wingi wa maana watafitiwa hawakulenga maana tarajiwa.

B1: Usilambe asali katika kila nyumba.



Watafitiwa 35 (17%) hawangeweza kufafanua ujumbe huu jinsi ilivytarajiwa kwa sababu ya wingi wa maana. Ujumbe huu ulizua zaidi ya maana moja mionganini mwa watafitiwa. Baadhi yao waliweza kutoa fasiri zifuatazo:

Mtafitiwa MK101: *Kwangu ujumbe huu unatuonya kuwa tusile chakula kwa nyumba za watu ovoyovo.*

Mtafitiwa MK108: *Mimi naonelea kuwa ujumbe kwenye hii bango unatuambia kuwa ni vizuri kula chakula kwenye nyumba za watu unaowajua.*

Mtafitiwa MK114: *Kuna hatari katika kula chakula katika kila nyumba, huenda ukapewa sumu.*

Mtafitiwa MK122: *Lakini mimi naona kuwa hii bango inamaanisha kuwa hata kama asali ni tamu namna gani ni vizuri tuweze kujicontrol, tusiwe watu wa kurukiarukia mambo ya watu wengine ovyoovyo.*

Idadi hii ilijumuisha wanafunzi ambao ni wakufunzi rika. Wakufunzi rika walioshirikishwa katika utafiti huu hawakuwa wanasomea kozi ya Kiswahili. Wao walichukulia msamiati ‘asali’ kuwa chakula cha kawaida.

Kutokana na majadiliano haya ni wazi kuwa kwa sababu ya kuwepo kwa zaidi ya maana moja ya ujumbe huu, watafitiwa walifasiri ujumbe huu kwa njia mbalimbali. Fasiri hizi

hazikulenga maana tarajiwa ya ujumbe huu. Kwani wao walijikita kwenye maana ya juu na si maana ya ndani ambayo ilikuwa maana tarajiwa.

Kwa kurejelea majadiliano ya watafitiwa hawa ni wazi kuwa pasingekuwepo na ile hali ya wingi wa maana, yaani ujumbe kwenye mabango uwe wa moja kwa moja basi watafitiwa wangerejelea tu hiyo maana. Hii ni kwa sababu hakuna maana nyingine ambayo wangerejelea. Aidha, matumizi ya mitindo ya lugha kwenye jumbe hizi yalizua changamoto zilizodhihirika wazi katika kuelewa jumbe hizi na baadhi ya watafitiwa. Changamoto zilizodhihirika si haba, kwani zilikuwa: msuala ya utamaduni, kutotambua maana ya umaanisho, kutosoma sehemu zote za ujumbe, kudharau lugha ya Kiswahili na uwepo wa wingi wa maana.

4.5 Hitimisho

Sehemu hii imeshughulikia matokeo ya madhumuni yote matatu. Kwani imepambanua fasiri zilizotolewa na vijana kuhusu ujumbe unaowasilishwa na mabango ya ukimwi yaliyoandikwa katika lugha ya Kiswahili, pamoja na kuchanganua mitazamo ya vijana kuhusu mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango haya na kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhihirika katika kuelewa kwa ujumbe.

Kuhusiana na madhumuni ya kwanza watafitiwa walifasiri ujumbe jinsi walivyoulewa. Watafitiwa walitoa fasiri mbalimbali kuhusiana na ujumbe mmoja. Kutokana na fasiri zao tulitambua kuwa watafitiwa 45 (22%) hawakuweza kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Asilimia hii ya 22% ilijumuisha wanafunzi amba ni wakufunzi rika na amba hawasomei kozi ya Kiswahili. Fasiri mbalimbali zimeweza kusababisha ujumbe kupata maana tofauti zinazohitilafiana. Hali hii kwa kiwango fulani imesababisha ujumbe kukosa kueleweka jinsi ilivyotarajiwa jambo ambalo huenda linasababisha jukumu la ujumbe huu kutotimilika. Ni sharti vijana waweze kufahamu ujumbe unaopatikana katika mabango ya matangazo ya ukimwi ndiposa waweze kufasiri ujumbe huo jinsi ilivyokusudiwa. Lugha itumikayo sharti iwe inaeleweka mionganoni mwa vijana.

Aidha kuhusiana na madhumuni ya pili mitindo mbalimbali ya lugha ilidhihirika katika mabango haya. Mitindo hii ni pamoja na stiari, methali, tasfida, majazi, sheng, kinaya, taswira, tahiruki, kuchanganya ndimi, matumizi ya ishara na mafumbo. Matumizi ya mitindo ya lugha kwenye mabango haya yalichangia katika uibuaji wa fasiri mbalimbali mionganoni mwa watafitiwa. Kuna baadhi ya watafitiwa amba walitatzika kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa kwa sababu ya kutoelewa maana ya mitindo ya lugha iliyotumika. Hii inamaanisha kuwa matumizi ya mitindo ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango ya ukimwi yamesababisha mabango haya kwa kiwango fulani kutowasilisha ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Aidha, baadhi ya mitindo ya lugha kama vile kuchanganya ndimi na sheng imeathiri matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili mionganoni mwa wanafunzi. Ilibainika wazi pia kuwa kuna mitindo iliyotumika ambayo iliwasilisha maana tofauti na maana msingi. Leech na Short (2007) wanaeleza kuwa kutokana na maana msingi maneno huhusishwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi. Watafitiwa walihitaji kutambua maana ya msamiati kulingana na muktadha ambamo msamiati huo umetumika na wala siyo kutegemea maana msingi. Leech na Short (2007), wanaendelea kusema kuwa

maana hutegemea jinsi lugha ilivyotumika katika muktadha husika. Sababu ikiwa katika ukiushi wa kisemantiki maneno hupewa maana tofauti na maana ya kawaida, hivyo lazima maana ichunguzwe kwa undani na wala si kijuujuu. Kulingana McMahon (1994), maana mpya ya maneno huibuliwa kutegemea miktadha mbalimbali. Hii ina maanisha kuwa maneno ya kawaida yanaweza kutumika katika miktadha mahususi kuzua maana mpya. Hata hivyo, kwa upande mwagine mitindo ya lugha iliyotumika iliweza kusababisha msomaji kuwa na uwezo wa kutafakari kuhusu ujumbe uliowasilishwa kwenye mabango yenyе ujumbe wa ukimwi.

Kutokana na majadiliano ya makundi teule imebainika wazi kuwa mitindo ya lugha iliyotumika ilizua changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango hayo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Changamoto zilizodhihirika ni pamoja na kutotambua maana ya umaanisho, masuala ya utamaduni, kudharau lugha ya Kiswahili, wingi wa maana, kutosoma sehemu zote za ujumbe na uhitaji wa ufahamu wa ujumbe wa awali. Changamoto hizi zilisababisha baadhi ya watafitiwa kufasiri ujumbe kwa namna tofauti na maana tarajiwaa.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kutoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo kwa misingi ya matokeo ya utafiti huu. Utafiti huu ulifanywa katika chuo kikuu cha Maseno na chuo kikuu cha Masinde Muliro cha Sayansi na Teknolojia. Kusudi la utafiti huu lilikuwa ni kuchanganua kiuhakikifu mtazamo wa wanafunzi wa vyuo vikuu kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi. Mabango yametumika kama njia mojawapo ya kuwahamasisha vijana katika vyuo vikuu nchini Kenya kuhusu ugonjwa wa ukimwi. Licha ya haya, ugonjwa huu umeendelea kuwa changamoto kubwa katika vyuo hivi. Jambo hili lilizua haja ya kuchunguza na kuweka wazi mitazamo ya vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango haya.

5.2 Muhtasari wa matokeo ya utafiti

5.2.1 Fasiri za vijana kuhusu ujumbe upatikanao kwenye mabango ya ukimwi

Watafitiwa waliposoma mabango waliweza kufikiria na kuwaza kuhusu ujumbe huo na kisha kueleza mawazo yao kuhusu jinsi walivyoolewa ujumbe kwa kutumia lugha. Vijana hawa walifasiri ujumbe kwa njia mbalimbali zinazohitilafiana. Kila mmoja alifasiri kulingana na namna alivyoolewa. Fasiri hizi zilifanya ujumbe kupata maana tofauti. Fasiri hizi ziliashiria mitazamo tofauti ya watafitiwa licha ya kusoma mabango sawa. Utafiti huu ulibainisha kwamba baadhi ya watafitiwa hawakuweza kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Asilimia kubwa ya vijana waliofasiri ujumbe kwa njia tofauti na ile iliyotarajiwa walikuwa ni wakufunzi rika. Wakufunzi rika ambao walihusishwa kwenye utafiti huu walikuwa kiwakilishi cha vijana ambao hawana umilisi na tajiriba ya lugha ya Kiswahili. Matokeo haya ni ya kutiliwa shaka kuhusiana na mawasiliano ya mabango kuhusu ugonjwa wa ukimwi katika jamii. Watafitiwa ambao hawakuweza kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa walilalamika kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu na haieleweki kwa haraka. Kulingana nao mabango haya hayajaongeza thamana yoyote kwa vile wao wakiwa baadhi ya hadhira lengwa waling^{“ang”}ana kuelewa ujumbe huo. Watafitiwa hawa pia walikuwa na mtazamo hasi kwani hawakupendelea kusoma mabango ya Kiswahili. Baadhi yao walidai kuwa hawana muda wakusoma mabango hayo. Kukosa kwao kuelewa ujumbe kwenye mabango haya kulitokana na mtazamo hasi waliokuwa nao kuhusu lugha ya Kiswahili. Walikosa umakini wa kuchunguza namna ambavyo ishara za kiisimu zilitumika kuusimba ujumbe kwenye mabango na hivyo kusababisha wao kukosa kuelewa ujumbe jinsi ilivyotarajiwa.

Utafiti huu ulifichua kuwa mabango ya ukimwi yana wingi wa maana. Wingi wa maana huashiria ile hali ambapo ujumbe kwenye bango huzua zaidi ya maana moja. Hali hii husababisha utata. Kulingana na watafitiwa mabango haya yalipasha ujumbe zaidi ya moja. Maana zilizojitozea zilikuwa kadhaa. Watafitiwa walidai kuwa maana hizi zinaweza kuwatatiza wasomaji na kuwafanya wasiweze kupokea ujumbe jinsi ilivyotarajiwa.

Watafitiwa hawa walihitaji kutambua maana ya ujumbe kulingana na muktadha ambamo msamiati huo umetumika na wala siyo kutegemea maana msingi. Hii inamaanisha kuwa maneno ya kawaida yanaweza kutumika katika miktadha mahususi kuzua maana mpya.

Hata hivyo kwa upande mwingine huenda fasiri hizi mabalimbali zilijitokeza kwa ajili ya tamaduni na tajriba tofauti ya maisha miongoni mwa watafitiwa hawa. Hali hii aghalabu husababisha hali inayosababisha fasiri mabalimbali na mitazamo tofauti kuhusiana na ujumbe mmoja. Kutokana na maelezo haya tunatambua kuwa kuna sababu kadha wa kadha ambazo zinaweza kusababisha fasiri mabalimbali za ujumbe husika.

Aidha kuhusiana na mabango ya ukimwi mlengwa vile vile ana jukumu la kufasiri ujumbe jinsi inavyotarajiwa. Kwani hakuna ye yeyote aliyepewa jukumu la kuwafasiria walengwa ujumbe huo. Wao wanastahili kufasiri ujumbe kwenye mabango punde tu wanapoyasoma. Iwapo ujumbe huu hutafasiriwa jinsi inavyotarajiwa basi jukumu la ujumbe halitatimilika. Kwani mpokezi ndiye wa mwisho kuzingatia ujumbe ulioko kwenye mabango.

5.2.2 Mtazamo wa vijana kuhusu mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi

Mtafiti aliweza kujadili mitazamo ya watafitiwa kuhusu mitindo mabalimbali iliyotumika katika mabango husika. Viwango vya semantiki, leksia na grafolojia vilirejelewa. Mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango haya ni pamoja na isitiari, methali, taharuki, taswira, tasfida, mafumbo, kuchanganya ndimi, majazi, kinaya, matumizi ya ishara na kilugha cha sheng.

Utafiti huu ulizidi kuonyesha kuwa mitindo ya lugha ilikuwa kizuizi katika uelewaji wa ujumbe kwa hadhira lengwa. Watafitiwa walihisi kuwa matumizi ya mitindo ya lugha kwenye mabango haya yalisababisha kutolewa kwa ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Watafitiwa hawa walisema kuwa lugha hiyo ni fiche na hivyo ngumu kueleweka kwa wale wasio weledi wa lugha ya Kiswahili. Asilimia hii ilijumuisha wanafunzi wanaosomea kozi ya Kiswahili. Walisema kuwa ujumbe haukueleweka kwa uwazi. Aidha watafitiwa hawa waliyakosoa mabango haya kwa kusema kuwa ujumbe huu ulilenga watu wenye upeo wa juu katika kuielewa lugha ya Kiswahili na wala si vijana wa kawaida ambao wana upeo wa wastani au chini kuielewa lugha ya Kiswahili. Matokeo haya yanaonyesha kwamba licha ya lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya taifa bado kuna watu ambao hawajaimdu vyema. Lugha ya taifa ni lugha ambayo hutumika kwa wingi. Kulingana na majadiliano ya makundi teule, matumizi ya tamathali za usemi yalisababisha kutolewa kwa ujumbe na uibuaji wa maana zilizohitilafiana na maana iliyotarajiwa wakati ambapo msomaji alikosa kutambua matumizi ya mitindo hiyo.

Aidha kutokana na majadiliano ya watafitiwa, utafiti huu ultambua kuwa lugha fiche ilitumika kwenye mabango ya ukimwi kwa minajili ya heshima. Baadhi ya watafitiwa walieleza kuwa matumizi ya tamathali za usemi huenda yametumika ili kuashiria mambo ambayo hayazungumzwi wazi wazi katika jamii kwa minajili ya heshima. Katika tamaduni nyingi za Afrika kuna miiko ya kiisimu ambapo maneno na misemo fulani hairuhusiwi kutajwa hadharani, na iwapo itatajwa itakuwa ni kuwakosea wanajamii heshima. Hivyo basi masuala yanayohusiana na ngono katika jamii nyingi za Kiafrika ni mwiko kuyataja.

Matokeo haya ni ya kutiliwa shaka. Sababu ni kwamba mambo yanayohusiana na ngono ndicho chanzo nambari moja cha usamabzaji wa ugonjwa wa ukimwi miongoni mwa

wanafunzi wa vyuo vikuu. Masuala ya utamaduni yanafaa yawekwe kando ili ujumbe uweze kuangazia masuala kuhusiana na ngono kwa uwazi pasipo kuficha chochote.

Watafitiwa hawa vile vile walihisi kuwa aidha ujumbe ulisimbwa kwa matumizi ya mitindo hii kwa vile ulilenga kundi fulani la watu katika jamii na hivyo kudhibiti hadhira. Matokeo ya utafiti huu yalizidi kuonyesha kuwa matumizi ya mitindo kama vile kuchanganya ndimi na kilugha cha sheng yameathiri matumizi ya Kiswahili sanifu kwa njia hasi. Watafitiwa walilalamika kuwa matumizi ya mitindo hii kwenye mabango ya ukimwi yameathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu kwa njia hasi na kwa kiwango kikubwa sana. Asilimia hii inajumuisha vijana wanaosomea kozi ya Kiswahili. Kulingana nao vijana wengi wanaiga matumizi haya ya lugha na hivyo kupotosha matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili mionganoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Kufikia sasa wanafunzi katika vyuo vikuu wameanza kukipa kilugha cha sheng hadhi. Wanakionea kilugha hiki fahari hata kushinda lugha sanifu ya Kiswahili. Vijana wengi wanapenda kunasibishwa na kilugha cha sheng.

Hata hivyo kuna baadhi ya watafitiwa ambaeo walipendelea sana aina hii ya lugha. Kulingana na wao matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi yanawavutia vijana wengi na kuwasbabisha kujaribu kusoma mabango. Asilimia hii ilijumuisha vijana ambaeo ni wakufunzi rika. Wengi wao waliweza kuelewa ujumbe jinsi ilivyotarajiwa kwa ajili ya matumizi ya mtindo wa kuchanganya ndimi. Wao walihisi kuwa kuchanganya ndimi na matumizi ya kilugha cha sheng kuliwalenga wao kama vijana na hata kufanya ujumbe huo kuwa wa kuvutia.

Kuhusiana na matumizi ya kilugha cha sheng kuna baadhi ya watafitiwa ambaeo hawakuunga mkono matumizi ya kilugha cha sheng. Asilimia hii ilijumuisha watafitiwa ambaeo wanaosomea kozi ya Kiswahili. Kulingana na wao kilugha cha sheng hutumika kimzaha mionganoni mwa vijana na hivyo matumizi yake katika kuwasilisha ujumbe hupunguza uzito wa ujumbe huo na kuwafanya vijana kuchukulia ujumbe huo kimzaha. Matokeo haya ni ya kutiliwa shaka kwani masuala kuhusiana na ukimwi ni mionganoni mwa masuala nyeti katika jamii. Ni lazima tutambue kuwa suala la ukimwi ni tanzia katika jamii. Hili si tatizo ambalo limetengewa sehemu finyu za jamii; linaathiri jamii nzima. Hili si tatizo la mitaani tu bali limeziathiri taasisi mbalimbali, jamaa, maeneo ya kazi, na hata shule. Ni tatizo ambalo limeathiri watu wa kila umri, kuanzia watoto hadi watu wazima. Anayehusika anaathirika kiafya na kisaikolojia. Jamaa yake nayo inateseka kumwona mwenzao akiangamia. Matumizi ya kilugha cha sheng ni sharti yapunguzwe.

Matokeo ya utafiti yalizidi kubainisha namna kilugha cha sheng kimechangia kupotosha baadhi ya maana ya msamiati wa Kiswahili. Majadiliano ya watafitiwa yalionyesha namna msamiati „bamba“ ulivyotumika visivyo. Watafitiwa wote hawakuelewa maana sanifu ya msamiati „bamba.“ Watafitiwa hawa walichukulia msamiati huu kumaanisha „kufurahia“ ilhali ulimaanisha „kubaka“ Sheng hupotosha maana halisi ya maneno katika lugha ya Kiswahili. Matumizi ya sheng vile vile huchangia katika matumizi mabaya ya lugha ya

Kiswahili mionganoni mwa vijana, kwani wengi wao huiga matumizi ya aina hii na hivyo kuathiri matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili. Aidha kuna watafitiwa ambaeo walihisi kuwa siyo kila mtu anawenza kutambua mitindo ya lugha iliyotumika katika mabango ya ukimwi.

Kulingana na watafitiwa hawa kuna wale ambao watatambua matumizi ya mitindo ya lugha ya Kiswahili lakini hawatajua namna ya kuifasiri. Aidha msomaji anaweza kuelewa maana batini iwapo anaelewa muktadha ambamo ujumbe huo umetungiwa na maana batini ndiyo aghalabu inayotarajiwa. Hivyo basi watafitiwa ambao hawakurejelea muktadha husika hawakufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Ni vyema kuelewa kuwa kutokana na maana msingi maneno huhushishwa na maana mbalimbali kutegemea jamii na matumizi ya neno fulani la kimsingi. Watafitiwa walihitaji kutambua maana ya msamati kulingana na muktadha ambamo msamati huo umetumika na wala si kutegemea maana msingi. Sababu ni kuwa maana mpya ya maneno huibuliwa katika miktadha mbalimbali ya lugha. Hii ina maanisha kuwa maneno ya kawaida yanaweza kutumika katika miktadha mahususi kuzua maana mpya.

Isitoshe, utafiti huu umebainisha kuwa mitindo ya lugha imesababisha ujumbe kuwa na wingi wa maana. Baadhi ya mabango yaliwasilisha maana zaidi ya moja kwa ajili ya mitindo ya lugha iliyotumika katika kuwasilisha ujumbe husika. Hali ya wingi wa maana ilisababisha wanafunzi kukosa kuelewa ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Hali hii inapoitokeza huwa ni tatanishi na ngumu kubainisha maana iliyotarajiwa na ujumbe husika.

Kutokana na matokeo ya utafiti imebainika wazi kuwa matumizi ya mitindo ya lugha kwenye mabango ya ukimwi ilisababisha watafitiwa kutofasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Kulingana na matokeo haya ni wazi kuwa mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi hayajaweza kufasiriwa jinsi inavyotarajiwa na baadhi ya walengwa. Matumzi ya baadhi ya mitindo ya lugha ndicho kimekuwa kizuizi katika hali hii. Hata hivyo, mitindo ya lugha iliyotumika iliweza kusababisha msomaji kuwa na uwezo wa kutafakari kuhusu ujumbe uliowasilishwa kwenye mabango ya ukimwi.

5.2.3 Changamoto za matumizi ya lugha zilizodhihirika katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana

Utafiti huu uliweka wazi changamoto zilizodhihirika vijana walipokuwa wakifasiri ujumbe kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi. Changamoto hizi zilisababisha vijana kutofasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Changamoto zilizobainishwa ni pamoja na mitindo ya lugha, maana ya umaanisho, kutosoma ujumbe wote, masuala ya utamaduni, kudharau na kupuuza lugha ya Kiswahili, uhitaji wa ujumbe wa awali na wingi wa maana.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa matumizi ya mitindo ya lugha yaliweza kusababisha kutoelewaka kwa ujumbe na uibuaji wa maana zilizohitilafiana na maana iliyotarajiwa. Hali hii ilijitokeza wakati ambapo msomaji alikosa kutambua matumizi na maana ya mitindo hiyo ya lugha. Aidha watafitiwa walihisi kuwa matumizi ya mitindo mbalimbali ya lugha kwenye mabango haya yalisababisha kutoelewa kwa ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Kuna watafitiwa ambao hawakuelewa maana ya mitindo ya lugha iliyotumika katika kuwasilisha ujumbe kwenye mabango haya. Watafitiwa hawa walilalamika kuwa

matumizi ya mitindo ya lugha yalifanya lugha hiyo kuwa ngumu kuelewaka. Watafitiwa hawa walilalamika kuwa mabango haya hayakupasha ujumbe jinsi ilivyotarajiwa walipogundua kuwa hawangeelewa maana ya baadhi ya mitindo ya lugha iliyotumika. Walisema kuwa wao wanglipenda kuona mabango ambayo ujumbe wake ni wa moja kwa moja. Watafitiwa walieleza kuwa siyo kila mtu angeweza kutambua mitindo ya lugha iliyotumika katika mabango haya. Kulingana nao kuna wale ambao wangeitambua ingawa

hawangejua namna ya kuifasiri. Matumizi ya mitindo hii yalisababisha watafitiwa kufasiri ujumbe kwa njia mbalimbali na hivyo kupotoka kimaana. Ni muhimu kujua kwamba kabla binadamu hajatenda jambo ni vyema alifahamu kwanza. Mabango yalipewa maana mbalimbali kulingana na mtafitiwa binafsi. Hali hii ilisababisha mitazamo tofauti kuhusu matumizi ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi. Ufasiri wa ujumbe ulitegemea aina ya lugha iliyotumika katika kuwasilisha ujumbe huo. Namna mitindo ya lugha na ishara za kiisimu zilivyotumika kuusimba ujumbe kwenye mabango ilichangia kusababisha fasiri mbalimbali mionganoni mwa wanafunzi na hata kusababisha changamoto katika kuelewa kwa ujumbe wa mabango haya kwa wanafunzi.

Katika utafiti huu mtafiti aligundua namna ukosefu wa kutambua maana ya umaanisho ilivyokuwa changamoto katika kuelewa ujumbe wa mabango haya kwa vijana jinsi ilivyotarajiwa. Ujumbe uliopatikana kwenye mabango mengi ulisema mambo fulani na kumaanisha mambo mengine. Watafitiwa hawakuweza kutambua maana ya umaanisho ya ujumbe uliowasilishwa katika mabango haya na hivyo kukosa kufasiri ujumbe jinsi ilivyokusudiwa. Watafitiwa hawa hawakutambua kuwa ujumbe kwenye mabango ulikuwa na maana fiche na hivyo kushindwa kuuelewa jinsi ilivyotarajiwa. Hawakutambua kuwa maana iliyolengwa ilikuwa tofauti kabisa na jinsi ujumbe ulivyokuwa ukisema. Maana hii inafasiriwa tu katika muktadha. Muktadha humfanya msikilizaji au msomaji kuzua umaanisho wa kile ambacho kimeandikwa na mwandishi.

Matokeo ya utafiti huu yализиди kuonyesha kuwa dhana ya kuzingatia kusoma sehemu fulani ya ujumbe na kuacha kusoma sehemu zingine ilichangia pakubwa katika kusababisha vijana kukosa kuelewa ujumbe katika mabango haya. Namna watafitiwa walivyofasiri ujumbe kwenye mabango ilionyesha kuwa walilenga sehemu fulani za ujumbe, kuashiria kuwa walichagua sehemu ambazo walitaka kusoma huku wakipuuza kusoma sehemu zingine za ujumbe uo huo. Mtazamo huu ulisababisha baadhi ya watafitiwa kukosa kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa kwa sababu hawakusoma ujumbe wote mzima. Baadhi ya watafitiwa walidai kuwa aghalabu hawakuwa na wakati wa kusoma mabango.

Utafiti huu ulizidi kuonyesha kuwa kudharau na kupuuza lugha ya Kiswahili kulisababisha hali ya kutoeleweka kwa ujumbe wa mabango na wanafunzi jinsi ilivyotarajiwa. Baadhi ya watafitiwa hawakupendelea kusoma mabango ya Kiswahili haswa wale ambao hawasomei kozi ya Kiswahili. Wao walihisi kuwa lugha ya Kiswahili ni ngumu na haieleweki kwa haraka. Kukosa kwao kuelewa ujumbe kwenye mabango haya kulitokana na mtazamo hasi waliokuwa nao kuhusu lugha ya Kiswahili. Walikosa umakini wa kuchunguza namna ambavyo ishara za kiisimu zilitumika kuusimba ujumbe kwenye mabango na hivyo kusababisha wao kukosa kuelewa ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Huu mtazamo hasi uliathiri namna walivyofasiri ujumbe kwenye mabango ya Kiswahili kwani walikosa umakini wa kuchunguza elementi za kiisimu katika fasiri zao na hivyo kukosa kuelewa ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Aidha kutokana na matokeo ya utafiti ilibainika wazi kuwa kuna mabango mengine ambayo yalihitaji ufahamu wa ujumbe wa awali. Kutokana na majadiliano ya watafitiwa hawa ni wazi kuwa kuna mabango ambayo hayakuwasilisha ujumbe vikamilifu. Dhana ya uchukulio ilijitokeza hapa. Uchukulio ni ile hali ambapo msemajii au mwandishi huwa anachukulia kuwa msikilizaji au msomaji anajua mambo yanayojadiliwa.

Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa aliyeandaa mabango haya alichukulia kuwa walengwa walikuwa wanaelewa masuala aliyokuwa akiyashughulikia. Kwa upande mwagine tunatambua kuwa baadhi ya walengwa hawakuwa na ufahamu wa awali kuhusu masuala yaliyokuwa yakishughulikiwa hali ambayo ilichangia wao kutoweza kufasiri ujumbe jinsi ilivyodhamiriwa.

Utafiti huu ulifichua namna masuala ya utamaduni yalivyochangia katika kusababisha vijana kukosa kuelewa ujumbe katika mabango husika. Katika tamaduni nyingi za Kiafrika kuna miiko ya kiisimu ambapo maneno na misemo fulani hairuhusiwi kutajwa hadharani, na iwapo itatajwa itakuwa ni kuwakosea wanajamii heshima. Masuala yanayohusiana na ngono katika jamii nyingi za Kiafrika ni mwiko kuyataja. Kwa sababu ya masuala haya ya utamaduni, lugha fiche imetumika katika kuashiria masuala ya ngono kuwasilisha ujumbe katika mabango mengi ya ukimwi na hivyo kusababisha changamoto katika kuelewa ujumbe na hadhira lengwa jinsi ilivyotarajiwa. Kwanza kabisa ni vyema kujua kuwa mambo yanayohusiana na ngono ndiyo chanzo nambari moja cha usambazaji wa ugonjwa wa ukimwi mionganoni mwa wanafunzi wa vyuo vikuu. Hivyo basi mambo haya yanastahili kuwekwa wazi ili kila mtu aelewe na hivyo kuchukua au kuweka mikakati inayofaa katika maisha yake.

Aidha utafiti huu ulibainisha namna matumizi ya kilugha cha sheng yamepoteza maana halisi ya baadhi ya maneno ya Kiswahili. Mathalani neno „ubambishe“ limepewa maana tofauti katika sheng nayo ni „kufurahia.“ Watafitiwa wote hawakuelewa maana sanifu ya msamati „ubambishe“ ambao ulipatikana katika bango la B13 lenye ujumbe *‘Jijue ubambishe life.’* Wao walichukulia neno hili kumaanisha „kufurahia“ na hivyo kuufasiri ujumbe huu kuwa *‘Jijue ufurahie maisha.’* Kutokana na mitazamo yao, wao walielewa kwamba ukijua hali yako ya ukimwi una uhuru wa kujiingiza katika anasa na raha za maisha. Neno ‘bamba’ linamaanisha kubaka.

Isitoshe, kutokana na matokeo ya utafiti ilibainika wazi kuwa hali ya wingi wa maana ilisababisha watafitiwa kukosa kutambua maana tarajiwa ya ujumbe kwenye mabango ya ukimwi. Wingi wa maana huashiria ile hali ambapo ujumbe kwenye bango huzua zaidi ya maana moja. Hali hii huzua utata katika ujumbe. Kuna mabango ambayo yalizua zaidi ya maana moja kwa kurejela fasiri za watafitiwa. Hali hii inapojitokeza huwa ni ngumu kubainisha maana tarajiwa ya ujumbe husika.

Aidha matokeo ya utafiti yalidhibitisha kuwa kulikuwepo na changamoto kadha wa kadha ambazo zilisababisha watafitiwa kukosa kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Changamoto hizi zilidhahirika wakati ambapo watafitiwa walikuwa wakifasiri ujumbe kwenye mabango ya ukimwi. Licha ya changamoto ambazo ziliibuka kutokana na namna ambavyo ishara za kiisimu na za sanaa zilivyotumika katika kuusimba ujumbe kwenye mabango haya, kuna pia uwezekano wa tamaduni tofauti na tajriba tofauti za maisha na za usomi kusababisha vijana kuwa na mitazamo tofauti kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi.

5.2.4 Hitimisho

Utafiti huu unadhibitisha kuwa ujumbe kuhusu ukimwi unaowasilishwa kupitia njia ya mabango haujafasiriwa jinsi ilivyotarajiwa na vijana. Binadamu hufasiri ujumbe kwa njia

mbalimbali kutegemea namna wanavyoolewa. Fasiri mbalimbali ziliweza kusababisha ujumbe kukosa kueleweka jinsi ilivyotarajiwa na hivyo kusababisha jukumu la ujumbe huo kutotimilika. Hata hivyo huenda kuna mambo changamano ambayo huchangia hali ya kutoelewa au kutotenda kwa kuzingatia tahadhari kuhusu ugonjwa wa ukimwi. Watu wawili wanaweza kufasiri ujumbe kwa njia tofauti kabisa kwa sababu ya tajriba tofauti ya maisha na tamaduni tofauti. Hivyo basi kuna sababu kadha wa kadha ambazo zinaweza kusababisha fasiri mbalimbali za ujumbe husika.

Aidha, matumizi ya mitindo ya lugha kwenye ujumbe kuhusu ukimwi unaowasilishwa kupitia mabango pia yalichangia katika uibuaji wa fasiri mbalimbali za ujumbe. Vijana walitoa fasiri mbalimbali kwa sababu ya kutoelewa maana ya mitindo ya lugha iliyotumika. Matumizi ya mitindo ya lugha yaliathiri ufasiri kwa sababu iwapo msomaji hakuelewa mitindo ya lugha iliyotumika kwenye bango, maana aliyoibua haikuwa sawa na ya yule msomaji ambaye alitambua mitindo ya lugha iliyotumika. Watafitiwa ambao walitambua mitindo ya lugha iliyotumika waliweza kufasiri ujumbe jinsi ilivyotarajiwa. Maana ni muhimu sana na hivyo inafaa kupewa kipaombele wakati wa kuwasilisha ujumbe. Naam, baadhi ya watafitiwa hawakutambua mbinu za lugha zilizotumika katika kuwasilisha ujumbe kwenye baadhi ya mabango. Hali hii iliwasababisha kutoweza kufasiri ujumbe husika jinsi ilivyotarajiwa.

Isitoshe, kutokana na upambanuzi wa fasiri za vijana kuhusu ujumbe kwenye mabango ya ukimwi, pamoja na kuchanganua mitazamo yao kuhusu mitindo ya lugha iliyotumika mtafiti aliweza kutathmini changamoto za matumizi ya lugha ya Kiswahili zinazodhihirika katika kuelewa kwa ujumbe wa mabango haya. Changamoto hizi zilibainika watafitiwa walipofasiri ujumbe wa mabango kuhusu ukimwi. Kutokana na matokeo ya utafiti huu ni wazi kuwa mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi bado yanahitaji kuundwa upya ili yaweze kuwasilisha ujumbe kwa uwazi ndiposa yaeleweke vema bila usaidizi wowote.

5.3 Mapendekezo

Ili kuimarisha mawasiliano kuhusu ugonjwa wa ukimwi kupitia kwenye mabango yanayotumia lugha ya Kiswahili utafiti huu unapendekeza yafuatayo:

Kwanza lugha nyepesi itumike katika kuwasilisha ujumbe kwenye mabango ya ukimwi. Aina hii ya lugha ikitumika basi itakuwa rahisi kwa wanafunzi kufasiri ujumbe jinsi inavyotarajiwa.

Lugha iliyowazi itumike badala ya lugha fiche. Masuala ya utamaduni yawekwe kando ili ujumbe uweze kuangazia masuala kuhusiana na ngono kwa uwazi pasipo kuficha, kwani mambo haya ndiyo husababisha usambazaji wa ugonjwa wa ukimwi mionganoni mwa vijana kwa asilimia kubwa.

Aidha matumizi ya kilugha cha sheng yapunguzwe kwa vile kilugha hiki hutumika kimzaha mionganoni mwa vijana na hivyo kupunguza uzito wa ujumbe kuhusu masuala yanayohusu ugonjwa wa ukimwi mionganoni mwa wanafunzi. Kwani masuala ya ukimwi ni nyeti katika jamii. Matumizi ya kilugha cha sheng pia huchangia katika matumizi mabaya ya lugha ya Kiswahili mionganoni mwa vijana, kwani wengi wao huiga matumizi ya aina hii na hivyo kuathiri matumizi ya lugha sanifu ya Kiswahili.

5.3.1 Mapendekezo kuhusu utafiti wa baadaye

Mbali na kuchanganua mitazamo ya vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi, utafiti unaweza kufanywa katika sehemu zifuatazo:

Kuchunguza mitazamo ya vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango mengine kama vile ya siasa na biashara.

Kufanya utafiti linganishi kati ya matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza kwa kurejelea mabango ya ukimwi.

Kuchungza lugha ya Kiswahili inayotumiwa kuhamasisha jamii kuhusu ugonjwa wa ukimwi kuitia vyombo vya habari kama vile redio, runiga, magazeti na mtandao.

MAREJELEO

- Agu, I. E. (2008). *A linguistic stylistic analysis of Soyinka's „The interpreters.“* Unpublished thesis, Federal University of Technology, Yola
- Alreck, P.L. (1995). *The survey research handbook*, Homewood 111 Irwin
- Aloo, S. N. (2002). *Uchambuzi wa matangazo ya biashara katika radio na televisheni: mtazamo wa kipragmatiki*: Tasnifu ya uzamili iliyotolewa katika chuo kikuu cha Nairobi, hajachapishwa.
- Andrew, B. & Royle, N. (1995). *Introduction to literature criticism and theory*. London: Pearson Education Limited.
- BAKITA, (2004). *Makala ya siku ya Kiswahili na utandawazi*, Dar es Salaam.
- BAKITA, (2005). *Istilahi za Kiswahili*: Dar es Salaam.
- Bankole, Aderinokun & Denloye, (2005). *Evaluation of a photo-poster on nurses' perceptions of teething problems*. Southwest Nigeria.
- Barthes, R. (1984). „Rhetoric of the image“ in the responsibility of forms (Translated by Heath, S) Oxford: Blackwell.
- Baxter, P. & Jack, S. (2008). Qualitative case study methodology: Study design and implementation for novice researchers. *The Qualitative Report*, 13 (4) 544-559, <http://www.nova.edu/ssssQR/QR13-4/baxter.pdf>
- Berlson, B.C. (1981). *Content analysis in communication research*, New York: Free Press.
- Blamires, H.(1991). *A history literary criticism: Post structuralism or deconstruction*. London: Macmillan, Press Limited.
- Brierley, S. (1995). *The advertising handbook*, London, Routledge.
- Bryman, A.E.(2004). *Social research methods* (2nd Ed), Oxford University Press.
- Bryne, B.(1992). *Relevance theory and the language of advertising*. Ocassional paper No. 31 pp 1-7.
- Chimera, R.M. (1998). *Kiswahili, past present and future horizons*, Nairobi, Kenya: Nairobi University Press.
- Cook, G. (2013). *The discourse of advertising*, Routledge London.
- Cooter, R. & Stein, C. (2010). *Positioning the image of Aids*; Endeavour Retrieved on 2nd August 2015 from US library of medicine, National institute of health. (Pub med).
- Cresswell, J.W. (2003). *Researchdesign: Qualitative, quantitative and mixed methods approaches*, London: Sage Publications.
- Cross, J. & Dubblin, L. (2002). *Implementing e-learning*. U.S.A: American Society for Training and Development.
- Crystal, D. (1996). *The Cambridge encyclopaedia of language*, New York: McGraw-Hill.
- Crystal, D.(2008). *The dictionary of linguistics and phonetics*. UK Blackwell.
- Crystal, D. & Davy, D. (1981). *Investigating English style*. London: Longman Group Ltd.
- Denzin, N.K. (1970). *The research act: a theoretical introduction to sociological methods*, Chicago: Aldine.
- Dyer,G. (1982). *Advertising as communication*. England: Clays Ltd, St. Ives Plc
- Dodd, J.S. (2010). *The ACS style guide: A manual for authors and editors*, 2nd edition. The American Chemical Society.
- Edwards, J. (1985). *Language, society and identity*. Oxford, Basil Blackwell.
- Fairclough, J. (2004). *Discourse analysis*. London: Routlegde.
- Fish, S. (1970). *The authority of interpretive communities*. Cambridge, Havard University Press.

- Forman, L. (2009). *Both medium and message: Hiv/Aids, information and communication in Africa*. University of Toronto, Faculty of Law, Discussion paper, Association for progressive communications.
- Gakahu, N (2015). *Communicating HIV/AIDS among students in Kenya institution of higher learning*: A challenge for the 21st century. Journal of Economics and Sustainable Development.
- Golafshani, N. (2003). *Understanding reliability and validity in qualitative research. The qualitative report*, 8 (4), 597-606. <http://www.nova.edu/ssss/QR/0R8-4/golafshani.pdf>
- Goode, W. & Hatt, J. (1981). *Methods in social research*, Auckland: McGraw- Hill International Books Academy.
- Guowen, H. (2008). *A systematic functional approach to code switching studies: Some Chinese– English examples. Meaning in context: Implementing intelligent applications Of language studies* Ed. Jonathan J. Webster, Jonathan J. Webster and contributors, London.
- Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix.
- Hashim, A. (2010). *English inadvertising. The Routledge handbook of world Englishes*. Routledge, London.
- Hussein, A.(2009). The use of triangulation in social sciences research: Can qualitative and quantitative methods be combined. *Journal of comparative social work*, 1, 1-2. <http://jcsw.no/local/media/jcsw-issue-2009-article.pdf>.
- Iser, W.(1974). *The implied reader*. Baltimare: John Hopkins.
- Johnson, R.B & Onwuebuzie, A. J. (2002). *Mxed method research. A research paradigm. time has come*.Educational research vol 33 no. 7.
- Kimani, H.W. (2006). *Uwiano wa picha na matini katika mabango ya matangazo ya ukimwi; Mtazamo wa kisemantiki* (unpublished M.A Thesis) Nairobi: Kenyatta University.
- Kitsao, J.(1975). *A stylistic approach for the study of written Swahili prose texts*. Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa). Chuo kikuu cha Nairobi.
- Kothari, C.R. (2003). *Research methodology: Methods and techniques*, New Delhi: Vishwa Parkashan.
- Krueger, R. (2000). *Focus groups: A practical guide for applied research*. Thousand Oaks, C.A: Sage publications, Inc.
- Lawal, R.A. (1997). Pragmatics in stylistics: A speech – Act analysis of Soyinka's telephone conversation. Lawal In: *Stylisites in theory and practice*, Ilorin: Paragon books.
- Leech, G.N. (1969). *English in advertising*, London: Longman
- Leech, G.N. & Short, M.H. (1981). *Style in fiction: A linguistic introduction to English Fictional prose*, London: Longman Press.
- Leech, G.N. & Short, M.H (2007). *Style in fiction: A linguistic introduction to English Fictional prose*, (2nd Ed), Edinburgh: Pearson Edcation Limited.
- Local World Health Organization reference centre on HIV/AIDS (2018) *Report on the global AIDS pandemic*, Geneva.
- Lodge, K. (2009). *A critical introduction to phonetics*. London: Continuum.
- Lugwiri, (2011). *Stiari, taashira na tashbiha katika uwasilishaji wa dhamira katika Utensi wa Tambuk a: Uhakiki wa kimtindo*. Tasnifu ua uzamili ambayo haijapishwa, chuo kikuu cha Nairobi.

- Luka, B. (2017). *A linguistic analysis of selected antibiotic information leaflets*, College of Education, Hong, Nigeria.
- Lyons, J. (1981). *Language and linguistics: An introduction*, Cambridge University press.
- Maweja, M. (2002). *Linguistic taboo in African marriage context: A study of Oromo Laguu*: Nordic Journal of African studies.
- Michira, J.N. (1993). „*Uchanganuzi wa kimtindo wa lugha ya wachuuzi wa soko la Gikomba na matangazo ya biashara ya redio*“ Unpublished M.A. Thesis, University of Nairobi.
- Momanyi, C. (2007). *Suala la mielekeo ya lugha. Katika F. E.M.K Senkoro (Mhr), Lugha na fasihi ya Kiswahili Afrika Mashariki. CHAKAMA (uk. 106-113.)* Dar es Salaam, Tanzania: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI).
- Mukhwana, A. (2008) *Isimu jamii*. Nairobi Focus Publishers
- Mutonya (2008). Swahili advertising in Nairobi: Innovation and language shift. *Journal of African cultural studies* vol 1 no. 1 June 1990.
- Mutula, S.M. (2003). *Cyber café industry in Africa*, *Journal of information science*, vol. 29, no.6.
- Morgan, D.L.(1997). *Focus group as qualitative research*: Sage University paper series on qualitative research methods. Vol 19. Beverly Hills, C.A: Sage publications, Inc.
- Mugenda, O.M & Mugenda, A.G. (2003). *Quatitative and quantitative approaches*, Nairobi : Acts Press.
- Muchura, A.W. (2004). „*Textual function of women advertisement magazines*, Unpublished M.A Thesis University of Nairobi.
- Murray, J. (2005). *Success in communication*. London: Stuart Sillars.
- Mutekwa, F.O. (2013). *Uchanganuzi wa kisemantiki wa mabango ya Kiswahili kuhusu suala la afya*. (Unpublished) M.A. Thesis: Maseno University.
- Mwansoko, H.J & Tumbo. (1992). *Matumizi ya Kiswahili Bungeni*, TUKI, Dar es Salaam.
- Mzee.S. (1980). „*Differences in usage between some registers of written Swahili*.“ (Unpublished) M.A Thesis: University of Nairobi.
- Ogusunji, A. (2007). *Aspects of phono-graphological design in Soyinka's fiction*: Lagos: University of Nigeria.
- Okoto, W.L. (2015). *Athari za sheng kwa lugha ya Kiswahili*. Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Nairobi, hajachapishwa.
- Ombogi, J.N. (2003). *Interpersonal function of style in Kenyan newspaper advertisements* (Unpublished) M.A. Thesis: University of Nairobi.
- Ogechi, N.O. (2002). *Trilingual code switching in Kenya: Evidence from Ekegusi, Kiswahili, English and Sheng*, Unpublished Ph.D Thesis, Hamburg University of Hamburg.
- Owino, P. O. (2004). *Study of African universities in response to HIV/AIDS: Case of Kenya*; Report for ADEA, Nairobi, Kenya.
- Partington, A.S. (2009), „„*A linguistic account of word play: The lexical grammar of punning*““ Journal of pragmatics.
- Robin, W. (2009). *The non designers design book*, Peachpit Press, Beckley.
- Ridder, G.J, & Cramer, P. (1994) “*Down to ten: Estimating the effect of a red card in soccer*” Journal of the American statistical Association.
- Samovar, A.L. (1995). *Communication between cultures*, Wadsworth.
- Sharndama, E.C.(2013). *Stylistic analysis of selected political campaign posters*. (Published) M .A Thesis; Federal University.www.ajhss.org Retrieved on 14th May 2016.

- Shartiely, E.N. (2013). *Code-switching in university classroom interaction*, published Phd Thesis, Stellenbosch University.
- Shitemi, N.L. (2001). *Pidginization: Sheng, The melting pot of Kenyan languages and an anti Babel development, Kiswahili*, Vol. 64. Dar es Salaam; Institute of Kiswahili Research.
- Tanaka, K. (1994). *Advertising language: A pragmatic approach to advertisements in Britain and Japan*, Lodon, Routlegde.
- Tompkins, J. (1980). Foundations of behavioural research, New Delhi, Surjeet Publications.
- Tucker, N. (1981). *The child and the book: A psychological and literary exploration*. Cambridge: Cambridge University Press
- TUKI, (2004). *Kamus ya Kiswahili sanifu*, ToleolaPili, Oxford University Press, Nairobi
- UNESCO, (2009). *Evaluation report for universities in Ghana, Rwanda, Botswana and Kenya: Higher education science and curriculum reforms: African universities responding to Hiv/Aids through faculties of science and engineering*.
- Wamitila, K.W. (2000). *Archetypal criticism of Kiswahili poetry*. Bayreuth: Bayreuth African studies.
- Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha fasihi*, Focus Publications Nairobi, Kenya.
- Wamitila, K.W. (2008). Kanzi ya fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa fasihi. Nairobi: Vide-Muwa Publishers.
- Ward, K. & Hawthorne, K. (1995). *Do patients read health promotion posters in the British Journal of general practice BJGP*: Br. J Gen Pract 1994, December.
- White, R. (1995). *Advertising: What is it and how to do it*. 3rd edition, London: McGraw-Hill Companies.
- WHO, (2011). *World health report on the youths and Hiv/Aids*.
- Wilkinson, S. (2004). *Focus group research* in Silverman, D. (ed). *Qualitative research: Theory method and practice*. Thousand Oaks, C.A. Sage.
- Witte, K. (1992). *Preventing AIDS through persuasive communications: A framework for construction of effectively culturally specific health messages*. London: Sage.
- Yakub, A. (2008). *Linguistic analysis of Safaricom advertisements in Kenyan newspapers*. (Unpublished) M.A. Thesis Maseno University.

VIAMBATISHO

KIAMBATISHO 1: FOMU YA KUKUBALI KUSHIRIKI UTAFITI.

UJUMBE KWA MSHIRIKI

MADA YA UTAFITI: Mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi katika vyuo vikuu nchini Kenya.

ENEO LA UTAFITI: Chuo kikuu cha Maseno na chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro.

MTAFITI: Mukoko Alice Khayali.

NAMBARI YA SIMU: 0720343249.

Unaalikwa kushiriki katika utafiti kuhusu mtazamo wa vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe kuhusu ukimwi. Kukubali au kukataa kushiriki katika utafiti huu ni uamuzi wako. Iwapo hutaki kushiriki katika utafiti huu hauhitaji kupeana sababu yoyote. Ukipubali kushiriki katika utafiti huu na kisha uamue kujiondoa baadaye, hakuna shida yoyote. Vile vile hustahili kutoa sababu yoyote na hakuna atakaye kulaumu. Waweza kujiondoa wakati wowote.

Iwapo utakubali kushiriki katika utafiti huu unaombwa kujaza fomu ya „„kukubali kushiriki katika utafiti huu““ ipatikanayo katika ukurasa wa mwisho wa nyaraka hii. Utapewa nakala ya nyaraka hii na nakala ya fomu ya kukubali kushiriki katika utafiti huu.

Nyaraka hii ina kurasa tatu pamoja na fomu ya kukubali kushiriki. Tafadhali hakikisha kuwa umesoma na kuelewa kurasa zote.

LENGO LA UTAFITI HUU.

Lengo la utafiti huu ni kuchunguza mitazamo ya vijana kuhusu matumizi ya lugha kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi pamoja na kueleza umuhimu wa lugha katika kufahamisha masuala ya ukimwi.

SABABU ZA KUCHAGULIWA.

Umechaguliwa kushiriki katika utafiti huu kwa sababu ya nafasi yako kama aidha mwanafunzi anayechukulia kozi ya Kiswahili katika chuo kikuu au kama mkufunzi rika katika chuo kikuu. Utafiti huu utahusisha majadiliano ya wanafunzi wa vyuo vikuu amba ni wakufunzi rika na wale wanaochukulia kozi ya Kiswahili katika makundi teule ya vijana kumi na nne kwa kila kundi. Kila kikao cha makundi haya kitachukua takriban dakika 60 hadi 100. Makundi haya yatakutana mara kadha ili kumwezesha mtafiti kupata data anayohitaji. Kinasa sauti kitatumika katika kunasa majadiliano haya. Tepurekoda hizi zitaharibiwa punde tu utafiti utakapo kamilika.

ATAKAYEGHARAMIA UTAFITI HUU.

Gharama zozote zitakazotokea kwa ajili ya utafiti zitaghamariwa na mtafiti. Mshiriki hatagharamia chochote.

HAKI YA MSHIRIKI.

Mshiriki ana haki ya kujiondoa kushiriki katika utafiti huu wakati wowote bila ya kutoa sababu yoyote na hakuna atakaye mlaumu. Kwa upande mwagine mtafiti atahakikisha uaminifu wa ujumbe na maoni ya mshiriki yatatumika katika utafiti huu pekee pamoja na kuhifadhi siri na maswala ya kibnafsi ambayo huenda yakatokea.

FOMU YA KUKUBALI KUSHIRIKI KATIKA UTAFITI HUU.

Tafadhali weka mkwajo ili kubainisha kukubali kwako kwa yafuatayo.

Nimesoma na kuelewa ujumbe kwa mshiriki. Ndiyo [] La []

Nimepewa muda wa kutosha ili kuweza kutafakari na kufanya uamuzi wa kushiriki au kutoshiriki katika utafiti huu. Ndiyo [] La []

Nimeridhika na maelezo pamoja na majibu ambayo nimepewa kuhusiana na utafiti huu na nina nakala ya fomu hii ya kukubali kushiriki pamoja na nakala ya ujumbe kwa mshiriki. Ndiyo [] La []

Ninafahamu kuwa ni uamuzi wangu kushiriki katika utafiti huu na hivyo naweza kuamua kujiondoa katika utafiti huu wakati wowote na hakuna atakaye nilaumu. Ndiyo [] La [].

Ninafahamu kuwa mtafiti atahakikisha uaminifu wa ujumbe na maoni nitakayotoa kuhusu utafiti huu na kwamba ujumbe huo na maoni hayo yatatumika kwa minajili ya utafiti pekee. Ndiyo [] La []

Ninafahamu wajibu wangu kama mshiriki. Ndiyo [] La []

AZIMIO LA MSHIRIKI.

Ninakubali kushiriki katika utafiti huu.

Jina la mshiriki

Sahihi..... Tarehe.....

AZIMIO LA MTAFITI

Nimemweleza mshiriki kwa utondoti kuhusu utafiti huu. Nimeweza kujibu maswali yote yaliyoulizwa na mshiriki kuhusu utafiti huu na hivyo naamini kuwa bila shaka mshiriki anaelewa mada ya utafiti na amekubali kushiriki katika utafiti huu.

Jina la mtafiti: Mukoko Alice Khayali.

Sahihi..... Tarehe.....

KIAMBATISHO 2: DODOSO ILIYOTUMIKA KUONGOZA MAJADILIANO KATIKA MAKUNDI TEULE.

Mimi ni mwanafunzi wa chuo kikuu cha Maseno. Majina yangu ni Mukoko Alice Khayali. Ninasomea shahada ya uzamili katika lugha ya Kiswahili. Nadharamia kufanya utafiti kuhusu „Mitazamo ya vijana kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi.“ Ninatumia maswali yafuatayo kama mwongozo wa majadiliano katika makundi teule ili kukusanya data ya utafiti. Ni ombi langu kuwa mtaweza kushirikiana nami kujadili maswali haya katika makundi teule ili kufanikisha utafiti huu. Ujumbe na maoni mtakayotoa yatatumika tu kwa minajili ya utafiti pekee yake na wala si kwa madhumuni mengine.

DODOSO YA MWONGOZO WA MASWALI YALIYOTUMIKA KATIKA KUONGOZA MAJADILIANO KATIKA MAKUNDI TEULE.

Ujumbe katika bango hili unamaanisha nini?

Je, kuna mitindo yoyote ya lugha iliyotumika katika bango hili?

Ni nini maana ya mitindo hii kwa mujibu wa ujumbe unaowasilishwa?

Mitindo hii ina umuhimu gani katika kuwasilisha ujumbe huu?

Mitindo iliyotumika katika mabango haya inachangia vipi katika kuzua utata katika matumizi ya lugha ya Kiswahili?

Eleza makosa ya sarufi yanayopatikana katika mabango haya.

KIAMBATISHO 3: ORODHA YA UCHUNZAJI

Orodha ya uchunzaji iliyotumika kutambua mitindo ya lugha iliyotumika kwenye mabango yanayowasilisha ujumbe wa ukimwi katika lugha ya Kiswahili.

BANGO	MTINDO YA LUGHA INAYOPATIKANA KATIKA BANGO.
1.Usilambe asali katika kila nyumba	
2.Usiogelee mto Nyando naked. Vaa CD.	
3.Sisi tumeingia kwa network juu tunajua hali yetu ya HIV.	
4.Jitambue leo.	
5.Bila kondomu = Hakuna mapenzi.	
6.Uwanja mdogo, tuliza boli. Kamdudu kako. Tumia CD.	
7.Ati bila CD afadhali ikae!	
8.Chunga usipate red card. Vaa CD.	
9.Valia boots usidungwe na mwiba.	
10.Ukimwi si ajali bali ni msiba wa kujitakia.	
11.Mwanangu ngoja kwanza, la sivyo jikinge kila wakati. Fungua roho yako, ongea.	
12.Si hutest regularly kujua status yetu. Bila worries life inabamba.	
13.G-jue ubambishe life.	
14.Mwanzo na mwisho wa mawazo, G-jue hali yako ya HIV. Tu-meet VCT centre au hosy karibu na mtaa.	
15. Mwanamume kamili hujua sataus yake.	

KIAMBATISHO 4 : SEHEMU MABANGO YALIPATIKANA

B1 : USILAMBE ASALI KATIKA NYUMBA – MASINDE MULIRO UNIVERSITY

B2: USIOGELEE MTO NYANDO NAKED, VAA CD – MASINDE MULIRO UNIVERSITY

B3 : SISI TUMEINGIA KWA NETWORK JUU TUNAJUA HALI YETU YA HIV-MASENO

B4 : JITAMBUE LEO - MASINDE MULIRO UNIVERSITY

B5 : BILA KONDONU, HAKUNA MAPENZI – MASENO

B6: UWANJA MDOGO KAMDUDU KAKO. TUMIA CD – MASENO

B7: ATI BILA CD AFADHALI IKAЕ - MASINDE MULIRO UNIVERSITY

B8 : CHUNGA USIPATE RED CARD , VAA SEAT BELT - MASINDE MULIRO UNIVERSITY

B9 : VALIA BOOTS, USIDUNGWE NA MIMBA- MASINDE MULIRO UNIVERSITY

B10 : UKIMWI SI AJALI BALI NI MSIBA WA KIJITAKIA – COUNTY HOSPITAL KAKAMEGA

B11: MWANAGU NGOJA KWANZA, LA SIVYO JIKINGE KILA WAKATI, FUNGUA ROHO YAKO ONGEA- MASENO

B12: SI HU-TEST REGULARLY KUJUA STATUS YETU, BILA WORIES LIFE INABAMBA- MASENO

B13: JIJUE UBAMBISHE LIFE – MASENO

B14: MWANZO NA MWISHO WA MAWAZO, G-JUE HALI YAKO YA HIV TU-MEET VCT CENTRE AU HOSI KARIBU NA MTAA – COUNTY HOSPITAL KAKAMEGA

B15: MWANAUME KAMILIHUJUA STATUS YAKE YA HIV CHUKUA TEST LEO - MASINDE MULIRO UNIVERSITY

KIAMBATISHO 5: MPANGILIO WA KAZI

Mpangilio wa kazi ya utafiti kwa mwaka 2016-2018

Mwaka	Mwezi	Kazi
2016	Mei-Julai	Maandalizi ya suala la utafiti
2016	Agosti- November	Kuchunguza mapitio ya maandishi
2016	Disemba	Kuandika pendekezo la utafiti
2016/2017	Desemba – Januari	Masahihisho ya pendekezo la utafiti
2017	Feburuari	Wasilisho la pendekezo la utafiti
2017	Machi – Aprili	Kusahihisha pendekezo baada ya wasilisho
2017	Mei – Juni	Utafiti maktabani
2018	Februari	Ukusanyaji data
2018	Machi	Kuandika nakala ya kwanza ya tasnifu
2018	Aprili	Kuwasilsha nakala ya kwanza ya tasnifu
2018	Mei	Masahihisho
2018	Juni	Kuwasilisha nakala iliyorekebishwa
2018	Julai	Marekebisho ya mwisho
2018	Agosti	Kutetea tasnifu.

KIAMBATISHO 6: BAJETI

Vifaa vya utfiti	Bei ya vifaa
Vifaa vya kuandikia	10,000
Usafiri	5,000
Upigaji na utoaji picha	10,000
Uchapishaji	20,000
Mtandao	5,000
Malazi na chakula	15,000
Vitabu	5,000
Jumla	70,000

KIAMBATISHO 7: KIBALI CHA UTAFITI



MASENO UNIVERSITY ETHICS REVIEW COMMITTEE

Tel: +254 057 351 622 Ext: 3050
Fax: +254 057 351 221

Private Bag — 40105, Maseno, Kenya
Email: muerc-secretariate@maseno.ac.ke

FROM: Secretary - MUERC

DATE: 30th August, 2019

TO: Alice Khayali Mukoko
PG/MA/00041/2013
Department of Kiswahili and Other African Languages
School of Arts and Social Sciences
Maseno University
P. O. Box, Private Bag, Maseno, Kenya

REF: MSU/DRPI/MUERC/00680/19

RE: Mtazamo wa Vijana Vyuo Vikuu Kuhusu Matumizi ya Luga ya Kiswahili kwenye Mabango Yanayowasilisha Ujumbe wa Ukimwi Nchini Kenya. Proposal Reference Number MSU/DRPI/MUERC/00680/19

This is to inform you that the Maseno University Ethics Review Committee (MUERC) determined that the ethics issues were adequately addressed in the initial proposal. Consequently, the study is granted approval for implementation effective this 30th day of August, 2019 for a period of one (1) year. This is subject to getting approvals from NACOSTI and other relevant authorities.

Please note that authorization to conduct this study will automatically expire on 29th August, 2020. If you plan to continue with the study beyond this date, please submit an application for continuation approval to the MUERC Secretariat by 15th July, 2020.

Approval for continuation of the study will be subject to successful submission of an annual progress report that is to reach the MUERC Secretariat by 15th July, 2020.

Please note that any unanticipated problems resulting from the conduct of this study must be reported to MUERC. You are required to submit any proposed changes to this study to MUERC for review and approval prior to initiation. Please advise MUERC when the study is completed or discontinued.

Thankyou.

Dr. Bernard Guyah
Ag. Secretary,
Maseno University Ethics Review Committee.



Cc: Chairman,
Maseno University Ethics Review Committee.

MASENO UNIVERSITY IS ISO 9001:2008 CERTIFIED



KIAMBATISHO 2: ITHIBATI YA WAKUFUNZI RIKA NA WANAFUNZI
WA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA MASINDE MULIRO

MASINDE MULIRO UNIVERSITY OF SCIENCE AND TECHNOLOGY

Tel: 056 – 2031375/2030056
Fax: 056 – 30153
E-mail: vc@mmust.ac.ke
Website: www.mmust.ac.ke



P. O. Box 190
KAKAMEGA
50100
Kenya

Office of the Dean of Students

MMU/COR/5500010

19Th January 2019

Chairman
Department of Kiswahili &
Other African Languages
Maseno University
Private Bag
Maseno

Dear Madam,

Re: Research - Mukoko Alice Khayali

The above named student has informed us that she is your student pursuing a masters degree in the "Role of the Swahili Language in Controlling HIV/AIDS Pandemic among the youths".

She would like to use Masinde Muliro University of Science and Technology Peer Educators and Kiswahili student to assist in her research. This is to confirm that we currently have 265 active peer educators, and 1340 Kiswahili students

Thank you.

Yours faithfully,

M. Grace Muango
Mrs. Grace Muango
Senior Student Student Counselor